# Nipashe

Jumanne Februari 25, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580163

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Serikali yatangaza kiama, yaanza msako mkali wa madalali 'vishoka'

UKURASA 3




UKURASA 13

# Adhabu 5 zawakabili Membe, Kinana CCM

**MBIVU**, mbichi kujulikana Jumamosi, ripoti yao kutua rasmi Kamati Kuu... *Endelea ukurasa wa 2*



## NDAMA WA MAAJABU AIBUA TAHARUKI

UKURASA 3

Mkazi wa Kijiji cha Ngiresi, Kata ya Sokoni 2, katika Halmashauri ya Arusha, Eliakimu Mongasi, akiwaonyesha wanahabari ng'ombe wake ndama, aliyezaliwa akiwa na midomo miwili na macho matatu, hivyo kuwa gumzo kwa wakazi wa halmashauri hiyo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play | Download on the App Store


# Mwandishi Kabendera amalizana na serikali

UKURASA 2


MICHEZO | YANGA: HESABU SASA KWA AZAM SI SIMBA UK. 32 | MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Adhabu 5 zawakabili Membe, Kinana CCM

Na Augusta Njoji, DODOMA

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM), inatarajia kufanya kikao chake wiki hii ili kutoa uamuzi kuhusu ripoti ya uchunguzi wa tuhuma za utovu wa nidhamu zinazowakabili makatibu wakuu wastaafu, Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ametaja adhabu tano ambazo huenda vigogo hao watakumbana nazo ikiwa watapatikana na hatia za kukiuka taratibu za chama hicho.

Februari 12 mwaka huu, kamati hiyo ilitoa siku saba kwa Kamati Ndogo ya Udhibiti na Nidhamu, inayoongozwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Philip Mangula, kukamilisha taarifa inayowahusu wanachama hao na kuiwasilisha katika vikao husika.

Kwa mujibu wa Dk. Bashiru, kama watatu hao wakikutwa na hatia ya kuvunja kanuni za maadili, watapewa adhabu ambazo ni pamoja na kufutwa uanachama, kusimamishwa kwa muda, kupewa onyo, onyo kali au karipio.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini Dodoma wakati akipokea madiwani 11 kutoka Jiji la Mbeya waliohamia CCM, Dk. Bashiru alisema kamati hiyo ndogo imemaliza kazi yake na kesho itawasilisha taarifa yake kwa Kamati ya Usalama na Maadili na baadaye kuwasilishwa kwa Kamati Kuu ya chama mwishoni mwa wiki hii.

"Kamati kuu itakaa mwishoni mwa wiki hii kwa ajili ya kupokea ripoti ya Mzee Mangula, ilitakiwa kutolewa Februari 19, lakini imechukua muda kutokana na Mzee Mangula kuwa na kazi aliyopewa na Kamati Kuu.

"Uamuzi wa chama ni kwamba taarifa ya kina Mzee Mangula ipo tayari kwa kuwasilishwa kwenye vikao, baada ya vikao utamwona (Hamprey) Polepole atazungumza kuwa wamepatikana na hatia gani na kwa adhabu gani," alisema.

Alipoulizwa kuhusu adhabu watakazokumbana nazo vigogo hao endapo wakikutwa na hatia, Dk. Bashiru alisema adhabu hutolewa baada ya mtuhumiwa kusikilizwa, kujitetea na vikao kuchambua na kutoa uamuzi.

Hata hivyo, alisema: "Kwa hapa sijajua hadi vikao vitoe uamuzi."

Dk. Bashiru alidokeza adhabu mbalimbali ambazo hutolewa kwa wanaovunja kanuni za maadili ya CCM kuwa ni pamoja na kupewa onyo, akifafanua kuwa adhabu hiyo huwa haitangazwi licha ya kuthibitika mtu amevunja kanuni.

"Adhabu nyingine ni onyo kali ambayo inatangazwa hadharani na pia unaweza kukosa haki fulani za uanachama na kuwa chini ya uangalizi," alisema.

Alitaja adhabu ya tatu ni karipio ambalo alieleza kuwa ni kali kuliko onyo kali na mwanachama anayeangukia kwenye adhabu hiyo hupewa haki fulani na kukosa haki fulani huku akiwekwa chini ya uangalizi ili ajirekebishe.

"Adhabu nyingine ni kuachishwa uanachama, hapo unaacha uanachama unaenda kuwa raia huru, lakini unaweza kuomba upya uanachama, ukajiunga kwa mujibu wa taratibu za kanuni. "Kama ni kiongozi, unaweza ukasimamishwa kwa muda, kuachishwa uongozi, hizi ni adhabu hutolewa baada ya mtuhumiwa kusikilizwa, kujitetea na vikao kuchambua na kutoa uamuzi. Kwa hapa sijajua hadi vikao vitoe uamuzi," alisema.

Mwishoni mwa mwaka jana, sauti zilizodaiwa za baadhi ya watuhumiwa hao zilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii, wakidaiwa kupanga njama za kuuhujumu uongozi wa chama hicho.



Rais John Magufuli akikabidhi zawadi ya kinyago cha Umoja, kwa msomi na mwanajumuiya kutoka Kenya, Prof. Patrick Loch Otieno Lumumba maarufu zaidi Prof. PLO Lumumba, baada ya mazungumzo yao, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Hatimaye Kabendera, serikali wamalizana

Na Hellen Mwango

MWANDISHI wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, amehukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, kulipa faini na fidia ya Sh. milioni 273 baada ya kukiri makosa yaliyokuwa yakimkabili, likiwamo la kutakatisha fedha na kukwepa kodi.

Vilevile, mahakama hiyo imemhukumu Kabendera kulipa faini ya Sh. 250,000 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miezi mitatu baada ya kukiri kosa la kukwepa kodi.

Mshtakiwa tayari ameshalipa Sh. milioni 100, faini ya Sh. 250,000 na mahakama imemtaka kulipa Sh. milioni 173 ndani ya miezi sita kuanzia jana kwa mujibu wa makubaliano yake na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Hukumu hiyo ilisomwa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Janeth Mtega, aliyepangwa kusikiliza kesi hiyo.

Mshtakiwa aliingia makubaliano na DPP kuomba msamaha na kukiri mashtaka yaliyokuwa yanamkabili.

Awali, upande wa mashtaka ulimfutia shtaka la kuongoza genge la uhalifu na kumsomea mashtaka ya kutakatisha fedha na kukwepa kodi.

Hakimu Mtega alisema katika kosa la kwanza la ukwepaji kodi, mshtakiwa atatakiwa kulipa faini ya Sh. 250,000 au kifungo cha miezi mitatu jela. Pia atatakiwa kulipa fidia ya Sh. milioni 173.

Alisema katika kosa la pili la utakatishaji fedha, mshtakiwa atatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 na kusisitiza kuwa adhabu hizo zinajitegemea, hivyo kila adhabu itakwenda peke yake.

Kabendera alilipa faini ya Sh. 250,000 na anatakiwa kulipa Sh. milioni 273 ambazo tayari ametanguliza malipo ya Sh. milioni 100, akitakiwa kumaliza Sh. milioni 173 ndani ya miezi sita kuanzia jana.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu, Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alidai mtuhumiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na hawana kumbukumbu ya makosa ya nyuma, hivyo aliiomba mahakama itoe adhabu kulingana na makubaliano yaliyofanyika.

Wakili wa Mshtakiwa, Jebra Kambole, alidai kukiri makosa yake kumeipunguzia muda mahakama kuendesha mashtaka, ana familia na ndugu wanaomtegemea na pia ni zaidi ya miezi sita sasa amekaa mahabusu.

Alidai hali ya mshtakiwa kiafya si nzuri na akaomba katika kosa la kwanza alipe faini ya Sh. 250,000 kwa mujibu wa Sheria ya Kodi na alipe faini kwa kosa la pili pia.

Akisoma makubaliano ya mshtakiwa huyo na DPP, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai wameingia makubaliano na mshtakiwa huyo baada ya kukiri kosa la utakatishaji fedha na ukwepaji kodi, hivyo DPP ameamua kumwondolea kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Baada ya kusoma makubaliano hayo, Hakimu Mtega alimwapisha mshtakiwa na kumuuliza kama alitia saini kwa hiari yake na kudai alifanya hivyo kwa hiari yake.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Nchimbi alisema kati ya Januari Mosi 2010 na Julai 29, 2019, mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu kwa kuingia mikataba isiyo halali na watu wengine ambao wapo nje ya Tanzania, wakiwamo watu maarufu ambao hawakuwa mahakamani.

Alidai mshtakiwa alikubali kufanya makosa ikiwa ni pamoja na kughushi, kukwepa kodi na utakatishaji fedha ambayo yanachangia kudidimiza uchumi.

Nchimbi alidai Machi 23, 2010 kampuni ya Kabendera iliyosajiliwa kama Voxy Media Center (T) Ltd na Wakala wa Usajili (Brela) na Januari 11, 2016, mshtakiwa pamoja na mkewe, Loy Kabendera, walisajili Kampuni ya Sitrep Company Limited na katika usajili huo, walighushi fomu mbalimbali na kuonyesha ofisi ya kampuni hiyo inapatikana kwenye nyumba namba 13 kitalu namba 23 Mbweni Mpiji Kinondoni ambayo ni nyumba yao ya kuishi.

Alidai mshtakiwa huyo pia katika mkakati wake wa kiuhalifu, alitoa taarifa za uongo kwa maofisa wa serikali kwa lengo la kuidanganya serikali na kujipatia fedha kwa njia ya uhalifu.

Nchimbi alidai Aprili 2, 2016, mshtakiwa huyo pamoja na mkewe walifungua akaunti mbili za fedha katika benki ya CRDB, moja ikiwa ya fedha za kigeni, pia mshtakiwa alifungua akaunti yake binafsi.

Alidai Januari Mosi, 2015 alipokea Dola za Marekani 230,358.83 kutoka kwa washtakiwa wenzake kupitia akaunti yake binafsi ambazo zilitoka kwa watu mbalimbali ikiwamo Kampuni ya K2 Intelligence Ltd, Palladium (Tanzania) Ltd, Sitrep Co. Ltd, Eurasia Group Ltd, International Crisis Rou na taasisi zingine za kigeni.

Nchimbi alidai Januari Mosi 2015 na Agosti 29, 2019, mshtakiwa na mkewe Loy, wakiwa wakurugenzi wa Kampuni ya Sitrep, walipokea Dola za Marekani 432,000,541 na Paundi 119,000,130 na katika kipindi chote hicho hawakuwahi kulipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Wakili huyo alidai mshtakiwa aliwaambia maofisa wa Jeshi la Polisi kuwa hajapokea fedha zozote kinyume cha taratibu kutoka katika vyanzo visivyo halali.

Pia, alidai mshtakiwa huyo alikataa kutoa taarifa zozote za benki na kampuni ya Sitrep.

Nchimbi alidai uchunguzi wa awali ulionyesha mshtakiwa huyo alijihusisha na shughuli za kihalifu na kufuatia uchunguzi huo, alifunguliwa mashtaka mbele ya mahakama hiyo ambayo baadaye alikiri kuyafanya.

Akisoma mashtaka mapya, Wakili Simon alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari Mosi 2015 na Agosti 29 2019, Kabendera alikwepa kodi ya Sh. 173,247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe TRA.

Katika shtaka la pili, Kabendera alidaiwa kutakatisha Sh. 173,247047.02 huku akijua fedha hizo ni mazalia ya kosa la ukwepaji kodi.

**AZUNGUMZIA MAISHA YA MAHABUSU**

Saa 9:47, Kabendera alipoachiwa rasmi kutoka mahabusu ya Mahakama ya Kisutu baada ya kukamilisha taratibu za mahakama hiyo, alizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa baada ya kutoka mahabusu alikoishi miezi saba, jana ameanza rasmi kuomboleza kifo cha mama yake mzazi.

"Leo nimeanza rasmi kuomboleza kifo cha mama yangu mzazi, nawashukuru wanataaluma wenzangu, Watanzania wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuhakikisha anazikwa na kupunzishwa kwenye nyumba yake," alisema Kabendera.

Alisema anakusudia kumtafuta mmoja baada ya mwingine walioafanikisha safari yake ya mwisho ya mama yake.

Akizungumzia Jeshi la Magereza, Kabendera alisema analishukuru jeshi hilo kwa jinsi walivyomhudumia alipoingia gerezani alikuwa mgonjwa sana, lakini wamempa huduma tofauti na alivyoyokuwa akiwafikiria.

"Ninawashukuru sana wanataaluma, ndugu na marafiki zangu kwa kuwa pamoja na mimi katika kipindi kigumu nilichowahitaji kuliko wakati wote," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Msako wa madalali 'vishoka' waanza rasmi

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema kuanzia sasa hakuna dalali atakayeendesha shughuli hizo bila kujisajili na kuwa na leseni.

Kauli hiyo ilitolewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, wakati akizindua mfumo wa utoaji leseni za udalali na uendeshaji minada kwa njia ya kielektroniki, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema tayari shughuli hizo ni rasmi na wanaotakiwa kuziendesha ni waliosajiliwa pekee na kwamba wamejipanga kuanza kufanya oparesheni katika kila mtaa maeneo mbalimbali nchini kuwakamata madalali ambao hawajajisajili

Pia alisema madalali feki wote watakaokuwa wanakamatwa kufanya shughuli hizo bila kuwa na leseni, watakuwa wanatangazwa kwenye vyombo vya habari.

"Kama unajiita ni dalali na unafanya shughuli hizo bila kujisajili, mwisho wako umefika, serikali tuna mbinu mbalimbali za kufanya shughuli zetu, tutapita huko mitaani kwenu tutawakamata na hatutakuwa na huruma, tutakutana nao mahakamani Kisutu," alisema James.

"Wanatapeli watu kwa muda mrefu, wamesababisha hata wale waaminifu ambao wamejisajili na kulipa kodi serikalini nao waonekane ni matapeli, ilifika wakati hata kwenye familia mtu mmoja akiwa dalali, familia yote inadharaulika, sasa huu ni mwisho wao, hii sekta ni rasmi kama zilivyo nyingine,"

Katika uzinduzi huo, Katibu Mkuu huyo alisema usajili kwa sasa umerahisishwa na kwamba watajisajili kwa njia ya mtandao kupitia komputa au simu za mkononi katika mikoa wanayoishi badala ya kusafiri mpaka Dodoma kama ilivyokuwa zamani

"Mfumo huu utasaidia kufahamu taarifa sahihi za madalali na pia kufahamu na kuwabaini kwa urahisi wanaofanya shughuli hizo bila kujisajili,"alisema James

Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za serikali kutoka Wizara hiyo, Choto Sendo, alisema idadi ya madalali wanaotakiwa kujisajili ni wote wanaofanya shughuli hizo ikiwamo wanaoendesha minada ya hadhara kwa Tanzania Bara, ukusanyaji wa madeni, ushuru, tozo, udalali wa mahakama, nyumba, viwanja na mwingineo unaofanana na huo

Mkurugenzi Mtendaji wa Yono Action Mart, Scholastika Kevela, aliipongeza serikali kwa kupiga mafuruku madalali feki kuwa walichangia ionekane ya kitapeli

Pia alisema kwamba wako tayari kuisaidia serikali kuwafichua madalali feki wote ili kuhakikisha hakuna anayefanya shughuli hizo bila kujisajili



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James (kushoto), akizungumza na wawakilishi wa madalali pamoja na wahakiki mali wa mikoa Tanzania Bara, kabla ya kuzindua Mfumo wa Kieletroniki wa Utoaji Leseni za Udalalli na Uendeshaji wa Minada ya Hadhara Tanzania Bara, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WFM**

# Ndama wa ajabu azua taharuki

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

WAKAZI wa Kijiji cha Ngiresi Kata ya Sokoni 2 katika Halmashauri ya Arusha mkoani hapa, wameingiwa na hofu baada ya kuzaliwa kwa ng'ombe mwenye vichwa viwili, midomo miwili na macho matatu.

Hali hiyo imewashangaza wanachi hao kwa kile walichodai kuwa haijawahi kutokea wala hawajawahi kusikia imeotokea sehemu yoyote.

Aidha hali hiyo imewafanya wanakijiji kujitokeza kwa wingi kwenda kushuhudia ndama huyo alivyozaliwa, hali iliyomfanya mmiliki wa mnyama huyo kuzuia watu kwenda kumtazama.

Akizungumza na Nipashe, mmiliki wa ng'ombe huyo, Eliakimu Mungasi, alisema wakati anapewa taarifa ya ndama huyo alipata mshtuko kwa kuwa nijambo ambalo halijawahi kutokea katika maisha yake.

Mungasi alibainisha kuwa ng'ombe huyo alizaliwa Februari 3, mwaka huu na hadi sasa ana siku 23.

Alisema ng'ombe aliyemzaa ndama huyo ni uzao wake wa tano na kwamba awali alizaa salama na ng'ombe wenye afya lakini imemshangaza katika uzao wa safari hii.

"Watu wanasema mengi sana. Wengine wanasema ni uchawi wengine wanasema ni laana ya mababu. Lakini mimi sijali ninachokijua ni mpango wa Mungu na tutaendelea kumtunza hadi hapo atakapokufa," alisema Mungasi.

Mke wa mmiliki wa ng'ombe huyo, Elizabeth Mungasi, alisema yeye ndiye alikuwapo wakati ndama huyo anazaliwa na alishitushwa kuona mnyama wa aina hiyo lakini alivumilia na kumpokea.

"Kwani ukizaa mtoto kilema unaweza kumuua? Sasa mimi kama mama nitamlea na nitakaa naye hadi pale ndama huyu atakapokufa. Tuliita daktari akaja akamwona akatuambia hana jinsi ya kutusaidia, kwa hiyo tukae naye hadi pale atakapokufa. Ndama huyu hawezi kula kitu tunachofanya ni kumkamulia maziwa na kumnyesha,"alisema.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Arusha, Charles Ngiroriti, alisema jambo kama hilo ni kawaida kutokea kwa wanyama.

Alibainisha kuwa katika utungaji wa kiumbe, inaweza kutokea chembe zikagawanyika kama vile zilitaka kutengeneza viumbe viwili lakini zikishindwa kugawanyika na kufika mwisho ndiyo anatokea kiumbe kama huyo.

Ngiroriti alisema hali hiyo haiusiani na imani za kishirikina, hivyo watu waache kuzusha maneno na waone ni hali ya kawaida kutokea.

Pia alisema mgawanyiko kama huo unaweza kufikia sehemu viungo vingine vifanye kazi na vingine kutofanya kazi, hivyo ndama huyo anaweza kukaa muda mrefu au mfupi.

## Bashiru: Katiba Mpya mchakato, ajenda endelevu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk.Bashiru Ally, amesema mchakato wa Katiba mpya ni ajenda ya kudumu ya wananchi na haiwezi kufa licha ya kutekwa na wanasiasa wenye uchu wa kuingia Ikulu.

Akijibu swali la mwandishi kuhusu mchakato huo wakati akipokea madiwani 11 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wa Jiji la Mbeya waliohamia CCM, Dk. Bashiru alisema kuna watu wanadhani ukiibua mchakato huo inalipa kama ilivyokuwa mwaka 2015.

"Ninawajua watu wavivu wa kufanya siasa za ushindani. Wanatafuta viajenda hivi ambavyo vitawapa kiki. Hii ni ajenda muhimu lakini tumejadili tangu miaka ya 1980 na hii Katiba ya mwaka 1977 tumejadili sana na kuna mapinduzi makubwa yamefanywa ikiwamo kujumuisha haki za binadamu pamoja na mfumo wa vyama vingi mwaka 1992.

"Mwaka 2015 watu walidhani ajenda ile itawapeleka Ikulu wakaidandia Ukawa (Umoja wa katiba ya Wananchi), ajenda ya wananchi kuvishwa na vyama vya watafuta Ikulu ilionyesha mchakato ule ulidandiwa na watu wanaotafuta Ikulu," alisema.

"Ndio maana hawakupata Katiba mpya wala Ikulu na hili ndiyo kikwazo kikubwa tunapoingia kujadili masuala ya kitaifa, wanasiasa ndio wa kwanza kudandia ikiwamo mimi kwa sababu kwa sasa ni mwanasiasa," aliongeza.

Alisema jambo la wananchi wanasiasa wanatafuta namna ya kuligeuza na kuwa jambo lao.

"Mchakato ukavunjika wakapanda treni inaitwa Ukawa wakateka ajenda ya wananchi. Ikulu hawakuingia na Katiba haikupatikana. Hiyo Ukawa ingekuwa binadamu haina macho, masikio, miguu na mikono.

"Kama ajenda ya UKAWA ingekuwa ya kudumu si wangeendelea kuwa wamoja? Lakini baada ya Ikulu kugoma ngoma ikagoma ya Ukawa wengine wakaenda ACT, wengine wakabaki CUF ya Lipumba," alisema.

Alibainisha alipozungumza katika kipindi cha dakika 45 alisema ajenda ya katiba mpya ni ya wananchi na haiwezi kufa kwa sababu ya wanasiasa.

"Kuandika katiba mpya ni mchakato si maudhui, inaandikwa na nani inashirikishaje wananchi, ukisikiliza wanaosema katiba mpya wanasema tume huru, nchi yetu hii ina eneo la ardhi na uhuru wananchi kunufaika na rasilimali ardhi ni jambo kubwa kuliko Tume huru,"alisisitiza.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Taasisi za Serikali na Binafsi wa Benki ya NMB, William Makoresho, alipotembelea banda la NMB katika maonyesho yaliyokwenda sambamba na Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania wa Mwaka 2020 jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hukumu ya kina Mbowe Machi 10

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imepanga Machi 10, mwaka huu, kutoa hukumu ya vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe na wenzake wanane na kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Vincent Mashinji wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi.

Uamuzi huo ulitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Mbali na Mbowe na Mashinji, wengine ni, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Katibu Mkuu Chadema na Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee; Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Hakimu Simba alisema sheria inaelekeza pande zote mbili Jamhuri na utetezi kufanya majumuisho ya mwisho ili kuisaidia mahakama kutoa uamuzi kwa kuangalia masuala ya kisheria yaliyoibuliwa wakati wa usikilizaji wa kesi hiyo.

Alisema wametoa maelekezo kwa pande zote kuwasilisha hoja zao baada ya mahakama kukamilisha uchapaji wa nyaraka zilizopo kwenye kesi hiyo na kuwagawia mawakili wa pande zote.

"Kesi hii inamvuto kwa jamii ni lazima iishe ili kila mmoja aweze kuendelea na shughuli zake. Majumuisho ya mwisho mnatakiwa muyawasilishe siku tano za kazi, kwa njia ya maandishi, mwenendo wa kesi hii una kurasa zaidi ya 1,000 ambazo natakiwa kupitia na kutoa hukumu, hivyo hukumu ya kesi hii itatolewa Machi 10, mwaka huu asubuhi," alisema Hakimu Simba.

**MDEE AMPUUZA MASHINJI**

Kabla ya kesi hiyo kuanza, Dk. Mashinji alikutana na viongozi wa Chadema ikiwa ni siku chache tangu alipohamia CCM.

Awali, mahakamani hapo Dk. Mashinji ambaye alifika na kuanza kusalimiana na viongozi mbalimbali wa Chadema wakiwamo washtakiwa wenzake, Mdee alikataa kupokea mkono, huku akiendelea kuchezea simu yake ya mkononi kama vile hakuna mtu mbele yake.

Aidha, washtakiwa hao walionekana kumtenga Dk. Mashinji, hivyo kubaki peke yake tofauti na ilivyokuwa awali kabla hajahamia CCM.



Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo ulita mashahidi wanane na mahakama iliwaona washtakiwa wote kuwa na kesi ya kujibu, kujitetea pamoja na kuleta mashahidi wanne.

Mwaka 2018, viongozi hao walifikishwa mahakamani hapo wakikabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kufanya mkusanyiko usiohalali uliosababisha kifo cha mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT), Akwilina Akwiline.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Faraja Nchimbi alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Wilbard Mashauri (sasa Jaji wa Mahakama Kuu), kuwa washtakiwa kwa pamoja walitenda makosa hayo Februari 16, mwaka huo maeneo ya Viwanja vya Buibui pamoja na barabara ya Kawawa Mkwajuni wilayani Kinondoni, Dar es Salaam.

Katika mashtaka ya kwanza la kula njama, kwa pamoja inadaiwa Februari Mosi na 16, 2018, Dar es Salaam walikula njama pamoja na wenzao ambao hawapo mahakamani walikula njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali, mkusanyiko wenye ghasia na kukiuka tamko kutawanyika.

Ilidaiwa pia Februari 16,2018 katika viwanja vya Buibui na Mwananyamala Kinondoni washtakiwa hao wakiwa wamekusanyika na azima ya pamoja, waliitekeleza kwa kufanya mkusanyiko usio halali na kusababisha watu waogope kuwa watakwenda kupelekea uvunjifu wa amani.

Kadhalika washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Februari 16,2018 walifanya mkusanyiko wenye ghasia, wanadaiwa kuwa siku hiyo katika viwanja vya Buibui Mwananyamala na barabara ya Kawawa Kinondoni kwa pamoja na wenzao 12 ambao hawapo mahakamani walitekeleza mkusanyiko ama maandamano yasiyo halali wakiwa na lengo la kuvamia ofisi ya mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni na kuleta hofu ya uvunjifu wa amani.

Nchimbi alidai kuwa Februari 16, 2018 katika barabara ya Kawawa Kinondoni Mkwajuni washtakiwa hao wakiwa na wenzao 12 ambao hawapo mahakamani walikiuka tamko la kuwataka kutawanyika la Ofisa wa Polisi, SSP Gerald Ngiichi kwa kugoma kutawanyika na kupelekea uvunjifu wa amani ambao ulisababisha hofu na hatimaye kifo cha Akwilina na majeruhi kwa askari wawili ambao ni Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi.

## Kampuni za simu zaagizwa kujenga minara haraka

**Na Futuna Seleman, KILWA**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amezitaka kampuni za simu za mkononi zilizopewa ruzuku na serikali ya kujenga minara ya mawasiliano ili wananchi wapate huduma hiyo haraka.

Amesema serikali ipo kazini saa 24 katika kutekeleza Ilani ya CCM ili kuhakikisha wananchi wote wa mjini na vijijini wanapata mawasiliano ya uhakika.

Nditiye aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mavuji, Kata ya Mandawa, wilayani Kilwa mkoani Lindi, juzi wakati wa uzinduzi wa mnara wa mawasiliano uliojengwa na kampuni ya simu ya Tigo baada ya kupewa ruzuku na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), kujenga mnara huo ambao amesema hadi sasa asilimia 95.2 ya wananchi wanawasiliana nchini.

"Mawasiliano hayabagui, hayachagui serikali inatoa ruzuku kwa kampuni za simu za mkononi kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa ajili ya kujenga minara ya mawasiliano ili wananchi waweze kuwasiliana muda wote kwa hiyo mfanye kazi wakati wowote bila kuweka masharti eti hamjajiandaa, serikali ipo kazini, hapa kazi tu," alisema Nditiye.

Alisema serikali inafanya kazi bila kujali itikadi za vyama vya siasa bali inahakikisha wananchi wanawasiliana na serikali inataka wananchi watumie simu kuwasiliana.

"Niwatoe hofu wananchi msiogope maneno yetu ya bungeni ya wabunge wa vyama tofauti wenyewe tukitoka nje ya Bunge tunaongea na kunywa chai pamoja," alisema Nditiye.

Mwenyekiti wa Bodi wa UCSAF, Dk. Joseph Kilongola, alisema kuwa mfuko huo kwa kushirikiana na wawekezaji, kampuni za simu za mkononi wanahakikisha kuwa wananchi wanafikiwa na huduma za mawasiliano kwa kuwa ni haki yao.

Mbunge wa Kilwa Kusini, Selemani Bungala, aliishukuru serikali kwa kujenga mnara wa mawasiliano na kuwa sasa kijiji cha Mavuji wananchi wanawasiliana kwa kupiga simu wanavyotaka tofauti na zamani ilikuwa mpaka wakajitege ili kupata mawasiliano.

Mkurugenzi wa Tigo mikoa ya Pwani, Christopher Mutalemwa, alisema kuwa kampuni za simu zimepata fursa ya kufikisha huduma za mawasiliano kwa wananchi baada ya serikali kuunganisha nguvu na kujenga minara kwa kuwa maeneo mengine kampuni za simu haziwezi kupeleka mawasiliano peke yao mpaka washirikiane na serikali.

# NGS yaanza kulipa deni la pamba

**Na Happy Severine, BARIADI**

WIKI mbili tangu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Simiyu, kuitaja Kampuni ya NGS ya Mjini Bariadi, ambayo ilikuwa miongoni mwa kampuni zilizonunua pamba mwaka jana kuwa na usumbufu kulipa madeni ya wakulima na tozo nyingine, hatimaye kampuni hiyo imeanza kulipa deni hilo.

Takukuru iliitaja kampuni hiyo kuwa inadaiwa Sh. bilioni 3.173 deni la wakulima, ushuru wa halmashuari na vyama vya msingi vya ushirika na idadi kubwa ya wakulima walikokuwa wakidaiwa ni kutoka Wilaya ya Itilima na Bariadi mkoani humo.

Akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kaimu Mkuu wa Taasisi hiyo, Alex Mpemba, alisema kampuni hiyo imelipa Sh. bilioni 1.389 kwa awamu ya kwanza huku ikiendelea kukamilisha taratibu nyingine za kumalizia deni hilo.

Mpemba alisema viongozi wa kampuni hiyo wametoa ahadi Takukuru kuwa ndani ya wiki mbili kuanzia jana watakamilisha deni lote lililobaki Sh. bilioni 1.784 kwa ajili ya kulipa Amcos 60 zinazomdai pamoja na ushuru wa halmashauri.

"Hadi Februari 21 kampuni hiyo ililipa deni hilo la awali, na ambalo limebaki tumewekeana makubaliano ndani ya wiki mbili litakuwa tayari limelipwa, tuna imani na viongozi wa kampuni hii kuwa watatekeleza makubaliano haya," alisema Mpemba.

Taasisi hiyo imesema kuwa katika kuhakikisha kampuni zote zilizonunua pamba zinalipa madeni, waliona kutumia njia ya mazungumzo kwanza kabla ya kuanza kutumia sheria na nguvu zaidi.

Kampuni nyingine ambazo zinadaiwa ushuru wa Halmashuari na Amcos huku zikiwa zimekamilisha kulipa deni la wakulima, ni Biosustain, Gaki Investment, Ick, Lugeye, Matongo, Nsagali na deni linalodaiwa likiwa ni Sh. bilioni 2.228.

Takukuru imesema wanatarajia kabla ya kufika kwa muda wa ununuzi wa pamba msimu wa mwaka huu, kampuni zote nane zinazodaiwa mpaka sasa zitakuwa zimelipa madeni yao.



Sehemu ndogo ya Barabara ya Sewa, iliyokuwa ikijengwa kwa kiwango cha zege katika eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaam, ikiwa haijamaliziwa kujengwa kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vijana kufaidika na ajira kupitia mafunzo miradi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WATANZANIA hasa vijana wa kike wameshauriwa kujitokeza na kuchangamkia miradi, mafunzo na fursa mbalimbali zinazolenga kuwajengea uwezo wajasiriamali kwa kuwa eneo hilo ni umuhimu katika kuzalisha ajira, maendeleo ya jamii na kuinua uchumi wa taifa.

Wito huo umetolewa na Rais wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Jinsia wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Dk. Samwel Kabote, wakati wa mafunzo ya mpango wa kuendeleza vijana, wajasiriamali na wavumbuzi Tanzania hususani vijana wa kike.

Mafunzo hayo yalifanyika chuoni hapo kwa kuwakutanisha vijana walio kwenye mradi wa mafunzo ya ujasiriamali kutoka Tanzania, Kenya, Uganda na Marekani.

Mradi huo unatekelezwa na SUA kwa kushirikiana na vyuo vikuu vingine vya Jimbo la Michigan nchini Marekani, Nairobi cha Kenya na Chuo Kikuu cha Kyambogo cha nchini Uganda na kuwakutanisha vijana wajasiriamali walio kwenye mradi huo ili kubadilishana uzoefu wa mbinu walizojifunza.

Dk. Kabote, alisema kuwa taarifa iliyotolewa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka 2017 inaonyesha kuwa asilimia 12.7 ya Watanzania walikuwa hawana ajira na chuo kimekuwa na jitihada binafsi za kuanzisha ushirikiano na vyuo vingine duniani.

Rais wa Ndaki ya Sayansi za Jamii na Jinsia, Dk. Kabote, alisema lengo la ushirikiano huo ni kuwezesha utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali hususani kwa vijana wa kike ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

"Sisi Ndaki ya Sayansi za Jamii na Jinsia ni mkono wa chuo kikuu hiki katika masuala yote yanayohusiana na mambo ya jinsia," alisema Dk. Kabote.

Dk. Kabote alisema mashamba ya mfano yamekuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo ikiwamo juisi na mikate kupitia Idara ya Sayansi ya Chakula na Teknolojia.

Naye Mratibu wa Kituo cha Masuala ya Taaluma za Insia ambao ndio waratibu wa mradi huo kwa upande wa Tanzania, Dk. John Jeckoniah, alisema mpango huo unahusisha wajasiriamali wote vijana wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 25 hadi 40 ambao wameajiriwa au wamejiajiri wenyewe.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Theresia Jacob, alisema mkulima anaweza kuuza si bidhaa pekee iliyotoka moja kwa moja shambani bali pia kuna uwezekano wa kuuza bidhaa iliyosindikwa.

Mwisho.

# Mwongozo mabaraza ya biashara sasa waja

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imezindua mwongozo wa mabaraza ya biashara ya mikoa na wilaya namna ya kuendesha majadiliano kati ya sekta za umma na binafsi.

Imeelezwa kuwa mwongozo huo utasaidia kutatua changamoto wanazokabiliana nazo wafanyabiashara na wawekezaji nchini.

Mwongozo huo umeandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kwa udhamini wa Investment and Enterprise (Engine) na Mradi wa kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC) kwa lengo la kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya serikali na sekta binafsi.

Akizungumza baada ya kuzindua mwongozo huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, alisema utawezesha sekta hizo kufikia maazimio yenye tija na maendeleo kwa taifa.

"Mwongozo utasaidia sekta binafsi kuunga mkono maono au azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi imara na wenye nguvu. Sekta binafsi ndiyo injini kwa serikali kujenga maendeleo ya ukuaji wa uchumi," alisema Mhagama.

Alisema serikali ina kila sababu ya kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa sekta binafsi kukua na kutoa mchango stahiki katika maendelea ya uchumi na jamii.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, kati ya mikoa 26 Tanzania Bara, ni mikoa 16 ilikuwa na mabaraza hai wakati huo huo wilaya nyingi zilikuwa pengine hazina baraza wala kufanya mkutano wa baraza.

Alisema labda kutowapo kwa mwongozo ilikuwa sababu ya mabara hayo kutokuwa hai.

"Natoa miezi mitatu kwa kila mkoa kuleta taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mabaraza ya biashara nchi nzima kwa ngazi ya mkoa na wilaya," alisema Jafo.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, aliwambia wajumbe kuwa mabaraza yalikuwa hayajajipanga vizuri ndiyo maana yalishindwa kufikia malengo yaliyo kusudiwa kama kutatua changamoto za wafanya biashara na wawekezaji.

"Mwongozo huu mpya unatoa uhalali, utaratibu na mahitaji ya kufuata ili baraza liwe hai. Miongozo hii inatoa pia masharti namna ya kuunga mkono kifedha kwa kila baraza ambapo sekta za umma na binafsi kwa pamoja zinachangia gharama za uandaaji wa mikutano," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tusihujumu miundombinu kushinikiza kupewa huduma

KATIKA toleo letu la jana tuliripoti habari kwamba wakazi wa Kijiji cha Lipumburu, Kata ya Lipumburu, Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wamekata na kuangusha nguzo ya umeme kwa kutumia msumeno wakishinikiza kijiji chao kupatiwa huduma ya umeme wa Mpango wa Umeme Vijijini (REA).

Kufuatia tukio hilo ambalo linadaiwa kutokea mwishoni mwa wiki katika kijiji hicho, Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Masasi ikiongozwa na Mkuu wa wilaya hiyo, Selemani Mzee, ilikwenda katika kijiji hicho kujionea tukio hilo na kufanya mkutano wa hadhara na wanakijiji.

Mzee alieleza kuchukizwa na kitendo hicho na kueleza kuwa serikali haitakivumilia na kwamba wahusika lazima wabainike na wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Alitoa saa 24 kwa wanakijiji kuhakikisha wanawatafuta na kuwabaini wahusika kisha kutoa taarifa serikalini ili hatua za kisheria zichukuliwe mkondo dhidi ya wahusika.

Mzee alisema kitendo hicho cha kukata na kuangusha nguzo ya umeme ni wazi kwamba kina lengo la kurudisha nyuma jitihada za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Kwamba zipo njia sahihi ambazo kama wananchi wanakuwa na malalamiko wanaweza kuzitumia ikiwamo kukutana na viongozi wao wa vijiji na kata kufikisha kero au malalamiko walionayo badala ya kutumia njia ambazo sio rafiki na hazina tija kwao.

Mzee alisema kuharibu miundombinu kama njia ya kufikisha ujumbe kwa wahusika au kupinga jambo linalowakabili kamwe hakuwezi kumaliza malalamiko yao bali ni kutaka kupambana na serikali.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, alidai kuwa kwa muda mrefu waliahidiwa kupatiwa umeme kwenye kijiji hicho, lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa licha ya kusimikwa kwa nguzo katika kijiji hicho. Alidai zaidi kuwa jitihada za uwekaji umeme zimekuwa zikifanyika katika kijiji jirani na kijiji chao.

Kimsingi, kitendo walichokifanya ni cha hujuma, kwa sababu haiwezekani wananchi waharibu kwa makusudi miundombinu ambayo serikali imetumia fedha za walipakodi kuigharamia.

Kosa hilo ni la jinai na wahusika wote hawapaswi kuachwa hivi hivi bali wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria ili hatua zichukuliwe, na wakikutwa na hatia walipe gharama za uharibifu.

Haiwezekani watu wafanye wanavyotaka bila kujua kuwa fedha iliyopotea ingeweza kugharamia huduma nyingine muhimu kwa wananchi wenye mahitaji mbalimbali.

Tukio hili linapaswa kuwa fundisho kwa wananchi wengine kuwa huduma kwa jamii hazidaiwi kwa shinikizo ikiwamo kuharibu miundombinu ya serikali. Kinachotakiwa kufanyika ni kutumia vikao au kuwatumia wawakilishi wao pale wanapoona wamecheleweshewa huduma hizo kama maji, umeme, barabara na nyinginezo.


Wananchi wanapaswa kujua kuwa serikali ina utaratibu wa kuwapelekea huduma na kwamba upelekeji huo ni mchakato unaotegemea na upatikanaji wa fedha baada ya bajeti kuidhinishwa.

Jambo la msingi kwao ni kusubiri, pale wanapoona kuwa kuna ucheleweshaji watumie utaratibu unaokubalika, ukiwamo wa kutumia vikao kuulizia kwa mamlaka husika.

Kama kila kijiji, kitongoni, mtaa au kata wakazi wake watahujumu miundombinu kama njia ya kushinikiza kupatiwa huduma za jamii basi itakuwa ni vurugu, hivyo serikali haitasita

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



# Watoto waliolelewa kikamilifu ni tija kitaifa

Na Gwamaka Alipipi

ZAIDI ya nusu ya idadi ya Watanzania ni watoto. Hivi sasa, kuwekeza kwa watoto kunanufaisha si familia nyingi pekee bali jamii na ni kwa mustakbali wa Tanzania.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inadhihirisha kuwa Tanzania ina idadi ya watu milioni 45, kati yao asilimia 44 ni wenye umri chini ya miaka 15.

Ili kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati inawezekana iwapo watoto wetu watakuwa na afya, wenye kupata lishe bora, elimu bora na kulindwa dhidi ya vurugu, udhalilishaji na unyonyaji.

Kila nchi iliyofikia kuwa na maendeleo ya kiuchumi ya kipato cha wastani imewekeza kwa watoto kwa kiwango kikubwa.

Hivi sasa kuwekeza kwa watoto kwenye elimu bora, huduma za afya zilizoboreshwa na kuwalinda watoto dhidi ya vurugu na udhalilishaji huzaa matunda yanayosababisha kuwapo kwa uchumi imara, kupungua kwa uhalifu na kuwapo kwa familia zenye afya bora na zilizolelewa kwenye maadili bora.

Vilevile endapo serikali ikianzisha utaratibu wa kuhakikisha kila mtoto anayezaliwa anafunguliwa bima ya afya itasaidia kwa kiasi kikubwa kumwezesha mtoto huyo kukua katika afya iliyo bora na malezi mazuri.

Maendeleo makubwa yanaweza kupatikana kwa kuzihamasisha jamii zetu, kuongeza uwajibikaji na uwazi na kuhakikisha kuwa sheria ya watoto inatekelezwa kikamilifu ili kuwalinda watoto wetu.

Matumizi mazuri ya rasilimali zilizopo kwa kuboresha huduma muhimu na kuimarisha fursa kwa watoto kutaziwezesha familia nyingi kujitoa katika umaskini.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto Duniani (Unicef) zinaeleza vifo vya watoto vimepungua nchini kwa asilimia 25, na Tanzania inaendelea vizuri kuelekea kwenye lengo la maendeleo ya milenia kuhusiana na uhai wa watoto.

Hata hivyo zaidi ya watoto 445 waliochini ya umri wa miaka mitano hufariki kila siku, na zaidi ya watoto 140 kati yao ni watoto walio na umri chini ya mwezi mmoja.

Kadhalika, kila saa moja kuna mwanamke anayefariki kwa kutokana na matatizo ya mimba au kujifungua, hivyo serikali inapaswa kuwekeza kwenye huduma za afya nafuu ambako kutaokoa maisha ya maelfu ya wananchi.

Serikali inahitajika kuweka mfumo bora zaidi wa afya utakaokuwa na wafanyakazi zaidi, vituo vya afya vyenye vifaa vya kutosha, ufuatiliaji na usimamizi mzuri na uwajibikaji mkubwa, sera, sheria, miongozo na miundo yote inayohusiana na afya, itoe kipaumbele kwa wanawake na watoto.

Matukio ya ukatili dhidi ya watoto yamekuwa yakishamili kila siku, tumekuwa tukiyasikia kupitia vyombo vya habari, mara mtoto kachomwa moto mikono au mara utasikia kafichwa kwenye boksi kwa miaka mine.

Jamii inapaswa kutambua na kujua uthamani wa mtoto kwa kuwalea na kuwatunza vizuri, kwani ukimlea mtoto kimaadili leo, kesho atakuwa hazina yako.

Watoto wengi wenye ulemavu wananyimwa haki ya kupata elimu, wengi hufungiwa ndani na kuwekwa katika mazingira ya kikatili.

Sheria zinazohusiana na watu wenye ulemavu zinapaswa kukamilishwa na kutekelezwa, wahisani washirikishwe ili kuhakikisha kunakuwapo na bajeti kwa ajili ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa chombo cha uratibu.

Upatikanaji wa huduma maalumu za watoto wenye ulemavu unapaswa kuzidishwa, ikiwa ni pamoja na mipango ya jamii ya kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida, vituo vya huduma vya matibabu mahusisi na kuwa na wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ili watoto wote wenye ulemavu waweze kupatiwa huduma muhimu za kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida, pamoja na vifaa wanavyovihitaji.

Aidha, serikali inapaswa kukumbuka kuwa ule msemo usemao mtoto ni taifa la kesho umepitwa na wakati, bali mtoto ni taifa la sasa na mtoto umleavyo ndiyo akuavyo.

## BARUA/MJADALA

# Tumieni miwani kuzuia mwanga unaoua macho

*MHARIRI naomba niseme jambo kuhusu afya ya macho ambayo Watanzania wengi tunaipuuza.*

*Kitaalamu mara nyingi kumulikwa na mwanga mkali kwa muda mrefu machoni husababisha sehemu ya mbele ya jicho kuharibika.*

*Hali hiyo, husababishwa na mwanga mkali unaoweza kutokana na umeme wakati wa kuchomea au kukata vyuma. Husababishwa pia na kumulikwa na taa kali wakati wa kupiga picha.*

*Unaweza kuathirika na mwanga wa radi iwapo ukipita karibu yako, lakini mionzi ya jua inaweza kuleta tatizo hilo au unapomulikwa na taa kali za mwanga wa umeme au gesi.*

*Aidha, hata mwanga wa taa za gari wakati wa usiku unachochea sana kuharibu macho, maana unakuta dereva wa gari nyingine anawasha taa 'full' kiasi kwamba dereva aliyepembeni yake hawezi kuona mbele kutokana na mwanga mkali wa taa.*

*Suala hili ni hatari sana na linatakiwa lizingatiwe, macho ni kila kitu katika maisha yanapaswa kutunzwa kwa kuepuka miale ya jua au wanga mkali unaosababishwa na vyanzo mbalimbali.*


*Wakati mwingine hata mwanga wa kompyuta nao huathiri macho kutokana na matumizi ya muda mrefu, hivyo wananchi wachukue tahadhari kulinda macho yao.*

*Ndiyo maana nataka kuwashauri wanaofanyakazi kwenye mwanga mkali, wanaotembea juani muda wote, wapiga picha kwenye matukio hata waendesha magari yakati za usiku watumie miwani ya kulinda macho yao.*

**Ni Mike Mbowe**
**Dar es Salaam.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz




# Jamii ijifunze kutoa taarifa uharibifu wa miundombinu

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya majukumu muhimu ya wananchi ni utunzaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao ambayo imewekwa kwa ajili yao ili iweze kuwanufaisha sasa na vizazi vijavyo.

Ni aibu badala ya kuwa walinzi wanajamii wanageuka kuwa waharibifu wa miundombinu na mambo mbalimbali ya huduma za jamii yaliyoko kwenye maeneo yao. Ndiyo mana wananchi wamekuwa wakielimishwa ili kutambua wajibu huo, lakini baadhi yao hawatambui jukumu hilo na wanadhani kwamba hawawajibiki kutunza na kulinda miradi hiyo katika maeneo yao.

Badala yake wanapoona imeharibika au kuna watu wanaiharibu, hawatoi taarifa kwenye mamlaka husika, ili hatua za kurekebisha au kuwakamata waharibifu zichukuliwe haraka.

Katika mazingira ya aina hii, kuna uwezekano wa miradi mingi kuendelea kuharibika au kuharibiwa huku wakishuhudia bila kuchukua hatua kana kwamba hawajapewa elimu ya kutoa taatifa.

Kwa mfano bomba la maji linaweza kupasuka na kusababisha maji mengi kupotea, lakini hakuna anayejali wala kuchukua hatua za kutoa taarifa kwenye mamlaka husika ili mafundi wafike kumaliza tatizo.

Lakini kinachofanyika ni watu kubeba ndoo nyingi kwenda kukinga maji yanayomwagika, huku wakidai kwamba wakitoa taarifa watayakosa, hivyo ni bora wawe kimya, ili waendelee kufaidi.

Hatua hii inasababisha upotevu mkubwa wa maji na kuinyima serikali mapato na kuongeza gharama za uendeshaji ambazo ni pamoja na umeme pamoja na kemikali zinazotumiwa kusafisha maji, hivyo ni vyema sasa jamii ikatambua kuwa inatakiwa kutoa taarifa inapoona hali kama hiyo au uharibu wa aina yoyote.

Wale wanaouza maji mitaani, nao ni wafaidika wakubwa na inawawia vigumu kutoa taarifa, kwa vile wanajua kwamba wakifanya hivyo watayakosa, na kujikuta hawapati fedha zinazotokana na maji, ambayo hawakuyalipia.

Wiki mbili zilizopita, bomba la maji lilipausuka maeneo ya Malamba Mawili Dar es Salaam ikiwa ni sherehe kwa baadhi ya wakazi wa eneo hilo kubeba ndoo na vidumu ili kujaza maji bila kujali kwamba wanatakiwa kutoa taarifa.

Baadhi walisikika wakisema, hawaoni sababu ya kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) wakati wamepata maji ya bure.

Wanaongeza kuwa na kwamba hata kama hali hiyo ingeendelea siku zote, kwao ni sawa tu kwa vile wanapata maji na kumaliza shida kubwa ya huduma hiyo inayowakabili.

Kwa hali kama hii ni wazi kwamba inawezekana wapo, ambao wako tayari kuharibu miundombinu mbalimbali ili wapate vya bure, hali ambayo inaweza kuwakatisha tamaa hata wafadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ninaamini kwamba suala la utoaji taarifa kwa mamlaka husika pale miundombonu mbalimbali inapoharibika au kuharibiwa, siyo geni masikioni mwa Watanzania, lakini inashangaza kwa nini limekuwa na ugumu.

Wananchi wamekuwa wakielimishwa na kutakiwa kutoa taarifa pale wanapoona kuna uharibifu wa miundombinu kwenye maeneo yao, ili hatua za kudhibiti hali hiyo zichukuliwe, lakini baadhi yao hawafanyi hivyo.

Badala yake uharibifu huo unageuka kuwa faida kwao na kuacha kutoa taarifa kwa mamlaka husika bila kujali kwamba mwisho inaweza kuwa hasara kwao iwapo wataendelea kunyamaza.

Kwa mfano katika taarifa ya hali ya utoaji huduma ya majisafi na uondoaji taka na mipango iliyopo mkoani Dar es Salaam iliyowahi kutolewa na serikali, ilionyesha changamoto mbalimbali katika utoaji wa huduma hiyo muhimu.

Miongoni mwa changamoto hizo ni wizi wa maji, uharibifu na wizi wa miundombinu ya majisafi na majitaka na kuchangia kwa kiasi kikubwa cha maji yasiyolipiwa zaidi ya asilimia 45.

Umefika wakati sasa wananchi kutambua jukumu hilo, kwamba wanawajibika kutoa taarifa pale wanapoona kuna tatizo au uharibifu wa miundombinu kwenye maeneo yao kuliko kufurahia.

Ni kweli kwamba jiji la Dar es Salaam lina changamoto ya kutopatikana kwa maji ya kutosha yanayokidhi wingi wa wakazi wake, lakini hilo lisiwe sababu ya kuruhusu uharibifu wa miundombinu.

Kuna miradi miundombinu mingi ya maendeleo, lakini hii ya maji imekuwa ikionewa zaidi, kufuatia wananchi kunyamaza kimya pale wanapoona bomba limepasukia na kumwaga maji mitaani.

Hawaoni kwamba ni hasara kwao, badala yake inageuka kuwa neema, ambayo mwisho wa siku wanaweza kujikuta wakikosa huduma hiyo muhimu, kwa sababu ya uzemve au makusudi.

Wakati wakifanya hivyo kwenye maji, linapotokea tatizo la kukatika au uharibifu wa miundombinu ya umeme huwa ni wepesi wa kulalamika pale mafundi wanapochelewa kufika kufanya marekebisho.


Kwenye suala la maji, hata mafundi wasipofika kurekebisha tatizo, wanaona ni jambo la kawaida, kwa vile wanajichotea bure, lakini linapotokea tatizo kukatika kwa umeme kwa siku moja tu malalamiko yanakuwa ni mengi.

Utasikia wakidai kwamba wametoa taarifa tangu siku fulani, lakini bado mafundi hawajafika, lakini hatua hizo za kutoa taarifa hazifanyiki pale linapotokea tatizo la kupasuka kwa bomba la maji.

Wananchi kunyamazia uharibifu wa miundombinu ya maendeleo ni sawa na kujikwamishia maendeleo yao wenyewe, hivyo ni vyema wakabadilika na kuchukua hatua zinazostahili.

## KABWELA

NA FADHILI MOHAMMED



# JPM, Prof. Lumumba wateta mazito Dar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, jana alikutana na kufanya mazungumzo na msomi na Mwanajumuiya wa Afrika, Prof. Patrick Loch Otieno Lumumba, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu ilisema Rais Magufuli na Prof. Lumumba ambaye ni raia wa Kenya, walizungumzia masuala mbalimbali yahusuyo juhudi za Afrika katika kuimarisha uchumi kwa kutumia rasilimali zake.

Pia taarifa hiyo ilisema walizungumzia wajibu wa Waafrika na viongozi wao katika kuimarisha huduma za kijamii na kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Magufuli alimpongeza Prof. PLO Lumumba kwa juhudi zake za kueleza waziwazi makosa yanayosababisha nchi za Afrika kubaki nyuma kiuchumi, kijamii na kisiasa, wajibu wa viongozi na wananchi wa Afrika katika kukabiliana na changamoto zinazozikabili nchi zao na mapenzi yake makubwa kwa Afrika.

Rais Magufuli alimweleza juhudi ambazo serikali yake inazifanya katika kujenga uchumi imara wa kujitegemea ikiwamo utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa Bwawa la Nyerere litakalozalisha megawati 2,115 za umeme.

Miradi mingine ni kuongeza usambazaji wa umeme kutoka vijiji 2,018 hadi 8,587, ujenzi wa barabara na madaraja makubwa na madogo, kutoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari, kuongeza mikopo ya elimu ya juu, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kudhibiti rasilimali muhimu ya madini na kupambana na rushwa.

"Mimi sijawahi kukutana nawe kabla, lakini nakusikia na kukuona kupitia vyombo vya habari unavyopaza sauti kuhusu Bara la Afrika. Nakupongeza kwa juhudi hizo na ninafarijika kwamba unaisemea vizuri Afrika," alisema Rais Magufuli.

Naye Prof. Lumumba, taarifa hiyo ilisema, alimshukuru Rais Magufuli kwa kutenga muda wake kuzungumza naye na alimpongeza kwa juhudi kubwa alizozionyesha katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake.

Prof. Lumumba alisema Rais Magufuli ameonyesha mfano wa namna ya kupigania rasilimali za nchi ikiwamo madini, kujenga nidhamu ya utumishi serikalini, kuimarisha uchumi, kupambana na wizi wa mali za umma, rushwa na ufisadi.

Prof. Lumumba alisema inafaa kwa nchi za Afrika kujifunza mambo yanayofanyika Tanzania kwa sasa na kusisitiza kuwa ni muhimu kwa Waafrika kujiamini na kuchukua hatua madhubuti za kuwaondoa katika hali ya sasa, ambapo rasilimali zake zinachukuliwa na mataifa ya nje ilhali wananchi wake wakikabiliwa na changamoto mbalimbali.

Wakati huo huo, Rais Magufuli alikutana na Mwakilishi wa Kansela wa Ujerumani anayeshughulikia masuala ya Afrika, Guenter Nooke, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Nooke aliwasilisha ujumbe wa Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel na pia alielezea kufurahishwa kwake na hatua kubwa za maendeleo zilizofikiwa hapa nchini ikilinganishwa na alipokuja mara ya mwisho miaka ka iliyopita.



Mchuuzi wa vinywaji baridi akiwa amejipumzisha wakati akisubiri wateja ambao asilimia kubwa ni abiria wa kwenye vyombo vya moto katika taa za kuongozea magari za Ubungo External, katika barabara ya Mandela jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: JOHN BADI**

# Hasunga asema vijana wana nafasi pekee kukuza uchumi

**Na Mwandishi Wetu, SONGWE**

WAZIRI wa Kilimo amesema vijana wana nafasi katika kukuza uchumi kwa kutumia ardhi nzuri iliyopo kupitia kilimo kutokana na mazingira wezeshi yaliyowekwa na serikali na wadau.

Hasunga alisema hayo jana mjini Vwawa, Mbozi mkoani Songwe wakati akizindua kongamano la kitaifa la kujadili fursa za kilimo kwa vijana.

Aliwaambia vijana kuwa sekta ya kilimo imetoa ajira kwa Watanzania asilimia 58 na imechangia asilimia 30 ya mapato yatokanayo na mauzo ya nje, hivyo kuwa na fursa nzuri ya kukuza uchumi.

"Katika nchi yetu vijana wako milioni 16.1 sawa na asilimia 35 ya idadi ya watu wote takribani milioni 55," alisema Hasunga.

Waziri pia alisema sekta ya kilimo imechangia asilimia 28.2 ya pato la Taifa na kwamba sekta ndogo ya kilimo inayojumuisha mazao ya biashara, bustani na mazao mengine (nafaka, mikunde na mazao ya mafuta) ilichangia kwa asilimia 16.2 ya pato la taifa kwa mwaka 2018.

Aliongeza kuwa uwapo wa nguvu kazi ya vijana ni fursa nzuri ya kutumia ardhi kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kupata malighafi za viwanda na chakula.

Hasunga aliwafahamisha vijana kuwa Tanzania ina eneo linalofaa kwa kilimo ambalo ni hekta milioni 44 na kati ya hizo hekta milioni 29.4 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini zinazotumika ni kidogo.

Katika hatua nyingine, Waziri Hasunga aliwataka vijana kujiunga na kuanzisha shughuli za kilimo kama uzalishaji mbegu za mazao kutokana na mahitaji makubwa yaliyopo.

"Mahitaji ya mbegu kwa nchi ni tani 187,000 wakati uzalishaji nchini ni tani 71,000 kwa mwaka hali inayowapa vijana kuwa na fursa ya kuzalisha," alisisitiza.

Aidha, aliwataka vijana wa Songwe kutumia eneo la Sasanda wilayani Mbozi lenye zaidi ya ekari 700 kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kupitia vikundi vya ushirika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema mkoa wake una ardhi nzuri yenye rutuba ya kutosha, hivyo wajitokeze kuzalisha mazao.

## NSSF yamwagia mabilioni wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limetoa mikopo ya Sh. bilioni tano kwa wajasiriamali wadogo na wa kati walio katika sekta ya viwanda ambao wana lengo la kuanzisha au kuongeza uzalishaji kwenye kazi zao.

Utoaji wa mikopo hiyo unatekelezwa kwa ushirikiano na Benki ya Azania, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), baada ya kuingia makubaliano ya mradi huo utakaozihusisha taasisi hizo nne kwa lengo la kuwawawezesha wajasiriamali wadogo.

Lengo ni kuwawezesha kupata mitaji au mikopo ya ununuzi wa mitambo ya uzalishaji ili waweze kuendeleza viwanda vyao.

Akifafanua kuhusu mikopo hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alisema shirika hilo limeendelea kuwekeza katika uchumi wa viwanda kwa kuwa uwekezaji ni moja kati ya majukumu manne ya kisheria ya kuanzishwa kwa shirika hilo.

Alibainisha kuwa majukumu ya mifuko ya hifadhi ya jamii ni kuwekeza, kuandikisha wanachama na kwamba kwa sasa kinachofanyika ni kushiriki katika eneo la kuwekeza kwa utaratibu unaofanyika kisayansi na kitaalamu, ikiwa ni pamoja na NSSF kutoa fedha kwa utaratibu uliopangwa na kukubaliana na taasisi zote tano zilizosaini makubaliano hayo.

Kwa mujibu wa Erio, Sh. bilioni tano zitatolewa kianzio na kwa kuwa mfuko huo ni endelevu, zikiisha zitatoka fedha zingine na wakati wote watu watakapotaka kukopa ambao watawezeshwa ili kutimiza lengo la kuwa na uchumi wa viwanda hapa nchini.

Alisema mara mradi huu wa pamoja utakapoingia kwenye hatua za utekelezaji NSSF itakuwa na uhakika wa kuongeza wanachama kwa kuwa kila mnufaika wa mkopo ana wajibika kuchangia NSSF kwa mujibu wa sheria na kwamba mkopo huo utaongeza pato kwa Taifa kupitia ulipaji kodi kutoka kwa wajasiriamali watakaowezeshwa.

Katika uwekaji saini wa makubaliano ya uanzishwaji wa mradi huo unaotekelezwa na taasisi hizo tano nchini, Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'I Issa, alisema kuwa mradi huo unalenga kutekeleza na kuendeleza azma ya Serikali ya awamu ya tano ya maendeleo ya viwanda.

Alifafanua NSSF imetenga Sh. bilioni 5 ambazo zimewekwa katika Benki ya Azania, itakayokuwa msimamizi mkuu wa kutoa mikopo, kufanya uchambuzi wa mikopo na kufuatilia mikopo hiyo kwa wajasiriamali kwa kushirikiana na baraza hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, alisema kuwa benki hiyo imepewa jukumu la kutoa upembuzi yakinifu wa wale ambao watapokea fedha hizo, kwa ajili ya kwenda kuwekeza katika maeneo ambayo tayari yatakuwa yamefanyiwa upembuzi yakinifu na VETA na SIDO, hatimaye benki itafanya tathmini ya namna gani viwanda hivyo vitajiendesha kwa faida ili fedha hiyo iweze kurudi kwenye mzunguko na kupewa watu wengine ambao nao wataenda kuwekeza pia kwenye maeneo mengine.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Prof. Sylvester Mpanduji, aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kununua bidhaa kutoka kwenye viwanda hivi vidogo ili viwanda hivyo viweze kukua.

Mpanduji alizitaja changamoto ambazo zimekuwa zikivikabili viwanda vidogo nchini na kuchelewesha ukuaji wake kuwa ukosefu wa mitaji na ukosefu wa vifungashio.

# Unesco sasa yakitambua Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), limeitambua lugha ya Kiswahili kama lugha itakayosaidia kukuza utangamano barani Afrika wakati wa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Lugha Mama yenye kaulimbiu "Lugha Bila Mipaka" iliyofanyika jijini Paris, Ufaransa hivi karibuni.

Katika kuadhimisha siku hiyo, Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa kwa kushirikiana na Unesco uliandaa mjadala kuhusu "fursa na changamoto za kukitambua Kiswahili kama lugha rasmi ya Bara la Afrika kwa ajili ya kukuza utangamano."

Akizungumza wakati wa mjadala huo, Balozi wa Tanzania nchini Ufaransa na Mwakilishi wa Kudumu katika Unesco, Samuel Shelukindo, pamoja na mambo mengine, alieleza hatua iliyochukuliwa na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa

Afrika (SADC) chini ya Mwenyekiti wake, Rais John Magufuli ya kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha zitakazotumika katika jumuiya hiyo.

Aidha, Balozi Shelukindo alizipongeza nchi za Afrika Kusini na Namibia kwa kuwa nchi za kwanza Kusini mwa Afrika zilizoamua kuanzisha ufundishwaji wa lugha ya Kiswahili katika shule mbalimbali. Mjadala huo uliwashirikisha wataalamu mbalimbali akiwamo Prof. Aldin Mutembei kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kufanyika kwa mjadala huo katika Unesco ni moja ya juhudi zinazofanywa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kupitia Ubalozi wa Tanzania nchini Ufaransa kwa kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha itakayotumika katika shirika hilo.



Wakazi wa Kata ya Bwasi, mkoani Mara, wakiandaa msingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya ya Shule ya Msingi Bwasi juzi, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa madarasa unaosababisha baadhi ya wanafunzi kusomea chini ya miti. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mangula ataka mashina kwenye kampeni 2020

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tanzania Bara, Philip Mangula, amewakumbusha viongozi wa mashina ambao hawajaunda kamati za uongozi kwenye mashina yao, waunde mara moja.

Amesema kwa kufanya hivyo, kamati hizo zitaweza kusaidia kuongoza na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yote ya CCM na utendaji kazi kwenye ngazi za shina.

Akizungumza na viongozi wa CCM wa ngazi mbalimbali pamoja na wanachama wa chama hicho Wilaya ya Singida Mjini, Mangula alisisitiza kuwa kamati ya uongozi ya shina ndiyo itakayokuwa ya kampeni za uchaguzi, na kwamba ili mafanikio ya kamati hizo yaweze kupatikana, ni vyema zikaandaliwa mapema.

Kwa mujibu wa Mangula, wakati wa kufanya kampeni ni lazima kamati hizo na wajumbe wake wahakikishe wanatetea chama chao hata kama mgombea aliyepitishwa na vikao vya juu hawatakuwa wamemuunga mkono, cha msingi ni kukipigania na kuweka mbele maslahi ya chama.

"Hata kama ulimchukia au hukumuunga mkono huyo, lakini chama chako ni lazima kishinde kwa hiyo mnajipanga, mnajadili namna ya chama chetu kishinde... ninyi mtakuwa mmeshakutana hivi sasa muwe mnaongelea namna ya kupata ushindi," alisisitiza.

Mjumbe wa Kamati Kuu CCM Taifa, Munde Tambwe Abdallah, alisema serikali ya awamu ya tano imetekeleza kwa vitendo ilani, hivyo hawana zawadi ya kumpa Rais John Magufuli zaidi ya kura za kishindo.

Munde ambaye ni mlezi wa chama hicho wa Mkoa wa Singida, pia alizitaja pia baadhi ya kazi za kamati za uongozi za shina kuwa ni kuongoza na kusimamia utekelezaji na maamuzi yote ya CCM na utendeji kazi katika shina, kuandaa shughuli za vikao vyote vya CCM vya shina na kutambua pamoja na kutunza kumbukumbu za wanachama katika shina husika.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Alhaji Juma Kilimba, alitamba kwamba mkoa huo utaibuka na ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu ujao.

# Fursa zaidi kwa wakulima korosho

**Na Hamisi Nasiri, MTWARA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Naliendele Mtwara (TARI), imesema kuwa tunda la bibo linaweza kuwa fursa mpya kwa wakulima wa korosho kujiinua kiuchumi.

Tunda hilo linaweza kuchakatwa na kutengeneza mvinyo, hivyo itaondoa dhana ya kutegemea mbegu (korosho) pekee yake.

Kauli hiyo ilitotolewa mkoani Mtwara na Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Dk. Fortunus Kapinga, alipokuwa akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Biashara mkoa wa Mtwara.

Alisema kwa muda mrefu taasisi hiyo imekuwa ikifanya utafiti wa zao la korosho na uligundua bidhaa mbalimbali ikiwamo mvinyo wa mabibo kuwa ni bora na una thamani kubwa katika soko

Alisema kutokana na ugunduzi huo mpya unaotokana na bibo la zao la korosho kutengeneza mvinyo, utafiti huo utamwezesha mkulima kunufaika na mazao mengine ya korosho kuliko ilivyo hivi sasa ambapo thamani ya korosho imeonekana kwenye mbegu yake pekee.

Alisema ugunduzi huo utaongeza uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, hivyo kuiongezea serikali mapato na kwamba hata wakulima pia wataweza kujiinua kuchumi kupitia zao la korosho.

Dk. Kapinga alisema teknolojia hiyo ya utengenezaji wa mvinyo kwa kutumia mabibo ya zao la korosho itakuwa ya kwanza nchini, na kwamba hiyo inajibu hoja ya muda mrefu ya uongezaji wa thamani ya zao la korosho kwa kutumia bidhaa zingine zinazotokana na zao hilo.

Kwa mujibu wa Dk. Kapinga, kwa sasa wakulima hawana sababu ya kuhofia utunzaji na usafirishaji wa mabibo kwani mabibo yaliyofanyiwa utafiti na kubainika kuwa na sifa ya utengenezwaji wa mvinyo ni yale yaliyokaushwa.

Dk. Kapinga aliongeza kuwa mazao mengine ya korosho yaliyofanyiwa utafiti na taasisi hiyo ni nishati na mafuta ya kuulia wadudu, ambayo yanatengenezwa kutokana na maganda ya korosho, maziwa yanayotengenezwa kutokana na mbegu za korosho na siagi ya korosho.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema serikali inapongeza hatua hiyo kwani itaongeza thamani ya zao la korosho na pia hata uchumi wa mkulima mmoja mmoja utafunguka zaidi.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kumchangia fursa hiyo adimu pamoja na wafanyabiashara wa ndani wanaoshughulika na biashara ya korosho kuanzisha mashamba ili kuongeza uzalishaji kwa kuwa serikali iko bega kwa bega kuhakikisha wanafanikiwa kwa kuitumia fursa hiyo.

# Kijiji Rufiji chapata mawasiliano simu

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, amesema huduma za mawasiliano ni sehemu ya maisha ya Watanzania kwa kuwa wananchi wanahitaji mawasiliano na wametambua umuhimu wa huduma za mawasiliano nchini.

Nditiye ameyasema hayo wakati akizindua mnara wa mawasiliano uliojengwa kwenye kijiji cha Mbunju Mvuleni Kata ya Mkongo wilayani Rufiji mkoani Pwani, uliojengwa na kampuni ya mawasiliano ya Halotel Tanzania kwa kutumia ruzuku ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotolewa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ili kufikisha huduma za mawasiliano kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara na yaliyopo vijijini ambapo kampuni za simu haziko tayari kufikisha huduma za mawasiliano.

"Sasa mawasiliano ni sehemu ya maisha ya Watanzania, wanahitaji mawasiliano, UCSAF inatoa ruzuku kwa kampuni za simu na zinajenga minara ya mawasiliano, UCSAF imesaidia wananchi kuwasiliana," alisisitiza Nditiye.

Aliongeza kuwa ipo minara zaidi ya 68 ambayo serikali inahitaji izinduliwe ili wananchi wafahamu serikali inatekeleza majukumu yake na ujenzi wa minara, na kwamba ni miradi mikubwa kwa kuwa ujenzi wa mnara mmoja gharama yake ni kati ya Sh. milioni 300 hadi Sh. milioni 400.

"Hatutegemei umwone mtu anaharibu mnara huu mkakaa kimya kwa kuwa mnara huu ujenzi wake umegharimu Sh. milioni 320, hatutegemei mtu aende mbali kuuza bidhaa, utauza kwa simu na utapokea pesa kwa simu," alisema Nditiye.

Naye Mbunge wa Rufiji, Mohammed Mchengerwa, aliishukuru serikali kwa kujenga minara ya mawasiliano ili kuwawezesha wananchi kuwasiliana kwa kuwa hapo awali wananchi wa kata ya Mkongo walikuwa wanapata changamoto ya huduma za mawasiliano na sasa mawasiliano yanapatikana.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, alimweleza Nditiye kuwa asilimia 80 ya eneo la wilaya hiyo mawasiliano yanapatikana.

Mwenyekiti wa Bodi ya UCSAF, Dk. Joseph Kilongola, alisema: "Sisi kama bodi tunatekeleza maelekezo ya serikali ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za mawasiliano."

# Mambo saba kuibeba Mara kielimu

**Na Sabato Kasika**

MKOA wa Mara umefanya kongamano la kuboresha elimu kwa ajili ya kuongeza ufaulu katika shule za msingi na sekondari, na kutoka na maazimio saba ya kufanikisha uboreshaji huo.

Kongamano hilo lililoandaliwa na Mkuu wa mkoa huo, Adam Malima, lilifanyika Jumapili Mjini Musoma likishirikisha wadau mbalimbali wa elimu zaidi ya 400, kutoka ndani na nje ya mkoa huo.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kongamano hilo, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mara, Ephaim Simbeye, aliwataja baadhi ya wadau hao ni Stephen Wasira, Prof. Sospeter Muhongo na wengine kadhaa.

Kuhusu maazimio, alilitaja la kwanza ni uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya aina zote katika shule za msingi na sekondari ukiwamo ujenzi wa madarasa, uongezaji wa madawati na vifaa vingine vya shule.

"Azimio la pili ni kudhibiti utoro wa wanafunzi, ambao nao unachangia kushuka kwa elimu, wakati azimio la tatu ni kuanzisha utaratibu wa kutoa chakula shuleni na pia kuhakikisha shule zenye mashamba zinazalisha chakula ambacho kitatumiwa na wanafunzi," alisema Simbeye.

Alisema, wadau hao wameazimia kuwapo kwa mahusiano mazuri ya shule na jamii na pia kudhibiti nidhamu ya wanafunzi, na kwamba azimio la tano ni kupambana na ukatili na mimba kwa wanafunzi.

Azimio la sita ni ushirikishwaji wa jamii katika masuala ya elimu wakati la saba ni usalama wa walimu na wanafunzi ili kuhakikisha kila upande unatimiza wajibu bila kukwazwa.

Aidha, Simbeye alisema, imeundwa kamati maalum ya kufuatilia maazimio hayo, ambayo itaongozwa na RC Malima, huku wajumbe wake wakiwa ni wakuu wa wilaya zote.

"Kamati itasaidiana na wataalamu wa elimu katika shughuli zake na kisha Agosti mwaka huu wadau wa elimu watakutana tena kufanya tathmini ya utekelezaji wa maazimio hayo," alisema.

Mkoa wa Mara una zaidi ya shule za sekondari 204, huku za msingi zikiwa ni 847, ambazo zimewekewa maazimio hayo ili ziweze kuwa na matokeo mazuri katika mitihani.

"Kwa miaka mitatu mfululizo, mkoa wetu umekuwa ukifanya vibaya kwenye mitihani ya taifa, hivyo tukaona kuna haja ya kuitwa wadau wote wa elimu ili kutoa maoni yao kwa ajili ya kuboresha elimu mkoani mwetu," alisema.

Katika mtihani wa taifa wa darasa la saba wa mwaka jana, mkoa wa Mara ulikuwa wa 26 kitaifa, huku kidato cha nne ukiwa wa 25 kitaifa.



Lundo la takataka zikiwa zimetelekezwa bila ya kuzolewa kando ya Barabara ya Mandela, eneo la Soko la Vetenari Tazara, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya na kinaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC akerwa waliowachongea wanafunzi kuonyeshwa mtihani

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amesikitishwa na kitendo cha baadhi ya watu kupeleka maneno ya uchonganishi kwenye Baraza la Mtihani wa Taifa (NECTA) kuwa wanafunzi waliofanya vizuri mkoani Shinyanga kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana walionyeshwa mtihani.

Telack alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanzia Januari 2016 hadi Desemba 2019, kikao kilichohudhuriwa na watendaji wa serikali pamoja na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Shinyanga.

Alisema ni kitendo cha ajabu sana baadhi ya watu kuonea wivu mkoa wa Shinyanga, kutokana na wanafunzi watano tena wasichana kushika nafasi tano bora kitaifa kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka jana, na kupeleka maneno ya uchonganishi kuwa wanafunzi hao walionyeshwa mtihani.

"Nimekerwa sana na kitendo hiki cha kupeleka maneno kwenye Baraza la Mtihani la Taifa kuwa wanafunzi wetu waliooshika nafasi tano bora kitaifa eti walionyeshwa mtihani... tena ndugu wajumbe ni waambie tu wanafunzi hawa walirudia mtihani huo wa taifa, na cha ajabu wakafanya vizuri zaidi kuliko mara ya kwanza," alisema Telack.

"Tena wanafunzi hawa wanatoka kwenye shule moja ya Serikali ya Ilobi iliyopo wilayani Kishapu, ambapo Suzana Maige Sabale alishika nafasi ya pili kitaifa, Pili Bugomora Jileta ya tatu, Wande Ngassa Shija ya tano, Rahel Richard Jizenga ya Saba, Ngolo Mipawa Buhilu nafasi ya tisa na wote ni wasichana pongezi kwao," alionngeza.

# Madiwani wambana kigogo utalii milimani

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA MJINI

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha wamemwagiza Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Ardhi, Saloni Lukumay, kuhakikisha anatenga fungu kwa ajili ya uwekezaji kwenye maeneo ya milima yote ya jiji hilo ili kuvutia watalii.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwa niaba ya madiwani wenzake, Gaudency Lyimo, alisema milima iliyoko kwenye Jiji la Arusha ni vyema ikatunzwa vizuri kwa faida ya vizazi vijavyo.

Alisema licha ya kujaliwa kuwa na milima mizuri, anashangazwa na jiji kutoijali na baadhi ya maeneo kama vile milima ya Nadosoito na Murieti, imesababisha baadhi ya watu kudai ni mali yao na kuzuia jiji kuipima.

"Kweli hiki kitu kinashangaza sana, sababu milima hii ni rasilimali za watoto wetu na tunaomba isiwekwe siasa, nendeni mkaipime, ili tuwekeze kwenye milima hii kwa ajili ya kuvutia uwekezaji kwenye jiji letu," alisema.

Akijibu hoja za madiwani hao, Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Ardhi, Lukumay, alisema milima yote inafuatiliwa kwa karibu na hakuna uliotelekezwa na jiji hilo.

Alisema hata Mlima wa Suye tayari umeshapimwa kwa ajili ya uwekezaji na katika kuhakikisha milima yote iliyoko katika jiji hilo inahifadhiwa, halmashauri imetenga Sh. milioni 100 katika bajeti ya mwaka 2020/2021.

"Tumetenga fedha hizi kwa ajili ya kufanya uwekezaji mkubwa kwenye milima yetu na hakuna wa kuzuia serikali kuwa milima ni mali yao, sababu sheria ipo wazi, maeneo haya ya milima yote mali yetu," alisema.

Aliwaomba madiwani hao kuacha kuwa na wasiwasi na utendaji kazi wao katika uhifadhi wa milima hiyo kwa kuwa inafuatiliwa na ipo salama.

"Lakini, hakuna siasa yoyote inafanyika juu ya uwekezaji wa milima hii, maana tunatambua milima yote ni rasilimali kwa ajili ya watoto wetu," alisema.



Watalii kutoka nchi mbalimbali wakiangalia Bonde la Ngorongoro, wakati walipotembelea kuangalia vivutio vinavyopatikana ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, iliyopo wilayani Ngorongoro, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# DC aona mwanga maendeleo elimu

Na Cynthia Mwilolezi, SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amesema baada ya kupiga hatua kwenye sekta ya elimu kwa kuanzisha shule mbili za sekondari za kidato cha sita na Chuo cha Ufundi, sasa wanaingia kwenye mchakato wa kuanzisha shule nyingine ya kidato cha sita.

Chaula aliyasema hayo juzi wakati akizungumzia maendeleo yaliyofanyika chini ya uongozi wa Rais John Magufuli katika eneo hilo.

Alisema wakati serikali inaingia madarakani mwaka 2015, hakukuwa na shule ya kidato cha tano na cha sita wala Veta Simanjiro, lakini sasa zipo shule mbili na chuo kimoja kilichoko Kata ya Emboreet.

"Tupo kwenye mpango wa kuanzisha shule nyingine ya kidato cha sita kwenye Tarafa ya Moipo eneo la Naisinyai, hivyo tutakuwa na shule tatu za kidato cha sita katika Wilaya yetu ya Simanjiro," alitamba.

Alilipongeza shirika lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation kwa kushiriki mapinduzi ya sekta ya elimu kwenye maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Alisema ECLAT Foundation wameshiriki kwa kiasi kikubwa kufanikisha uanzishwaji wa shule ya kwanza ya kidato cha sita kwenye wilaya hiyo.

"Pia juhudi zao zimesababisha tukawa na Chuo cha Ufundi cha Veta, ambacho kwa namna moja au nyingine kitawajengea uwezo vijana wetu mbalimbali watakaopata elimu kwenye chuo hicho," alisema.

Mwenyekiti wa Shirika la ECLAT Foundation, Peter Toima, alisema waliona kuwa na shule ya kidato cha sita kwenye wilaya hiyo ni maendeleo makubwa, ndiyo sababu wakashirikiana na serikali kuianzisha katika Kata ya Emboreet.

"Na pia chuo cha kwanza cha ufundi cha Veta kitachochea vijana wa eneo hili la Simanjiro kuwa na taaluma ya ufundi na kujiajiri au kuajiriwa pindi wanapohitimu," alisema.

Alisema ataendelea kushirikiana na wafadhili wake, Upendo Society kutoka Ujerumani, ili watoto wa eneo hilo wapevuke kielimu kwa kuboresha miundombinu ya shule.

# Muro ajivunia mitambo ujenzi uboreshaji barabara

Na Cynthia Mwilolezi, ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amekunwa na utekelezaji wa uboreshaji wa barabara za wilaya hiyo baada ya kununua vifaa vya kisasa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara mwishoni mwa mwaka jana.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na waandishi wa habari kuhusiana na uboreshaji wa miundombinu ya wilaya yake, Muro alisema serikali iliahidi kutatua kero sugu za barabara ambazo zilikuwa zimeharibika kwa kiwango kikubwa na kushindwa kupitika wilayani humo na sasa inatekeleza.

Alisema kutokana na kero hizo za muda mrefu, aliamua kutafuta mitambo imara ya kisasa ya ukarabati na matengenezo ya barabara zote za wilaya hiyo, ili wananchi wasiendelee kuteseka na tatizo hilo.

"Kazi yangu ni kusikiliza kero za wananchi na kuzitolea ufumbuzi, nilisikiliza kero sugu ya ubovu wa barabara inayowakabili wananchi wa Arumeru na tumeipatia ufumbuzi na ufumbuzi wenyewe ni kama huu wa kuleta kifaa hiki, ambacho tutakitumia pamoja na kile kijiko chetu kwa ajili ya kutengeneza barabara zote za Wilaya ya Arumeru," alitamba.

Muro alisema ukarabati wa barabara hizo ulianza rasmi Agosti 19 mwaka jana na unaendelea hadi sasa, lakini ujenzi hauishi kwa kuwa barabara zinaharibika kila wakati kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

"Barabara zote za kata na vijiji vyote vilivyopo katika Halmashauri ya Meru, pamoja na Arusha DC zinakarabatiwa na hata mvua ikinyesha, zikiharibika tunafanyia uboreshaji, ili wananchi wasiteseke," alisema.

Muro aliongeza kuwa mtambo huo wa ujenzi wa barabara aina ya loader, umepatikana kutokana na juhudi walizofanya kwa kushirikiana na Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo.

**"Barabara zote za kata na vijiji vyote vilivyopo katika Halmashauri ya Meru, pamoja na Arusha DC zinakarabatiwa na hata mvua ikinyesha, zikiharibika tunafanyia uboreshaji, ili wananchi wasiteseke," alisema.**





# Wataka mjadala ukatili wa kijinsia

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

JUKWAA la vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) Mkoa wa Kilimanjaro, limeikumbusha Wizara ya Afya kuitisha kikao cha wadau wa mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ili kujadili suala la uhuishaji wa takwimu kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia.

Wadau hao wanataka yafanyike mabadiliko katika takwimu za ukatili zinatotumika sasa, kwa kuwa ripoti ya upimaji wa demografia na afya Tanzania ya mwaka 2015/16 ni kama inakosa uhalisia, baada ya takwimu kuonekana kupitwa na wakati.

Jana, Mratibu wa jukwaa hilo mkoa wa Kilimanjaro, Veronika Ullomi aliishauri wizara hiyo kuona namna bora ya kuja na takwimu mpya, ambazo zitasaidia kuonyesha hali halisi ya ukatili wa kijinsia na namna mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto (Mtakuwwa) utakuwa umefanikiwa.

"Wenzetu ambao ni wadau wanaotoka na serikali, wao walishashauri hili, na leo sisi tunakumbusha kwamba ni vyema wizara ikashughulikia mapendekezo ya wadau kuhusu jambo hili.

"Kimsingi, kuna utafiti ulishafanyika mwaka 2011 baina ya WHO (Shirika la Afya Ulimwenguni) kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania unaona umefanyika zaidi ya miaka mitano iliyopita.

Zaidi aliongeza: "Tunahitaji kufanya upya tathmini nyingine kuona kama hali hii inapungua au inaongezeka, hasa baada ya kuwapo juhudi mbalimbali za kupambana na ukatili huu," alisema Ullomi.

Alisema uhitaji huo ni mkubwa kutokana na kuongezeka kwa matukio ya ukatili hasa wa kingono kwa watoto.

Ripoti iliyotolewa mwaka jana na Chama cha Maofisa Ustawi wa Jamii nchini (TASWO), ilionyesha kuwa hali ni mbaya zaidi katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ambako kati ya Januari hadi Septemba mwaka 2019, watoto 157 waliripotiwa kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali.

Katika ripoti hiyo, watoto 52 kati ya hao 157 wamefanyiwa ukatili wa kingono ambayo ni sawa na asilimia 33.

**"Wenzetu ambao ni wadau wanaotoka na serikali, wao walishashauri hili, na leo sisi tunakumbusha kwamba ni vyema wizara ikashughulikia mapendekezo ya wadau kuhusu jambo hili.**

# Kampeni yaanza kuwapatia taulo wanafunzi wa kike 4,000

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

TAASISI ya Maendeleo ya Uru (UDF), imeanzisha kampeni maalum ya kimkakati ya 'Binti Nabaki Darasani' ambayo imepewa jukumu la kutafuta fedha za ununuzi wa taulo za kike kwa ajili ya kufikia wanafunzi zaidi ya 4,000 wanaosoma Shule za Sekondari Wilaya ya Moshi.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Wakili Wilhard Kitali, alisema katika awamu ya kwanza ya kampeni hiyo itakayozinduliwa Machi 9 mwaka huu, wanafunzi 500 kutoka Shule za Sekondari za Mangi Sabasi, Mawela na Chuo cha Ufundi Mawela (MVTC) watanufaika na taulo hizo au kwa jina jingine sodo.

Alisema katika mgao wa taulo hizo za kike, wanafunzi wa shule tatu ambazo ni Mangi Sabasi watapata taulo 200, Mawela 250 na Chuo cha Ufundi Mawela watapewa taulo 50.

"Lengo letu kama taasisi ya kimkakati ni kuwafikia wanafunzi wa kike zaidi ya 4,000 waliopo katika Wilaya ya Moshi. Tunataka kampeni hii ya Binti Nabaki Darasani tuipeleke katika Wilaya nyingine za Siha, Same, Mwanga, Rombo na mkoa mzima wa Kilimanjaro, na baadaye tutakwenda tena mikoani," alisema Kitali.

Kwa mujibu wa wakili huyo, idadi kubwa ya wasichana hasa wanaotoka katika familia au koo za Wachaga, wazazi wa kiume na wa kike wamekuwa wakikwepa jukumu la msingi la kuzungumza na watoto wao wa kike kuhusu suala la hedhi salama na afya ya uzazi kwa ujumla.

"Wengi wa wasichana wanaotoka katika familia au koo za Wachaga, hawapati elimu sahihi kuhusu hedhi salama na afya ya uzazi, tukaona tuje na kampeni ya kutoa elimu kwa jamii, lakini kuanzisha mkakati wa kutoa sodo kwa wahitaji hasa walioko Shule za Sekondari ambao hawana uwezo wa kumudu gharama zake," alisisitiza.

Alisema kwa kuwa kampeni hiyo ni endelevu, kila mwaka taasisi ya UDF inalenga kuwaondoa wanafunzi wanaotoka kwenye kaya duni katika adha ya kushindwa kuhudhuria shuleni na kukosa masomo wakati wanapokuwa katika siku za hedhi.

Bei kubwa ya taulo za kike au sodo inatajwa kuwa sababu ya wanawake kwenye maeneo mengi ya vijijini kuendelea kutumia njia za asili kujihifadhi ambayo sio salama kwa afya zao.

Inaelezwa kuwa wasichana na wanawake wanaojilazimisha kwenda kazini au shule, licha ya kutokuwa na vifaa toshelezi na vyenye ubora vya kujihifadhi katika siku zao za mwezi, huwa na siku ngumu na mara nyingi na mara nyingi hata ushiriki wao aidha katika masomo au kazi huwa ni dhaifu.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, akipanda mti katika eneo la shule mpya ya sekondari ya Tambarare, wilayani Hai, wikiendi, iliyojengwa kwa nguvu za wananchi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wawekezaji waonyesha nia kuwekeza Hai

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, amesema kuna mabadiliko makubwa ya kiuchumi yananukia wilayani humo hivi sasa, baada ya watu wenye uwezo wa kiuchumi kuonyesha nia ya kuwekeza katika eneo la ukanda maalum wa viwanda (EPZ).

Kwa mujibu wa Sintoo, eneo ambalo limeanza kuvutia wawekezaji wa ndani lina ukubwa wa hekta 463.

"Kasi ya watu wanaojitokeza kutaka kuwekeza Hai inatia faraja, kwa sababu eneo tulilolitenga la mashine tools, njia panda ya Machame linavutia wengi na hivi sasa mnaona kuna ujenzi wa kiwanda kimoja kikubwa pale kinaendelea na bado kuna wanaoomba wanajitokeza," alisema.

Alisema eneo hilo hivi sasa, limewekwa wazi kwa ajili ya uwekezaji wa bidhaa za viwandani.

Kuhusu uwekezaji katika sekta ya utalii, alisema wilaya hiyo ina vivutio muhimu vya utalii ambavyo ni pamoja na chemchemu ya Chekimaji inayotoa maji ya moto.

"Hai yako pia maeneo ya kutosha kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli za kitalii hasa ukizingatia ni eneo lililo karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Hivi sasa tunahangaika kutafuta wawekezaji ndani na nje ya nchi ambao watakuja kuwekeza hapa kwa ajili ya kuchochea sekta ya utalii," alieleza Sintoo.

Kuhusu mchakato wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa soko la kimataifa la nafaka ambalo uwekezaji wake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 11 katika eneo la Kwa Sadala, alisema unaendelea.

Soko hilo ambalo limepewa jina la 'The Magufuli International Complex Centre' (MICC-Hai), litajengwa karibu na kiwanda cha Arsho au mkabala na njia panda ya kwenda Masama.

Inaelezwa kuwa soko hilo ambalo litakuwa na kazi ya kuongeza thamani ya mazao, kuchochea pato la mkulima na kuingizia serikali kodi, litakuwa na eneo maalum la viwanda vya usindikaji, eneo la utalii zikiwamo hoteli, kituo cha habari za utalii, migahawa ya kisasa na maeneo ya huduma za kibenki.

Nipashe
# TESA
Jumanne Februari 25, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 18

## Wabongo wengi hupoteza muda kwenye simu


Ukurasa 17

## Kirusi corona chaua 12 Iran, 80,000 wafariki duniani kote


Ukurasa 14

## Ulinzi wa Polisi Farasi



# Mimba zimewachosa sekondari za Moro Vijijini, wawekeza mabweni kwa mpigo

Ukurasa 16

## ELIMU YA KIPOLISI



Vikosi vya farasi vikiwa kazini kwenye miji mbalimbali. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





## JIELIMISHE

# Ulinzi wa Polisi Farasi

MATAIFA mengi hufanya juhudi mbalimbali kuwapa askari wake vifaa vya kisasa kuimarisha utendaji wao. Hapo zamani, polisi walikuwa wanatumia bastola au bunduki zaidi lakini sasa wamewezeshwa kwa vifaa vya kisasa kama kamera, vinasa sauti, radio na dege zikiwano dron.

Hata hivyo, wanyama kama mbwa na farasi ni muhimu . Haijalishi taifa limepiga hatua kiasi gani kimaendeleo, zinatumia farasi na mbwa kuzunguka katikati ya miji na majiji mbalimbali duniani. Ndiyo maana kikosi cha farasi cha polisi kipo Kilwa Road jijini Dar es Salaam na hutumiwa kwa matukio mbalimbali hasa kwenye kukabiliana na uhalifu unaotokea kwenye umati.

Wanatumika kutuliza ghasia na kutawanya makundi ya watu ambao hawawezi kudhibitiwa na askari polisi wanaotumia magari.

Farasi ni alama ya utamaduni na kivutio cha wageni wanaotembelea miji mikubwa . Wanyama hao ni hodari katika uokozi na kuyafikia maeneo yasiyofika na magari.

Ukitembelea miji mikubwa duniani unaweza kushuhudia farasi wanaoongozwa na askari waliovalia sare wakizunguka katika mitaa mbalimbali bila kufahamu sababu za wanyama hao kuwepo mjini.

Farasi ambao ni warefu wa kimo hutumika zaidi kwa shughuli za usalama wa raia na mali zao. Lakini kwanini farasi na siyo teknolojia nyingine za usalama kama matumizi ya taa na kamera maalum za kurekodi matukio za CCTV au vizuizi vya barabarani?

Hizi ndizo sababu, miji mbalimbali duniani kuwa na kikosi maalumu cha farasi kinachojulikana kama mounted police wanaoongozwa na polisi.

Farasi hudhibiti fujo na vurugu za watu wengi kama kwenye viwanja vya taifa wakati wa kandanda na matukio makubwa Zaidi.

Sababu kubwa ya farasi wanaotumika kwenye ulinzi kwenye majiji makubwa ikiwamo London nchini Uingereza, New York (Marekani) na Berlin (Ujerumani) ni kutuliza ghasia wakati makundi mbalimbali ya watu yakizozana.

Polisi wanaotumia farasi hao wana uwezo mkubwa wa kuvunja na kutawanya mkusanyiko wenye fujo, hasa kwenye mechi za mpira wa miguu.

Farasi zinaweza kupenya kwa urahisi katikati ya umati wa watu na ni rahisi kwa polisi aliye juu ya mnyama huyo kuwaona watu na kujihami kwa lolote wakati akitekeleza majukumu yake.

Pia mnyama huyo anaweza kukimbia kwa haraka na kupenya kwenye maeneo yaliyobanana kama mitaa yenye maduka na pembezoni mwa barabara.

**Makala kwa msaada wa mtandao**



Polisi wakifanya doria kwa kutumia farasi. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# Baada ya kusikia utabiri TMA taasisi ziamke kukabili maafa



Mabwana afya washirikiane na wananchi kufukia madimbwi mitaani ili kuepusha maafa. **PICHA: MTANDAO.**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), tayari imeshatoa utabiri wa mvua za masika ambazo ni maalum kwa mikoa inayoapata mvua mara mbili kwa mwaka, au ile yenye misimu miwili ya vuli na masika.

Katika utabiri huo uliotolewa hivi karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk Agnes Kijazi, anaelezea kuwa mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya Machi yaani wiki ijayo, katika maeneo hayo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka.

Mikoa hiyo ambayo utabiri huo unaihusu ni pamoja na Dar es Salaam, Pwani, Zanzibar, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kigoma.

Kimsingi TMA imefanyakazi yake hivyo ni jukumu la wakulima, wafugaji, wasafirishaji na sekta zote ambazo zinategemea uwapo wa taarifa za hali ya hewa ili kujua namna ya kuendesha shughuli zao.

Dokta Kijazi katika utabiri anaoutoa anaeleza wazi kuwa kuna baadhi ya maeneo yatapata mvua kubwa kwa maana ya kufikia kiwango cha juu ya wastani huku sehemu chache zikipata mvua za wastani mpaka chini ya wastani au mvua haba.

Anasema maeneo ambayo yatapata mvua kubwa au ya juu ya wastani mvua hizo zitafuatana na athari mbalimbali na hilo ndilo watu wanapaswa kulizingatia.

Utabiri wa TMA unaeleza kuwa mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani, mikoa ya kanda ya ziwa kutakuwa na mvua za wastani na mvua kubwa kwa maeneo hayo.

"Kwa mikoa hii ambayo mvua zake zitakuwa za juu ya wastani, tunatarajia pia zitakuja na athari zake katika maeneo hayo, yapo mapendekezo na ushauri tumeutoa kwa mamlaka husika," anasema Dk. Kijazi.

Anawaeleza wananchi kuwa maeneo hayo wanapaswa kufuatilia kwa karibu taarifa za hali ya hewa pamoja na kuchukua hatua stahiki kuepuka madhara ya mvua hizo.

"Niwaombe wananchi wa maeneo hayo, ni muhimu sana kuchukua tahadhari, kwa wale wanaoishi mabondeni ni vyema kuchukua hatua na ikibidi kuondoka mapema, pia kwa wakulima wasafirishaji wachukue tahadhari," anasema Kijazi.

TMA inataja sekta ambazo zinaweza kukumbwa na athari za mvua hizo za juu ya wastani kuwa ni pamoja na kilimo, usalama wa chakula, uvuvi na mifugo.

Kwa upande huo, TMA inasema wadudu waharibifu wa mazao na magonjwa vinaweza kujitokeza kutokana na mvua kubwa zinazotarajiwa kunyesha na kwamba zinaweza kuongeza uzalishaji wa mifugo pamoja na mazao ya mifugo kama maziwa kutokana na kuogezeka kwa malisho ya wanyama.

Kwa mikoa hii ambayo mvua zake zitakuwa za juu ya wastani, tunatarajia pia zitakuja na athari zake katika maeneo hayo, yapo mapendekezo na ushauri tumeutoa kwa mamlaka husika.

"Lakini pia kwa wafugaji wa samaki wanapaswa kuchukua hatua kwa sababu mvua zinaweza kuharibu miundombinu ya mabwawa, wafugaji waimarishe miundo mbinu," anasema Dk Kijazi.

## NISHATI, MADINI NA MAJI

Akizungumzia eneo hilo anasema tahadhari inatolewa kwa wachimbaji wadogo wa madini wakiagizwa kuchukua tahadhari kutokana na unyevunyevu kwenye udongo unaoweza kusababisha maporomoko ya udongo na machimbo ambayo yanaweza kusababisha kupoteza maisha na mali.

Pia , kwenye sekta ya nishati hususani umeme kutokana na mvua nyingi zinatarajiwa kunyesha kwenye maeneo ya mikoa mingi ni vyema kuangalia nguzo kuu, miti inayoangukia nyaya na pia kukata umeme kutokana na radi.

"Lakini mvua hizi zitasaidia kuongezeka kwa kina cha maji kwenye mabwawa na mito na pia upatikanaji wa maji ya kutosha unatarajiwa kutokana na mvua hizi hivyo kuongeza samaki na umeme", anasema Dk Kijazi.

## SEKTA YA AFYA

Dokta Kijazi anasema mvua kubwa zinazotarajiwa kunyesha kwenye mikoa hiyo zitapelekea kutuama kwa maji na kuweka mazingira wezeshi kwenye mazalia ya mbu na hivyo kupelekea ongezeko la ugonjwa wa malaria.

"Na pia kipindi kama hiki tunatarajia mlipuko wa magonjwa kama kuhara na homa ya matumbo. Hapa pia wananchi wanapaswa kuchukua hatua kwa kuhakikisha wanasafisha kila mala mazingira yao kwa kuondoa mazalia ya wadudu", anakumbusha.

Aidha, pia kwa mamlaka za miji, TMA inatoa tahadhari ya uharibifu wa miundombinu kama barabara na madaraja kutokana na mvua kubwa katika maeneo hayo.

TMA imesisitiza katika mikoa ambayo itapata mvua za wastani na mvua ndogo, mkoani Kigoma wilaya za Kakonko na Kibondo na mkoani Kagera, wananchi wanapaswa kutunza vyanzo vya maji na pia kulima mazao yatakayostahimili mvua ndogo.

Utabiri wa mvua za masika kwa mwaka huu unafananishwa na mvua zilizonyesha mwaka 2007.

## KUTIMIZA WAJIBU

Maadamu TMA imeshaeleza kile kinachotabiriwa kutokea ni wajibu wa wataalamu kuwajibika kuifundisha jamii namna ya kukabiliana na kudhibiti changamoto na fursa zinazotokana na mvua.

Ni vyema maofisa ugani wakaanza kuwaeleza wakulima kuhusu wadudu na visumbufu vitavyoharibu mazao ili wajiandae au kutayarisha viuatilifu.

Wataalamu hao wanapaswa kuwaeleza wakulima njia za kuepuka visumbufu hivyo hasa wakati huu wanapoandaa mashamba.

Kwa upande wa mabwana afya waanze kampeni za kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kutumia vyoo wakati wote ili kuepusha vinyesi kuchafua maji na kusambaza magonjwa.

Ni wakati wa kuhimiza jamii kukumbuka kunywa maji yaliyochemshwa na kula vyakula vya moto ili kujiepusha magonjwa yanayoibuka wakati wa mvua.

Viongozi wa mitaa na vijiji waanze kuchukua tahadhari kuwahimiza wananchi na wanaojenga nyumba kufunika makaro ya majitaka na majisafi, kufukia visima na kuviwekea alama ili kuepusha watoto na wapitia njia pamoja na wanyama kutumbukia na kupoteza maisha.

Aidha, wakitumia utabiri wa hali ya hewa na taarifa za TMA wasisitiza watu kufukia mabwawa na kwa upande wa madimbwi makubwa ambayo hawawezi kuyafukia wazungushie uzio na kuzuia watu wasipite ili kuondoa hatari zinazoweza kuletwa na mafuriko au maji kutoka mabwawani.

Kwa upande mwingine Wakala wa Ujenzi wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura), watafute njia mbadala kwenye madaraja na sehemu zenye makalavati na mitaro iliyokwamisha usafiri wakati wa mvua.

Tarura ishirikiane na wananchi na vikundi vya kijamii kusafisha na kuzibua mifereji na pia kurudishia makalavati na kutengeneza sehemu korofi na zilizobomoka na hata kutafuta mbadala wa njia ili kupunguza kero msimu wa msimu wa mvua.

ELIMU

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

# Mimba zimewachosa sekondari za Moro Vijijini, wawekeza mabweni kwa mpigo

• Bodaboda, nyumba kupanga shida kubwa • Kidato 1 hadi 4 wananasa; dada zao wajanja

HALMASHAURI ya Wilaya ya Morogoro imetenga Sh. milioni 337 katika bajeti zake za ndani mwaka uliopo kwa ajili ya kujenga mabweni manne kwenye tarafa nne.

Lengo ni kuwanusuru mabinti kutembea umbali wa kilomita saba hadi nane kufika shule ni safari yenye madhila ya vishawishi vinavyoishia mikasa ya mimba, hiari ya kubakwa, zote zinaagukia jibu 'shule basi.'

Mhandisi wa Wilaya, Hamisi Nzumira, anasema fedha hizo zimetengwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Tamisemi, kuhusu ujenzi wa mabweni, maeneo tambarare itumike Sh. Mililioni 75 na kwenye miinuko Sh. milioni 110, zikiwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 80, sehemu ya kufua, vyoo, bafu, umeme na maji.

Nzumira anasema, lengo kuu la ujenzi huo ni kuwahakikishia wanafunzi wanafikia malengo wanayokusudia.



Baiskeli za aina mbalimbali za wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mvuha, iliyopo Morogoro Vijijini. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

### OFISA ELIMU

Ofisa Elimu- Sekondari wa halmashauri hiyo, Hatujuani Lukari, anasema idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari waliopata mimba na kushindwa kuendelea na masomo imepungua na kufikia 45 mwaka 2018/19 kutoka 55 mwaka 2017/18.

Lukari anasema katika mwaka 2017/18 wanafunzi waliopata mimba walikuwa 55 kwa mgawanyo; kidato cha kwanza 10; cha pili 21; cha tatu 11; na kidato cha nne 13.

Anafafanua mwaka uliofuata, 2018/19 walikuwa 45 katika mgawanyo; kidato cha kwanza sita; cha pili 14; tatu tisa; na wanaomaliza kidato cha nne 15, na cha sita mmoja

Lukari anasema, wanafunzi hao wanaotembea na wengine wanatumia baiskeli, wanakutana na vishawishi hasa vya waendesha bodaboda kuwapa lifti, simulizi inayoangukia katika mimba.

Anasema, kata zenye shule zinachukua vijiji kadhaa, baadhi ziko umbali mrefu, akitoa mfano wa Shule ya Sekondari Mvuha yenye wanafunzi wanaotoka kijiji cha Kongwa, umbali wa kilomita nane.

Katika kukabiliana, halmashauri imeanza kujenga mabweni manne kwa ajili ya wanafunzi kidato cha tano na sita kwenye shule moja ya kila kata kwenye tarafa nne, kati ya sita zilizopo wilayani humo; Ngerengere, Bwakira Chini, Mikese na Mkuyuni, huku tarafa ya Matombo ikishapata bweni ya vidato hivyo.

> Wanafunzi wanakuwa mikononi mwetu sisi walimu kuanzia asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana huku tukiwa na jukumu la kuwaangalia, lakini baadaye wanaondoka na kwenda majumbani.

### MKUU SHULE

Mkuu wa Shule ya Sekondari Mvuha, David Nduye, anasema suala la mimba kwa wanafunzi na kukatisha masomo, bado ni changamoto kubwa inayopaswa kuangaliwa kwa 'jicho la tatu' hasa katika haja ya kuwapo mabweni na kuwaweka mabinti kwenye ulinzi wazingatie masomo.

Mwalimu Nduje, wanafunzi hasa wa kike wako katika mazingira hatarishi ya kukaa katika nyumba za kupanga, kwa wale wanaoishi jirani kutasaidia kupunguza mimba za wanafunzi, pia hatari ya magonjwa.

"Wanafunzi wanakuwa mikononi mwetu sisi walimu kuanzia asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana huku tukiwa na jukumu la kuwaangalia, lakini baadaye wanaondoka na kwenda majumbani," anasema na kuomba:

"Lakini tukipata mabweni na sisi itasaidia kuwachunga muda wote shuleni na kuwafikisha mbali kielimu."

### MWANAFUNZI AFUNGUKA

Mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya Mvuha, Hanisha Hamisi (18), anasema wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya umbali kati ya nyumbani na shule.

Anashauri wanafunzi wenzake waone haja ya kufuata kinachowapeleka shule na siyo vishawishi vinavyowaharibia malengo.



Wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Mvuha, katika mjumuiko wao katika mazingira ya shule.

Mratibu wa Ukimwi wilayani Morogoro, Dk. Jihadhari Pazi. Akimwakilisha Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Robert Manyerere, anasema kitaalamu mtoto huathirika kisaikolojia baada ya kubakwa, hasa pale jamii inapojua lililomkuta, wakiwamo watoto wenzie. Hapo anaingiwa na unyonge.

Dk. Pazi anasema mtoto ana uwezekano mkubwa wa kuwa na hali ya kutojiamini kwa chochote kinachomhusu, hata inaishia kumletea madhara katika utu uzima.

"Kisaikolojia mtoto anaweza akaathirika na kuchukia wanaume wote kipindi atakapokuwa mtu mzima kwa kuwaona kuwa hawafai ni wakatili," anasema.

### MAENDELEO JAMII

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Morogoro, Frolence Mwambene, anawataka wazazi waendelee kuelimika na kufuata mipango, mikakati na taratibu za kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wasichana, hali inayosaidia kudhibiti wahalifu wa ubakaji.

"Mwaka 2018/19 nilipokea taarifa za watoto saba kubakwa ambao kati yao watuhumiwa wamefikishwa mahakamani na kuchukuliwa hatua zinazostahili" anasema.

Florence anasema, halmashauri yao imeunda mabaraza ya watoto katika kata zote 31 za wilaya yanayojengewa uwezo ikiwamo wa kujihami dhidi ya ukatili wa kijinsia na kuripoti matukio na anakiri kuna mafanikio, matukio ya ukatili wa kijinsia kuwekwa wazi, tofauti na zamani, uelewa ulipokuwa duni.

Pia, anataja mbinu za kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wasichana wakishirikiana na wadau mbalimbali kwa kuanzisha vituo vya taarifa na maarifa na katika kata nane zilizopo kwenye tarafa sita za halmashauri yao; Mkuyuni, Bwakira, Matombo, Mvuha, Kisaki na Mikese.

Anasema, hadi sasa kuna watoaji elimu katika kata za Kisaki, Kibuko, Bwakira chini, Kiroka, Tomondo na Mkambarani vinajengewa uwezo wa kuelimisha jamii.

Florence anasema kwa kushirikiana na wadau wa upingaji ukatili wa kijinsia, asasi ya TGNP-Mtandao, wameelimisha jamii kuhusiana na mengi ya ukatili kijinsia, ikiwamo maradhi ya Ukimwi.

### MZIZI WA USHAWISHI

Ofisa Ustawi Jamii Wilaya ya Morogoro, Boniventure Sikujua, anaziasa familia kuungana na serikali kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa watoto, kwa kuwataja wanaobaka watoto, hata kama wanatoka ndani ya familia, ili kusaidia kukomesha tabia.

Sikujua anasema ukatili wa kijinsia kwa watoto unapaswa kuwekwa wazi, kwa sababu unasababishwa na mambo kadhaa, ikiwamo kukosa maadili, imani mbaya kama za ushirikina na tabia ya ulevi.

Ushauri wake ni jamii inapaswa kujenga tabia ya kumkamilishia mahitaji muhimu ya mtoto hasa wa kike, ikiwemo chakula, malazi na mavazi, kwani kuna wanafunzi wanaojikuta wanaingia kwenye mitego ya kubakwa, hadi mimba kwa sababu ya tamaa ya vitu vidogo, ikiwamo chipsi.

Mkataba wa kimataifa wa Haki za mtoto uliopitishwa miaka 30 iliyopita (CRC 30) bado unathamini kwa upana haki za binadamu ukizitazama katika historia huku ukipigania maisha ya watoto, ukiipa uwezo serikali kubadilisha sera na sheria zilizopo na kuwekeza katika yanayohusu maendeleo ya watoto.

Hapo ina maana ya kuwawezesha kupata lishe bora, ulinzi kiafya na elimu. Ni mkataba unaofafanua kimataifa, kuwapo tofauti kwa watoto wa sasa wakilinganishwa na wa zamani, sasa wakikabiliwa na changamoto za mabadiliko ya kiteknolojia, tabianchi na mapigano.

Katika maadhimisho yaliyofanyika Juni mwaka jana, wameangalia zaidi mitazamo ya baadae ya watoto na kuahidi kutimiza haki kwa kila mtoto kwa maendeleo endelevu.

Tanzania imeandaa mpango wa kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2022.

> Lakini tukipata mabweni na sisi itasaidia kuwachunga muda wote shuleni na kuwafikisha mbali kielimu.

### VIONGOZI KITAIFA

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipozindua kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, anasema serikali ina Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto unaolenga kupunguza ukatili dhidi ya makundi hayo mawili.

Anasema, ni sehemu ya utekelezaji wa: Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000; Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Jinsia wa Mwaka 2005; Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008' na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana - SOSPA ya Mwaka 1998.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015/2016 inakadiria asilimia 40 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 15 - 49 wameshafanyiwa ukatili wa ama kupigwa au kingono katika kipindi cha maisha yao.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka jana mkoani Geita, aliwataka wakuu wa mikoa ambayo bado haijaanzisha mabaraza ya watoto, kuianzisha haraka pamoja na madawati ya kulinda watoto shuleni, ili kuhakikisha ukatili huo inafika hatua ya kutokomezwa.

Aliitaja mikoa mitano inayoongoza matukio ya ukatili wa kijinsia nchini na tajkwimu zao katika mabano ndani ya mwaka ni ; Tanga (1,034), Mbeya (1,001), Mwanza (809), Arusha (792) na Tabora (616) na kwamba matukio yanayoongoza ni ubakaji na ulawiti.

## Kirusi corona chaua 12 Iran, 80,000 wafariki duniani kote



HOFU ya virusi vya corona inazidi kuwa kubwa baada ya kupanda kwa maambukizi mapya nchini Iran, Italia na Korea Kusini, ingawa kiwango cha maambukizi mapya kimeshuka ndani ya China ambayo ndiyo chimbuko la kirusi hicho.

Mkoa wa nne kwa ukubwa nchini Korea Kusini, Daegu, umetangaza marufuku yake ya kuingia na kutoka, huku idadi ya maambukizi mapya ikidaiwa inapanda juu kwa kasi.

Mashirika ya ndege ya Asian Airlines na Korean Air yamesitisha safari kwenye mji huo hadi Machi 9 na 28 ili kujiepusha na athari za ugonjwa huo.

Waziri wa Afya wa Korea Kusini, Kim Kang-lip, anasema endapo watashindwa kuzuwia kusambaa kwa kirusi hicho kwenye mkoa wa Daegu, kuna uwezekano wa kusambaa nchi nzima.

Hadi sasa, zaidi ya watu 700 nchini humo wameshaambukizwa.

"Kufikia leo Februari 24, idadi ya wagonjwa walioambukizwa kirusi cha corona imefikia 763. Miongoni mwao, 18 wamepona na wameruhusiwa kurudi nyumbani na saba wamefariki dunia. Wengi wa walioambukiwa wamepatikana kwenye Kanisa la Shincheonji mkoani Daegu na kwenye Hospitali ya Daenam mjinji Cheongdo," alisema waziri huyo.

Ligi ya soka imeahirishwa kwa muda usiojulikana kote Korea Kusini kwa hofu ya kirusi cha corona.

Aidha, watu wane walikufa Italia, 12 Iran, Ulaya na Asia zachukuwa tahadhari

Barani Ulaya, Waziri wa Afya wa Ufaransa Olivier Veran, anasema atakutana na wenzake wa Umoja wa Ulaya hivi karibuni kujadiliana njia za kukabiliana na kirusi corona na uwezekano wa kusambaa kwa kirusi hicho barani humo.

Hayo yanakuja wakati Italia ikithibitisha kifo cha mtu mwengine wa nne, na maambukizi ya wengine 150.

Maambukizi yameripotiwa katika mataifa ya Ghuba na Mashariki ya Kati, ambapo Iran imethibitisha vifo vya watu 12 hadi sasa na wengine 43 wakiwa wameshaambukizwa. Bahrain imeripoti mgonjwa wake wa kwanza na Kuwait imesema watu watatu waliowahi kutembelea Iran wamegunduliwa na kirusi hicho. Maambukizi mengi nchini Iran yamegunduliwa kwenye mji mtukufu kwa waumini wa madhehebu ya Shia wa Qom.

Saudi Arabia, Kuwait, Iraq, Uturuki na Afghanistan zimeweka masharti magumu kwa watu kuingia na kutoka Iran kupitia mipaka yao. **DW**

JE, WAJUA?

# ‘Wabongo’ wengi hupoteza muda kwenye simu



Vijana wakilemaa na simu mitaani wakati mwingine husababisha kugongwa na vyombo vya moto. **PICHA: MTANDAO.**

YAPO maelezo kuwa duniani kuna vitu vingi vinavyofautiana lakini suala la muda popote utakapokwenda liko sawa.

Ni kitu ambacho duniani kote kinalinga kwa maelezo kuwa bila kujali mahala ulipo iwe kusini au kaskazini, siku moja ina saa 24 na kila saa moja ina dakika 60, kadhalika wiki ina siku saba na mwaka ni ziko 365.

Huo ni ukweli usiopingika kuwa wanadamu wote wamepewa muda unaolingana hakuna anayeweza kusema taifa lake lina mwingi zaidi kuliko jingine, lakini kinachotofautisha mtu mmoja na mwingine ni namna wanavyotumia muda ambao unalingana kwa kila mwanadamu.

Muda ni rasilimali inayotajwa kuwa ni muhimu na ikitumika kikamilifu ni chanzo cha maendeleo na mafanikio makubwa na bila kusita Waafrika wanatajwa kuwa ni maskini kwa sababu hawajali wala kuheshimu muda.

Wanapolinganishwa na mataifa ya Asia, Ulaya na Amerika nchi hizo zimepiga hatua kubwa kimaendeleo tofauti na Afrika kwa zinajali, kutunza na kuheshimu muda. Tena kuna msemo wa Kiingereza husema ‘time is money, au muda ni mali, Waafrika wanatamba kwa kusema no hurry in Afrika.’

Msemo kuwa Waafrika ni jamii ya kudharau muda unadhihirika miongoni mwa Watanzania kwa mfano, wengi hawafiki kwenye miada kwa wakati. Si hivyo, tu wanachelewa mikutano, ibada na hata kwenye mahojiano ya ajira.

Kila mara wakiulizwa kisingizio ni kuwa kuna foleni barabarani hasa wanaoishi mijini au sababu zilizo nje ya uwezo wao.

Kupuuza muda ni suala la watu wengi hata watendaji wakuu na viongozi mbalimbali wa taasisi za umma na hata binafsi na hilo mara nyingi ni gonjwa linalowasumbua watu ambao hawahangaiki kulitibu na limeendelea kusababisha umaskini, vifo, njaa , kuyumba kwa familia, taasisi na taifa.

Wapo wajawazito wanaopuuza muda ikiwamo kwenda kliniki na hata siku ya kujifungua matokeo yake watoto hupoteza maisha, kuumia na hata mama mwenyewe kuwa na hali mbaya. Mama anashauri kuwa ni vyema kwenda kliniki akiona ana dalili za ujauzito hasa baada ya miezi mwili ila tofati na maelekezo watu hupuuza,

Si hivyo, wengi wanapokaribia kujifungua hupuuza kwenda zahanati, hospitalini na kwenye wataalamu wa rufani hupoteza watoto yao na wazazi hupoteza maisha au kupata matatizo ambayo kama wangewahi yasingetokea.

### TEKNOLOJIA Vs MUDA

Kiasi dunia inavyoelendelea kwenye sayansi na teknolojia Watanzania wengi hupoteza wakati kwenye simu. Ofisini bosi anachati na simu na kuongea na jamaa zake wakati kuna msururu wa wateja unamngojea mlangoni.

Kwenye ofisi za umma kuwaambia wateja wafike wakati mwingine ni suala la kawaida kisa bosi anachati na wasap, insta, au twita. Wagonjwa nao hospitalini wanakoma muda unapotea kwa sababu mganga, au mtaalamu wa maabara au wa vipimo kama X-ray na ultrasound anachati kwanza na simu .

Ni kupuuza muda na kutumia muda vibaya ndiyo maana hata wazazi na walezi nyumbani wanang’ang’ania kusoma ujumbe kwenye wasap na kujibu bila kuangalia kuwa watoto wao walioko shule wanafanya mazoezi na kufuatilia masomo kikamilifu.

Kwa wanandoa muda wa kujadiliana na kushirikishana mahaba na mapenzi, majukumu ya kifamilia mipango na changamoto zinazowakabili hakuna kwani kila mmoja anashikilia simu janja (smart phone) yake.

Wamewekeza muda mwingi kwenye kuchati na kuangalia mambo mbalimbali wanayotumiwa na washirika wake ambao ni zaidi ya makundi (groups) 20 aliyojiunga nayo.

Kuna kundi la wanakijiji alipozaliwa, kanisa analosali, shule na vyuo vikuu alivyosoma , wafanyakazi wenzake, wana vikoba na makundi ya ujasiriamali.

Ili kuhudumia makundi hayo anatumia saa tatu kila siku kufuatilia, kusoma na kujibu ujumbe mbalimbali. Je huko si kupoteza muda na kuutumia vibaya na hata kuwa mtumwa wa teknolojia? .

Kupoteza wakati ni jambo ambalo wengi wanalikubali. Haliwasumbui kwa mfano kwenye foleni barabarani abiria na madereva hawafikiria cha kufanya ili kukwepa foleni badala yake wanakaa ndani ya daladala au magari yao kuanzia saa 11 jioni hadi saa 3:00 usiku wanapofika makwao.

### KUTUNZA MUDA

Kwa kila mmoja hujachelewa jifunze kutunza muda. Usiwe mtumwa wa simu kila wakati. Wanaokaa mijini hasa katikati ya miji yenye foleni ni vyema kutumia muda huo kujisomea masomo pengine kozi za jioni badala ya kujitumbukiza kwenye foleni jioni.

Pengine unakaa Dar es Salaam nenda Chuo cha IFM, Taasisi ya Ufundi na kwenye shule za lugha za kigeni, kama Kiingereza, Kichina na Kifaransa. Kama unaweza kusoma jifunze kwa muda huo ambao ungekuwa barabarani uwe umejifunza na kupata cheti au shahada kwenye kozi mbalimbali.

Aidha, ili kutunza muda wako ni vyema kuainisha mambo yanayosababisha wewe kupoteza wakati kama unapenda kuongea sana punguza achana kwenda kwenye madawati ya ofisi za wenzako kuongea . Jiulize unachoongea kina manufaa au tija yoyote ? Unazungumza nini je ni umbea? uongo? Unasengenya? Au unalosema linakunufaishaje?

Ukiona hakuna cha maana mbali na kumaliza nguvu (calories)acha. Kama umezoea kwenda kijiweni jiulize unapata faida gani kila siku kukaa kijiweni kuongea umbea siasa au michezo ambavyo jioni jua likizama hupati chochote?

Ukiona hakuna jifunze kufanya kazi hata kama huzipendi kwa mfano Wanaque jiingize kwenye kazi za ufundi. Zipo nyingi kama kuchanganya zege na kusaidia mafundi.

RIPOTI

# WHO yaonya kupuuza kansa

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeonya kwamba ikiwa hali ya sasa itaendelea, dunia itashuhudia ongezeko la asilimia 60 wagonjwa wa saratani katika miaka 20 ijayo.

Ongezeko kubwa la takriban asilimia 81 ya kansa linatokea katika nchi maskini, ambapo viwango vya kuishi viko chini sana.

Hii ni kwa sababu nchi hizi kwa muda zimelazimika kuwekeza rasilimali kidogo za kiafya katika kupambana na magonjwa ya kuambukiza na kuimarisha afya ya mama na mtoto, wakati huduma za afya hazina vifaa vya kuzuia, kugundua na kutibu saratani.

Mwaka 2019, zaidi ya asilimia 90 ya nchi maskini ziliripoti kuwa huduma kamili za matibabu ya saratani zinapatikana katika mfumo wa afya ya umma ikilinganishwa na chini ya aslimia 15 katika nchi zilizoendelea.

Akizungumzia ripoti hiyo Dk.Ren Minghui, Mkurugenzi Mkuu Msaidizi, huduma ya afya kwa wote na magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukiza anasema, “huu ni wito kwa wote kushughulikia tofauti za usawa kati ya huduma za saratani katika nchi tajiri na masikini.”

Anaongeza, “iwapo watu wanapata huduma za msingi basi saratani inaweza kugundulika mapema, kutibiwa vizuri na kupona. Haipaswi kuwa adhabu ya kifo kwa mtu yeyote, mahali popote. “

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk Tedros Adhanom Ghebreyesus anasema, “angalau maisha ya watu milioni saba yangeokolewa katika kipindi cha miaka 10 ijayo kwa kutambua sayansi inayofaa kwa hali ya kila nchi ili kushughulikia saratani kupitia mifumo ya afya ya umma kwa wote na kwa kuhamasisha wadau mbali mbali kufanya kazi kwa pamoja.” **BBC**



Dawa kutibu na vifaa tiba kwa ajili ya uchunguzi ni muhimu kwa ajili ya kukabiliana na saratani. **PICHA: MTANDAO**



UCHAMBUZI
**NA MICHAEL ENEZA**

# Je, wajua asili ya jina Kawe?

KUNA usemi kuwa 'kila mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake.' Ni kanuni ya maisha kama ulivyo usemi mwingine wa kumaanisha kimo cha mtu katika maisha, hutambulishwa na hulka yake kuhusu maisha. Kimombo wanatumia 'attitude determines altitude.'

Ni hisia ukuaji wa kitu unatokana na anayehusika nacho, na kawaida katika maisha kuwa duka halifungwi kutokana na hali mbaya ya uchumi, ila kuna walakini katika huduma zake.

Inaelezwa hali mbaya ya uchumi inaongeza kasi na makali ya mashindano, hivyo wanaoshindwa wanakuwa wengi kuliko mwanzo.

Ukuaji uchumi na ukuaji lugha kwa njia moja au nyingine vinaendana, hivyo kunakuwapo vikwazo siyo kwa ukuaji wa lugha moja kwa moja, ila ufuatiliaji wa kukua huko na hapo kuna hali ya kushangaza kuwa, miji na lugha vinakua kwa njia zinazofanana.

Hali hiyo inaposhuhudiwa na mantiki yake kuwa wazi, inakuwa rahisi zaidi kupata kina cha mielekeo ya ukuaji lugha, kwani hapo kuna kitendawili kikali zaidi cha kuelewa vikwazo vyake.

Moja ya matatizo ya ukuaji miji kitamaduni na hasa kwa upande kwa Dar es Salaam, ni uhaba wa majina ya kutolewa katika mitaa; siju kama ni ukakasi au kigugumizi?

Mgeni anayeingia Dar es Salaam na akataka kujua jinsi majina ya mitaa inavyoonyesha historia ya nchi ya jiji, anaweza kushangaa anaishia majina kadhaa ya viongozi wakuu wa nchi na labda baadhi tu kati ya viongozi wengine waandamizi. Kihistoria majina hayo ni adimu.

Yanayoonekana ni yale ya jadi, ya wakazi wa awali au wahamiaji wa kwanza wakati jiji linapanuka,wenye majina tofauti na yale yanayounganishwa na wakazi wa awali.

Kwa mfano, simulizi (sijui ukweli wake kwa kiasi gani) Mikocheni inasemekana inatokana na mkazi 'Michael Chain' aliyekuwa eneo hilo kitambo,

Kawe ni 'cow way,' njia ya kupeleka ng'ombe katika kilichokuwa kiwanda cha nyama cha Tanganyika Packers, ambacho kimetoweka na uwanja wake ni ulingo wa mengine.

Pia, eneo la Msasani ni dai la mswahili aliyekuwa anaitwa 'Musa Hassani' ikidaiwa alitamkwa jina lake kwa lafudhi ya jamii ya wakazi mjirani wa kabila mojawapo la Kusini mwa nchi 'Mucha Chani."

Msingi wa mada hapa ni kwamba, linachozungumzwa hapo ni itachukua muda kamusi ya Kiswahili au ufuatiliaji wa maneno ya Kiswahili kutilia maanani utajiri huo wa vianzio, labda vile vinavyoendana na lugha zinazopendelewa na waratibu wa msamiati rasmi.

Jina la mtaa, Mwananyamala ni 'mwana nyamaza' kutowastua simba waliokuwa hawako mbali na hapo, hata ikiwa utajiuliza kama hiyo ni dawa? Ila ndio ilianza hivyo.



Askari wa Polisi Usalama Barabarani, akiwa katika Mtaa wa Makunganya, katikati ya jiji la Dar es Salaam. Ni jina lenye asili ya mkazi maarufu wa jiji. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Kawe ni 'cow way,' njia ya kupeleka ng'ombe katika kilichokuwa kiwanda cha nyama cha Tanganyika Packers, ambacho kimetoweka na uwanja wake ni ulingo wa mengine.



Wananchi wakiwa katika mitaa ya eneo la Chang'ombe Unubini. Ni jina linalodaiwa kutokana na kuwepo historia ya makazi ya jamii ya Wanubi, wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Ukija katika maeneo ya mitaa ambayo kimsingi ni njia (street) si rahisi kuona majina ila ya barabara muhimu, ambako viongozi wakuu wanaongoza na baadhi ya mawaziri kama Barabara ya Shekilango, iliyopo Sinza, ni kwamba aliyekuwa waziri na alikufa ajalini katika miaka ya 1980 na wakamuezi kwa kumpa jina la mtaa.

Maeneo mengi kwa sasa kuna majina yasiyo na sababu za zinazopaswa kubebesha jina mtaa. Ni kawaida mitaa mingi hasa ya 'vichochoroni' imeibuka kupewa jina la moja wa kazi wa eneo hilo.

Hapo ndipo kuna maswali ya msingi kutetea utamaduni yanapoanza, kwanini majina ya wanasiasa wazawa waliokuwa madiwani au meya jijini zamani, yanatajwa kwa tabu katika mitaa ya jiji hilo kongwe?

Ikirejewa katika lugha yenyewe, mamlaka zinazohusika na kufuatilia ukuaji wa lugha, zinapenda zitunge au ziunde maneno yaingizwe kwenye kamusi na yaelekezwe shuleni na kuanza kutumika, kwa kadri mahitaji yalivyo.

Ipo misamiati iliyofaulu kama vile, 'email' ambayo ni barua pepe imeshika kasi. Iko wazi, tekinolojia hiyo imekuwa sehemu ya maisha, tofauti na tekinolijia kama ya faksi kwa zama hizo, si muda mrefu sana, matumizi zaidi yaliishia ofisini.

Yako maneno yaliyoundwa mtaani, ambayo mwishowe yamekubalika kwa wafasiri na wasawiri, kwani hayapingani kimsingi na hisia zao.

Kwa mfano neno 'tapeli' lenye msingi wake kutoka lugha Kifaransa 'taper `a l'oeil' (kugonga jicho kwa tafsiri ya baki bandua).

Kwa matamshi yake ni Kiswahili, kiasi ambacho siyo rahisi mtu kulibishia, kutokana na lilivyoanzishwa na yapo mengine misimu yanayoendana ma wakati maalum, mengi hayakubalii sana si mahali pake kupajadili kwa kina.

Suala la msingi hapo ni kwamba, kuna vizuizi vya kitamaduni, ambavyo eneo linaloweza kuwa linahodhi nyenzo za lugha, ikawa na ama na mchango au kushawishi msemo wa lugha, kulingana na mchango ikiwamo pia katika majina ya mitaa.

Ni vyema kurejea maswali na fikra zilizowezesha wodi tatu za Hospitali ya Taifa Muhimbili kuoewa majina; Sewa Haji, Mwaisela na Kibasila.

Vivyo hivyo iende kwa ukumbi wa Karimjee, shule za Kibasila, Tambaza na Azania ili wanafunzi wa leo serkondari za Kata watembee na historia hai.



WADAU
SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

## Wanafunzi kutembea umbali mrefu kuafuata elimu na pia kukosa chakula shuleni ni miongoni mwa matatizo yanayowakumba baadhi yao na kusababisha wawe watoro. Wadau wanasemaje?



**ROGERS KAITIRA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HILO halina ubishi, ni kweli kwamba wanafunzi wengi bado wanapata changamoto ya kifedha, ingawa ada imetolewa shuleni, wanafunzi maskini wa Kitanzania bado hawana uwezo wa kuenda shule kwa sababu ya gharama zingine za kielimu, kwani wazazi wao au walezi hawana uwezo wa kuwalipia nauli ya kwenda shule, sare na mahitaji mengine kama vitabu.

Shule za sekondari zinapokua mbali, wanafunzi wakati mwingine inawabidi wapange kwenye hosteli binafsi au wakae mabwenini karibu na shuleni; familia nyingi maskini haziwezi kumudu hili.

Hii inakua changamoto kubwa kwa watoto kutoka familia maskini na kusababisha wawe watoro.

Kwa ujumla ni kwamba wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda shule ni tatizo, halafu wakati mwingine wazazi na walezi nao ni tatizo, hasa kwa kukataa kuchangia chakula wakidai kwamba serikali ilishaamua kutoa elimu bure.

Matokeo yake ni watoto wao kujikuta wakikosa hata uji shuleni.

Hebu fikiria mtoto anayetembea umbali mrefu kuafuata elimu halafu kule shuleni hakuna chakula, anaweza akasoma vizuri kweli? Hapa kuna mambo kadhaa ya kufanya.

Kwanza wanafunzi wasome katika shule za karibu na maeneo yao, kwani ndilo lengo la serikali, wazazi wachangie chakula na pia kila shule iwe na bweni ili wale wanaopanga mitaani wawahamie huko kuliko kuendelea kuishi mazingira hatarishi, hasa hao wa kike ambao ni rahisi kushawishika na kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na hatimaye kukatisha masomo.



**RICHARD KITAMBO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

INAUMA sana kuona wanafunzi wakitembea umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shuleni na kurudi. Ni kwanini wapelekwe shule za mbali wakati sekondari za kata zimeanzishwa ili wanafunzi wasomee karibu na maeneo ya nyumbani kwao? Sababu ni ipi inayochangia wanafunzi kuendelea kutembea umbali mrefu kufuata elimu?

Halafu katika mazingira hayo, unakuta hawapati chakula, kwa maana kwamba wanashinda na njaa, sijui kama wanaweza kusoma vizuri. Si wanafunzi wa mijini wala wa vijijini, wote wanakumbana na changamoto kusafiri umbali mrefu kwenda shule. Tofauti zao ni kwamba wale wa mijini wanawahi vituoni kupanda daladala, wakati wale wa vijijini wanaamka mapema kutembea kwa miguu au kutumia baiskeli kwenda shule.

Lakini kimsingi wote wanatakiwa kusaidiwa kuondokana na adha hii ambayo kwa namna moja ama nyingine inachangia kuwashusha kitaaluma. Kwa kuwa serikali ilianzisha sekondari za kata kwa lengo la kusogeza huduma ya elimu karibu na wananchi na kuwapunguzia wanafunzi kutembea umbali mrefu, basi hilo lionekane likitimia, ikiwezekana kuwe na sekondari za vijiji badala ya kata tu, ambazo unakuta vijiji viko mbali na kulazimisha wanafunzi kutembea umbali mrefu au kutumia usafiri wa baiskeli, hali ambayo kwa kweli ninadhani siyo salama kwao.

Halafu bahati mbaya ni kwamba baadhi ya wazazi hawajawa na mwamko wa elimu, hawako tayari kuwasaidia watoto wao kupata chakula shuleni wakiamini kuwa hiyo ni kazi ya serikali, hawa wanatakiwa kubadilika.



**BATULI MANGALA (MKAZI WA BAGAMOYO PWANI)**

KUNA haja ya kujadili kwa upana hili jambo, kutokana na ukweli kwamba lina changamoto nyingi kwa wanafunzi.

Serikali imeanzisha sekondari za kata ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania mwenye uwezo kiakili anaendelea na masomo ya sekondari, lakini lengo hili limegauka kuwa shubiri kwa baadhi ya wanafunzi, hasa kwa yale wanayokutana nayo njiani wanapokwenda shule au kurudi nyumbani.

Wanaoathirika na vitendo viovu ni wale wanaotembea umbali mrefu kwenda shule na kujikuta wakikumbana na vishawishi vikiwamo vya kujiingiza kwenye mambo ya ngono, huku wengine wakijiunga na makundi ya kihuni.

Aidha, kuchelewa kufika shuleni kwa wakati nayo ni changamoto nyingine inayowakabili. Unakuta wengine wanatoka nyumbani saa kumi alfajiri kwenda shule na kufika hata saa mbili asubuhi kutokana na adha ya usafiri wa kuwa wanakataliwa kupanda daladala. Lakini mbaya zaidi ni kwa wenzao wanaosoma sekondari za kata za vijijini.

Unaweza kukuta mtoto hana baiskeli, analazimika kutembea kilometa kumi kwenda shule na mazingira ya vijijini unayajua si salama sana kwa mtoto wa kike. Au unakuta wawili wanatumia baiskeli moja kwenda shule. Lakini bado ni shida kwao ila hawana namna nyingine ya kufanya na inawezekana kwa wale wasiopenda shida wakakata tamaa na kuwa watoro au kuacha



**MARIAM MJAGA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SISI ambao tumesoma katika shule hizo vijijini, tunajua changamoto zake. Ukweli ni kwamba umbali wa shule una athari nyingi kwa wanafunzi, miongoni mwake ikiwa ni utoro.

Halafu wakichelewa kufika shule, wanaweza kupewa adhabu ikiwamo ya viboko bila kujali wanatoka umbali kiasi gani na wanatumia usafiri gani. Sasa katika mazingira hayo, wengine wanaweza kukata tamaa kwa kudhani kuwa shule ni mateso.

Ila niwatie moyo kwamba maisha ya shule ni safari ndefu inayohitaji uvumilivu, kwani yana changamoto zake ingawa nyingine zinaweza kuwa chini ya uwezo wazazi wetu.

Yaani ni kwamba wazazi ni kiungo muhimu katika maendeleo ya watoto wao shuleni, hivyo wanatakiwa kuhakikisha watoto wao wanasoma katika mazingira ambayo yanaweza kuwasaidia kuepuka baadhi ya matatizo yaliyo chini ya uwezo wa wazazi wao.

Kwa mfano suala la ujenzi wa mabweni, kuwapo chakula shuleni, wanaweza kushiriki kuhakikisha watoto wao wanaishi mazingira salama na kupata chakula shuleni, kuliko kuwaacha wakitembea kilometa zaidi ya nane kufuata elimu bila kujali kuwa wanateseka.

Maisha ya shule ni safari ndefu inayohitaji uvumilivu, lakini pale ambapo ni muhimu kuingilia kati kuowandolea matatizo, wazazi wasione kama jambo la kawaida watoto wao na hasa wa vijijini wakipanga katika nyumba za uraiani kutokana na ukosefu wa mabweni na kumbe si salama kwao.



**EZZA TIMBA (MKAZI WA JIJINI MWANZA)**

SUALA la umbali wa shule ni muhimu lifanyiwe kazi kwani madhara yake kitaaluma ni makubwa kwa wanafunzi.

Wanafika shuleni wakiwa wamechoka, hata kuhisi njaa hali ambayo inawafanya wakose usikivu au kufuatilia masomo, kwasababu ya uchovu wa mwendo mrefu iwe kwa usafiri wa gari, baiskeli au miguu.

Kumbuka kwamba hata wanafunzi wa mijini wanaosoma mbali wanakumbana na matatizo katika usafiri hali inayowafanya wachoke.

Hivyo suala la kuwapunguzia umbali ni la muhimu ili waondokane na adha hiyo.

Hebu fikiria, mwanafunzi anasafiri umbali wa kilometa kama tano kwa miguu na kufikia kwenye vipi darasani, unadhani atakuwa na usikivu wa kutosha?

Halafu mbaya zaidi ni tatizo la kutokuwapo chakula shuleni, ambalo linawafanya baadhi ya wanafunzi kuwa watoro, kutokana na ukweli kwamba mazingira ya aina hiyo siyo rafiki kwao zaidi ya mateso.

Hebu wazazi wasaidie kumaliza tatizo hili, wasiiachie serikali kila kitu bali watambua kuwa shule ni zao wanatakiwa kuzihudumia kwa manufaa ya watoto wao.

Wasikae kimya wakisubiri kufanyiwa kila kitu. Shule hizo ni za umma, na umma wenyewe ni Watanzania kwa ujumla wao.



# Wanusa ufisadi ujenzi halmashauri

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mkoa wa Mbeya, imesema haijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ambao una miaka mitatu tangu uanze.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Bosco Mwanginde, ujenzi huo utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.6, lakini baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo wamedai kuwa na wasiwasi kwamba huenda mradi huo unasuasua kutokana na fedha kutafunwa.

Akitoa taarifa ya mradi huo mbele ya kamati hiyo iliyofanya ziara ya kukagua miradi wilayani humo mwishoni mwa wiki, Mwanginde aliieleza kuwa jengo hilo linajengwa na fedha za ndani za halmashauri na kwamba kusuasua kwa mradi huo kunatokana na uhaba wa fedha.

Kutokana na uhaba huo wa fedha, Mwanginde alisema halmashauri inalazimika kutenga kiasi kidogo kila mwaka kulingana na hali ya ukusanyaji wa mapato.

"Tunatenga fedha za kujenga kulingana na makusanyo yetu, lakini pia tunatenga fedha kidogo kidogo kwa sababu mradi huu si kipaumbele cha halmashauri, tuna miradi mingi ya kipaumbele ambayo inawagusa wananchi moja kwa moja," alisema.

Alisema tangu mradi huo ulipoanza mpaka sasa, wametumia Sh. bilioni 1.3 na wataendelea kutenga fedha hizo kutoka kwenye mapato ya ndani mpaka watakapomaliza.

Alisema halmashauri imekuwa ikituma maombi ya fedha Serikali Kuu kwa ajili ya mradi huo, lakini haijawahi kupatiwa fedha, hivyo kulazimika kuendelea na ujenzi yenyewe kwa fedha za ndani.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi (CCM) Mkoa wa Mbeya, James Mwampondele, alisema jengo hilo ni kubwa, hivyo likiendelea kujengwa kwa utaratibu wa sasa, hawatalimaliza.

Alishauri waanze kujenga kwa awamu ili liendelee kutumika huku ujenzi ukiendelea na kwamba kwa kutumia mfumo huo wataharakisha ujenzi kwa maelezo kuwa litakuwa linawakera.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye kwenye kamati hiyo ni mjumbe, alisema mfumo wa kutenga fedha kwa kila mwaka unatoa mwanya kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu kufanya udanganyifu na kuiba fedha za umma.

Alisema kama halmashauri haitaweka muda wa ukomo kukamilisha mradi huo, watajikuta wakitumia miaka mingi bila kuona tija yoyote na badala yake baadhi ya watu watautumia kama shamba la bibi kujinufaisha.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, aliwataka viongozi wa halmashauri kuzingatia ushauri uliotolewa na kamati ya siasa ya mkoa pamoja na wataalamu wa majengo ili mradi huo uwe na tija.

Pia aliwataka kuwa makini kwenye matumizi ya fedha za umma kwa maelezo kuwa serikali ya sasa haitamfumbia macho mtu yeyote anayefanya alichokiita uhuni.

## RC abaini tatizo vijana kusaka nguvu za kiume

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka vijana mkoani humo kuacha kwenda kwa waganga wa kienyeji kutafuta nguvu za kiume, akieleza kuwa nguvu hizo hazipatikani kwa waganga bali kwenye pesa.

Chalamila alitoa kauli hiyo juzi wilayani Rungwe alipozungumza na vijana wanaoendesha pikipiki za abiria, maarufu bodaboda, ambao wamekopeshwa pikipiki hizo na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe.

Aliwataka vijana kuwekeza nguvu zao kutafuta fedha kwa maelezo kuwa hizo ndiyo nguvu za kiume na siyo zile wanazofuata kwa waganga wa jadi.

"Acheni kwenda kwenye vibao vilivyoandikwa 'dawa ya kuongeza nguvu za kiume', fedha ndiyo nguvu za kiume, maana ukiwa nazo hata mwanamke wa kumuoa utampata. Kwa hiyo, vijana wangu fanyeni kazi," alisema.

Chalamila alisema halmashauri imetoa mkopo huo usio na riba ili kuwasaidia, lakini wasipokuwa makini, watajikuta wanashindwa hata kulipa mkopo huo.

Aliwataka warejeshe mkopo huo ili wananchi wengine wakopeshwe na kujiletea maendeleo kwenye familia zao na jamii inayowazunguka.

Alizitaka halmashauri kuendelea kukopesha vikundi vya wajasiriamali vifaa badala ya fedha kwa maelezo kuwa fedha huwa zinaishia kutafunwa na kuwagombanisha wanachama wa vikundi hivyo badala ya kuwaletea maendeleo.

**"Acheni kwenda kwenye vibao vilivyoandikwa 'dawa ya kuongeza nguvu za kiume', fedha ndiyo nguvu za kiume, maana ukiwa nazo hata mwanamke wa kumuoa utampata. Kwa hiyo, vijana wangu fanyeni kazi," alisema.**



Wafanyakazi wa kampuni ya ukandarasi ya China Railway 15 Bureau Group Corporation, anayejenga barabara ya Chunya-Makongolosi yenye urefu wa Km 39, wakiendelea na kazi za ujazaji wa mawe na kifusi katika Daraja la Chipoka, mkoani Mbeya juzi. **PICHA: WUUM**

# Wazazi washtuka shule yenye wanafunzi 3,000

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANANCHI wa Kata ya Nsalaga katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wameanza kufyeka vichaka na kuondoa takataka kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari tisa ili kuanza ujenzi wa shule ya sekondari.

Wananchi hao wameamua kuanza ujenzi wa shule hiyo mpya ili kukabiliana na msongamano wa wanafunzi kwenye shule ya sekondari iliyoko katika eneo hilo ikiwa na wanafunzi zaidi ya 3,000.

Wakizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki wakati walipokuwa wanasafisha eneo hilo, wananchi hao walisema eneo hilo lilikuwa limegeuka kuwa pori katikati ya mji.

Mmoja wa wananchi hao, Charles Mwandemba, alisema miaka 20 iliyopita, eneo hilo lilikuwa linatumika kwa ajili ya kuogeshea mifugo na baadaye likawa halitumiki, hivyo kugeuka pori ambalo hata baadhi ya vibaka walikuwa wanajifichа.

Alisema wananchi wa kata hiyo walikubaliana kulibadili matumizi ya eneo ili kujengwe shule ya sekondari ili kupunguza msongamano wa wanafunzi kwenye madarasa ya shule yao ya kata.

"Baada ya kuona shughuli za kuogesha mifugo zimesimama kwa muda mrefu katika eneo hili na wanafunzi wanapata shida, wananchi wote tulikubaliana kujenga shule mpya hapa na ndiyo maana mnaona watu wamejitokeza kwa wingi," alisema.

Naye Justine Ngoko, mkazi wa kata hiyo, alisema wananchi wengi walishauri ujenzi huo uanze ili kama itawezekana ianzishwe shule ya kidato cha tano na sita katika eneo hilo.

Alisema katika bonde lote la Uyole, hakuna shule hata moja yenye kidato cha tano na sita, hivyo watoto wakifaulu, wanalazimika kwenda shule za mbali na kuongeza gharama kwa wazazi.

"Tunaamini hii shule ndiyo itakuwa mkombozi wa watoto wetu, kwa sasa katika bonde hili shule zetu zote zimeishia kidato cha nne, sasa jiulize watoto wote wanaofaulu wanaenda wapi?" Alihoji.

Diwani wa Nsalaga, Mchungaji David Ngogo, alisema kwa miaka ya karibuni, wakazi wa kata hiyo wamekuwa wakiongezeka kwa kasi kubwa kutokana na wengi kuhamia kutoka katika maeneo mbalimbali.

Alisema kutokana na kasi hiyo ya ongezeko la watu, shule ya sekondari iliyopo, haitoshelezi mahitaji na ndiyo maana wameamua kuungana ili kujenga shule mpya.





# Viongozi wa dini watakiwa kukemea kauli tishio amani

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Felister Bura, amewataka viongozi wa dini kukemea wanasiasa wanaotoa kauli za kuhatarisha amani.

Kauli hiyo aliitoa juzi alipokuwa akizungumza na viongozi na waumini kutoka madhehebu mbalimbali ya dini kwenye ibada ya kumsimika Askofu wa Jimbo la Dodoma wa Kanisa la Tanzania Mothodist Church, John Mjelwa.

Bura alisema viongozi wa siasa hawapaswi kuogopwa.

"Baadhi ya maaskofu na wachungaji wamekuwa wakiwahofia viongozi wa siasa kutokana na dhambi zao wanazozifanya, badala yake wamekuwa wakiwapaka mafuta na kuonekana kama vile hawastahili kuonywa, tambueni kwa Mungu watu wote ni sawa," alisema Bura.

Aidha, aliwataka wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuunda vikundi ili kupata mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na halmashauri.

Alisema fedha hizo zipo, kinachotakiwa ni kuunda vikundi ili kupatiwa na kuanzisha miradi ya uzalishaji ili kuondokana na umaskini.

"Hivi sasa kutokana na kuwapo kwa fursa nyingi, baada ya mkoa wetu kuwa Makao Makuu ya serikali kumesababisha kuwapo kwa fursa nyingi zinazoweza kuongeza uchumi kwa kila anayefanya kazi," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Joseph Bundala, alisema kuwa kanisa litaendelea kukemea matendo maovu bila kujali nafasi ya kiongozi au muumini, kwa kuwa wasipofanya hivyo watakuwa wakishiriki dhambi hizo.

"Sisi kama viongozi wa dini kamwe hatutakubali kuwakumbatia wanasiasa au waumini ambao wanaokwenda kinyume cha maandiko ya Biblia takatifu ambayo kwa sehemu kubwa imekuwa ikionya juu ya madhara ya dhambi," alisema.

Bundala aliwataka viongozi wa kanisa hilo na waumini wake kufanya kazi ya Mungu kwa ufanisi ambao utakaowaletea mabadiliko ya maendeleo na hasa katika suala zima la kujiinua kiuchumi kupitia shughuli wanazozifanya za kiroho na kimwili.

Naye Askofu John Mjelwa alisema moja ya mpango mkakati wake ni kuhakikisha waumini wa kanisa hilo wanafanya kazi ili kuondokana na utegemezi, ambao mara nyingi umekuwa ukisababisha umaskini.

## Miundombinu yakarabatiwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MIUNDOMBINU iliyoharibiwa na mvua kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dodoma, imeanza kukarabatiwa ili kurejesha mawasiliano yaliyokuwa yamekatika kutokana na athari hizo.

Kukatika kwa mawasiliano kulisababisha gharama za usafiri kupanda, huku baadhi ya maeneo yakikosa huduma za kijamii.

Akizungumza jana katika ukaguzi wa miundombinu hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema serikali itahakikisha inakarabati miundombinu ya barabara iliyoharibiwa na mvua zilizonyesha mfululizo hivi karibuni.

"Nia ni kurudisha mawasiliano katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua na kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli za maendeleo kwa ufanisi," alisema.

Dk. Mahenge alisema serikali inafanya juhudi kuhakikisha njia zote zinapitika haraka kwenye wilaya za Chemba, Dodoma, Bahi na Kongwa.

Alisema barabara zilizoharibika kwa kiasi kikubwa zitatengenezwa njia za muda mfupi ili baadaye matengenezo maalum yafanyike.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Leonard Chimagu, alisema barabara zimeharibika kutokana na kubadilika kwa mikondo ya maji.

"Sasa zile sehemu zilizokatika tumeziimarisha na tunaboresha sasa hivi, hivyo wananchi wasiwe na hofu," alisema.

**"Nia ni kurudisha mawasiliano katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua na kuwaruhusu wananchi kufanya shughuli za maendeleo kwa ufanisi," alisema.**



Muuzaji wa samaki, Joseph Mlinga (kulia), akipima kitoweo hicho kwa ajili ya mteja wake, Deonatus Costantine, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Samaki huyo aina ya sangara kutoka Ziwa Victoria, mwenye uzito wa kilo 15.7, aliuzwa kwa bei ya Sh. 37,000. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## CCM yajigamba ushindi wa kishindo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, imesema haina hofu ya kupata ushindi wa asilimia 100 katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kutokana na kazi iliyofanywa na serikali.

Akizungumza na wanahabari jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo mkoa, Dk. Damas Mukasa, alisema jukumu walilonalo kwa sasa kama kamati ya utekelezaji ya jumuiya hiyo ni kupita katika majimbo yote kumi ili kuzungumza mambo yaliyofanyika.

Alisema serikali imeitekeleza Ilani ya chama chake kwa vitendo na hiyo ndio silaha ya kupatikana ushindi katika kata zote, majimbo yote na kura nyingi katika nafasi ya Rais.

"CCM hatuna hofu ya ushindi katika uchaguzi ujao, lakini kama nchi yenye mfumo wa vyama vingi ni lazima tujipange, tujiandae na tuwakumbushe wanachama wetu kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura na kuhakikisha wanakuwa hai kwa kulipa ada, hilo ni jukumu letu," alisema Dk. Mukasa.

Aliongeza: "Ushindi wa CCM sio wa kubahatisha ni wa maandalizi, hivyo kila mwaka lazima tujiandae, kama wapinzani wataweka au hawaweki mpira kwapani ni hiari yao... lakini sisi tunajipanga kushinda kwa kishindo na ikiwezekana hata hao upinzani wenyewe waipe kura CCM."

Alisema ziara hiyo pia wataitumia kutoa elimu, kuzungumza na watoto, wazazi na walezi ili kuwakumbusha jukumu lao la kusimamia maadili kwa kuzingatia mila na tamaduni za Mtanzania.


"Rais Magufuli katika hotuba yake wakati wa uchaguzi wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa alitukumbusha jukumu letu la kusimamia maadili, hivyo jamii lazima maadili yaangaliwe maana yakiporomoka hatutakuwa na Taifa lenye heshima na amani," alisema na kuendelea:

"Na siku hizi sio watoto tu, hata watu wazima wanaonekana kujisahau na kutoka katika misingi ya kimaadili, hivyo lazima tuwarudishe."

Alitaja shughuli nyingine watakayoifanya katika ziara hiyo kuwa ni kuhamasisha suala la uchumi na kuhimiza kupanda mikorosho katika kila wilaya na kata.

"Siasa inaendana na uchumi imara, lazima tubuni miradi katika ngazi zote ili jumuiya yetu iweze kusimama imara katika kujitegemea... watu wapande mikorosho, watunze mazingira yote haya ni majukumu yetu lazima tuyatekeleze," alisisitiza mwenyekiti huyo.

**HABARI ZANZIBAR**



# Kiwanda cha sukari Mahonda champa waziri matumaini

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema serikali imepata matumaini makubwa ya mfumo wa uendeshaji wa biashara ya sukari na kusaidia kiwanda cha sukari Mahonda kujiendesha kibiashara.

Akitoa tamko la serikali kuhusu kukisaidia kiwanda hicho kujiendesha kibiashara, alisema wafanyabiashara wanaendelea kununua sukari katika kiwanda hicho na kuiuza Zanzibar.

Alisema serikali imedhibiti uingizaji holela wa sukari na sheria za kuzuia magendo zimeimarishwa.

"Serikali itaendelea kuwalinda na kuwasaidia na pia kuhakikisha wananchi wanapata sukari bora na yenye bei nafuu," alisema.

Vile vile, alisema serikali kupitia vikao vyake mbalimbali iliwezesha serikali kupata mfumo bora wa uendeshaji wa biashara ya sukari Zanzibar.

Alisema kiwanda sukari Mahonda kimefanya mageuzi makubwa ya uwekezaji ili kuhakikisha kuwa kinazalisha na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kulipa kodi ya serikali na kutoa ajira kwa wananchi.

Hata hivyo alisema kiwango kidogo kinachozalishwa na kiwanda hicho na gharama za uzalishaji zipo juu ambazo zinaifanya sukari hiyo kushindwa kiushindani wa bei ya soko la ndani na sukari inayoagizwa kutoka nje.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, Dk. Mwinyihaji Makame, aliwataka wafanyabiashara wauridhie mpango uliowekwa na wizara ya biashara kuwapa fursa ya kuagiza sukari.

Alieleza kuwa Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya wimbi la wafanyabiashara wenye uzoefu tofauti ambao hutumia mwanya wa kusamehewa kodi kwa bidhaa ya sukari katika mwezi wa mfungo wa Ramadhani.

Alisema hoja ya sukari ya Mahonda kuuzwa Zanzibar pekee isipelekwe Tanzania bara haina mashiko.



Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa Jimbo la Dimani, Dk. Mwinyihaji Makame, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Njia uingizaji dawa za kulevya zatajwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KAMATI ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, imeishauri serikali kuongeza juhudi zaidi kudhibiti mianya ya uingizaji wa dawa za kulevya hasa katika maeneo ya bandari bubu.

Akiwalisha taarifa ya kamati hiyo katika baraza la wawakilishi Mwenyekiti wa kamati Panya Ali Abdallah alisema bandari hizo bubu zinaonekana kama ni chaka ambalo wahalifu wanalitumia katika kufanya jinai ya usafirishaji na uingizaji wa dawa za kulevya.

Alisema kuwa jitihada ya serikali dhidi ya mapambano ya dawa za kulevya iongezeke katika maeneo yenye mchanganyiko wa watu hasa wageni pamoja na maeneo ya fukwe za hoteli.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa vyombo vya usalama kushiriliishwa kikamilifu na kuwezeshwa ili waweze kusimamia suali hilo katika maeneo hayo.

Alisema kamati inasisitiza umuhimu wa nadharia nzima ya utekelezaji wa pamoja wa sheria za udhibiti wa dawa za kulevya hasa kwa taasisi za Mahakama ambayo inaonekana baadhi ya wanaoendesha kesi hizo hutumia udhaifu wa kisheria na hupindisha hukumu au kuwachia huru watuhumiwa wa dawa za kulevya.

Alisema kamati hiyo inaipongeza Tume ya kudhibiti dawa za kulevya kwa kuona umuhimu wa familia kuwa na utaratibu wa zamani wa malezi ya karibu zaidi baina ya wazazi na watoto.

"Kutokuwa karibu baina ya familia na watoto ni moja ya changamoto zinazosababisha watoto kujingiza katika masuala ya dawa za kulevya," alisema.

Wakichangia ripoti hiyo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walitaka serikali kuipatia vitendea kazi askari wa jeshi la polisi ili waweze kufanya majukumu yao kwa ufanisi hasa katika suala la kukamata wauzaji na watumiaji wa dawa za kulevya.

Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo alisema kuwa askari polisi wa kitengo cha dawa za kulevya wanafanya kazi katika mazingira magumu hivyo ni vyema wakapatiwa vitendea kazi ikiwamo gari kwa ajili ya kukamata wahalifu.

# 'Watanzania wanaosoma China wako salama'

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema wanafunzi wa Tanzania wanaosoma nchini China bado wako salama na hawajakumbwa na ugonjwa wa Corona.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohamed Saidi, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akimjibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Ramadhan Hamza Chande.

Mwakilishi huyo alitaka kujua wizara inachukua hatua gani za kuwasaidia wanafunzi wa vyuo vikuu wanaosoma nchini China kujikinga na ugonjwa wa maradhi ya Corona.

Alisema Serikali ya Zanzibar na Tanzania zinaendelea kufanya mawasiliano na wanafunzi wanaosoma China pamoja na kufanya mawwasiliano na ubalozi wa Chuna kuhusu kujua taarifa za wanafunzi wanaoendelea na masomo nchini China.

Alisema hadi sasa wanafunzi 157 wa Tanzania walioko China wako salama na hawajakumbwa na ugonjwa huo.

Wakati huo huo, akijibu swali la msingi aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua wizara inaweka mikakati gani kuhakikisha bajeti ya bodi ya mikopo Zanzibar inaongezwa.

Akijibu, Naibu waziri alisema wizara itaendelea kuiomba serikali kuongeza fungu la bajeti ya bodi ya mikopo ya elimu ya juu ili kukidhi ongezeko la wanafunzi wanaohitaji mikopo pamoja na kuongeza viwango vya malipo ya posho za wanafunzi za kujikimu maisha wakiwa vyuoni.

Alisema kwamba pia uongozi unatarajia kuendelea kutumia sehemu ya fedha za marejesho ya mikopo kwa matumizi ya bajeti ya mwaka 2020-2021.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa ofisi za makao makuu ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar, alisema wizara imeanza hatua ya kuanza michoro, kutathmini gharama za ujenzi na mataarisho ya nyaraka za zabuni.

Alisema kazi hiyo inafanywa na Zanzibar Building Authority" na baadae hatua ya kutafuta mkandarasi inafuata na inategemea kuanza ujenzi 2019-2020 amba ujenzi huo utafanyika katika makao makuu ya Wizara ya elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

## BOA yashukuru serikali, wadau

Na Sabato Kasika

BANK of Africa Tanzania Limited, imeishukuru serikali na wadau wote, ambao imekuwa ikishirikiana nao kwa kipindi chote cha miaka 13 tangu ilipoanza kutoa huduma za kibenki nchini.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Joseph Iha, akusema ushirikiano huo umeiwezesha benki kuendelea kutoa huduma zake vizuri nchini.

"Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, benki ilikuwa na mtaji wa kutosha unaotakiwa kwa kutoa huduma za kibenki nchini na hesabu za benki zilionyesha ilikuwa na mtaji wenye uwiano wa asilimia 17 dhidi ya unaotakiwa na mamlaka ya udhibiti wa benki wa asilimia 14.5," alisema Iha.

Alisema, kutokana na ushirikiano mzuri na serikali, benki, imeendelea kufanya shughuli zake vizuri na kwamba katika kipindi cha mwaka jana wamiliki wa benki waliongeza mtaji wa Sh. bilioni 22.9.

Alisema, lengo la kuiwezesha kutoa huduma ya mikopo na kuboresha huduma na kwamba benki ina mzunguko mzuri wa mtaji unaofikia uwiano wa asilimia 33 dhidi ya mtaji unaotakiwa na mamlaka ya udhibiti wa asilimia 20.

"Benki imekuwa ikipata faida katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015. Faida iliyopatikana baada ya kulipa kodi ni kiasi cha Sh. bilioni 12 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2017," alisema.

Alifafanua kuwa kodi hiyo ilitokana na ukuaji wa uendeshaji wa huduma za kibenki kila mwaka kwa asilimia tisa au Sh. bilioni 47, na kwamba kwa kipindi cha mwaka 2018 na 2019, benki iliboresha huduma za mikopo, na kwamba mchakato huo katika kipindi hicho cha mpito uliathiri faida ya benki.

Alisema, mwishoni mwa mwaka jana, benki ilipunguza uwiano wa mikopo chechefu kufikia Sh. bilioni 12, ambayo ni asilimia 9.2 kulinganisha na asilimia 16 ya mikopo hiyo iliyokuwa nayo katika kipindi cha kufikia mwishoni mwa mwaka 2018.

Alisema, ili kuelewa umuhimu wa kujumuisha wananchi kiuchumi, mwaka jana benki hiyo ilifanya uwekezaji wa zaidi ya dola za Kimarekani milioni moja katika miundombinu yake ya Teknolojia ya Habari (Tehama).

**"Benki imekuwa ikipata faida katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015. Faida iliyopatikana baada ya kulipa kodi ni kiasi cha Sh. bilioni 12 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2017," alisema.**

# Wasimulia Tasaf ilivyowainua kimaisha

Na Gideon Mwakanosya, TUNDURU

WAKAZI wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma wameupongeza mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) ambazo zimeweza kunufaika kwa kuwa na miradi ya maendeleo.

Baadhi ya miradi hiyo ni ya kilimo, ufugaji na ujenzi wa nyumba bora.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe kwenye mikutano ya uwezeshwaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, walisema Tasaf kwa Wilaya ya Tunduru imekuwa msaada mkubwa sana kwani imewajengea uwezo wananchi ambao wapo kwenye kaya maskini.

Dalia Abdalah Hassan, mkazi wa Kijiji cha Biasi nje kidogo ya mji wa Tunduru, aliishukuru Tasaf kwa kuwa ameshanufaika kwa mambo mengi ikiwamo kusomesha watoto wanne na amejenga nyumba ya bati yenye vyumba vitano na anaishi kwake bila bughudha.

Tabia Mnenga, mkazi wa Kjiji cha Tanesko anaye jishughulisha na kilimo cha miti ya maparachichi, michungwa, milimao, miembe pamoja na mikoro, lima kuwa kupitia mpango huo, Tasaf imemsaidia kununua malighafi ya viriba na tepu za kufungia.

Asha Salumu Bilali, mkazi wa Kijiji cha Misufini Kata ya Miungo, alisema Tasaf imemsaidia kununua bati 15 na boriti 55 kwa ajili ya kuezekea nyumba yake, huku na Mwajuma Kasim Mtoroka akisema Tasaf imemwezesha kujenga nyumba ya bati yenye vyumba vitatu na sebule na sasa anaishi na familia yake, hivyo ameishukuru serikali.

Mratibu wa Tasaf wilayani Tunduru, Muhidini Shaibu, alisema utekelezaji wa kunusuru kaya maskini ulianza mwaka 2014, na kuwa hadi sasa yamefanyika malipo kwa awamu ya 32 ambapo jumla ya vijiji 88 kati ya 157 vinatekeleza mpango huo kwa awamu ya kwanza.

Alisema jumla ya kaya zinazonufaika ni 13,751 na malipo ya Machi hadi Aprili 2019, jumla ya Sh. milioni 12 zilipokelewa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kutoka Serikali Kuu kupitia Tasaf kwa ajili ya malipo ya ruzuku kwa alengwa wanaotimiza masharti ya mradi.

Alieleza pia halmashauri ya wilaya hiyo imetekeleza miradi ya ajira za muda kwa walengwa kwa miaka mitano jumla ya miradi 424 imetekelezwa na walengwa ikiwamo utengenezaji wa mbolea kwa njia ya asili, kuandaa vitalu vya miche, miradi ya mazingira, kuboresha visima vya maji vya asili, kuchimba mabwawa ya samaki na malambo.



Wachuuzi wakipanga bidhaa zao kwenye eneo la Barabara ya Nyerere, jijini Mwanza jana, kitendo kinachosababisha usumbufu kwa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara hiyo, na pia wanaweza kuhatarisha usalama wa maisha yao. PICHA: NEEMA EMMANUEL

# Marufuku vyombo moto ndani ya soko

Na Neema Hussein, KATAVI

WAFANYABIASHARA wa soko la Mpanda Hoteli Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, wametakiwa kutoendesha vyombo vya moto pamoja na kupika chakula ndani ya soko hilo kuepusha ajali.

Akizungumza na wafanyabiashara hao baada ya kusoma taarifa ya mapato na matumizi, mwenyekiti wa soko hilo, Elisha Kang'ombe, alisema kuna watu wa aina mbalimbali wanaoingia katika soko hilo wakiwamo wenye ulemavu na watoto.

Kang'ombe alisema kutokana na makundi hayo, ajali inaweza kutokea muda wowote kwani hata wauzaji wenyewe wanakwenda na watoto na kuwaacha wakicheza na kuzunguka maeneo ya soko hilo.

"Kuanzia sasa ni marufuku kuendesha chombo cha moto humu ndani ya soko iwe gari, baiskeli, pikipiki... ni marufuku, kuna walemavu wanakuja humu kununua vitu, kuna wafanya biashara wanakuja na watoto wanacheza humu humu, je, mkiwagonga?" Alihoji.

Alisema atakayebainika atatoa faini ambayo wameazimia baiskeli ni Sh. 5,000, pikipiki ni Sh. 10,000 na gari Sh. 50,000.

Alisema kuna wafanyabiashara ambao wanapika chakula tofauti na mamalishe na wakimaliza wanaacha moto unawake, hivyo ajali ya moto inaweza kutokea na watu kupoteza mali zao.

Alisema wafanyabiashara 83 walikamatwa kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo utovu wa nidhamu kama kutukanana matusi ya nguoni, kuchomana visu na kununua vitu vya wizi kwa watu wasiowafahamu.

## HABARI KIMATAIFA

# India yajenga ukuta Trump asione umaskini wao

**NEW DELHI,** India

KATIKA hali ya kushangaza, Serikali ya India imejenga ukuta wa haraka kwa dhumuni ya kumficha Rais wa Marekani Donald Trump asione makazi ya watu masikini.

Rais Trump aliwasili mjini Ahmedabad, Magharibi mwa India jana katika ziara ambayo mataifa hayo mawili India na Marekani yanalenga kuimarisha upya uhusiano wao uliokumbwa mara kadhaa na mvutano wa kibiashara.

**Alipowasili, Rais Trump na mkewe walilakiwa na Waziri Mkuu, Narendra Modi.**

Alipowasili, Rais Trump na mkewe walilakiwa na Waziri Mkuu, Narendra Modi ambaye amejenga uhusiano wa kibinafsi na Rais Trump.

Modi alifanya juhudi zote kufanikisha ziara ya Rais Trump ijapokuwa mkataba wa kibiashara uliokuwa ukishinikizwa na Marekani umeingia matatani.

Serikali ya India imesema nchi yake na Marekani zimejenga uhusiano wa karibu wa kisiasa na kiusalama na kwamba ziara hiyo ya siku mbili ni ishara ya kuunganisha maslahi yao ya pamoja ikiwa ni pamoja na mbinu za kukabiliana na China kama taifa linaloinukia kuwa na ushawishi mkubwa duniani. **BBC**



Mafundi ujenzi wakijenga ukuta eneo la Ahmedabad ambalo linadaiwa wanaishi watu masikini, lengo kuu ni Rais wa Marekani, Donald Trump asione eneo hilo. **PICHA: REUTERS**

## Polisi, wanajeshi wafyatuliana risasi

**PORT-AU-PRINCE,** Haiti

SHIRIKA la habari nchini Haiti limeripoti kuwa mtu mmoja amefariki na wengine wengi wamejeruhiwa baada ya maandamano ya polisi ya kulalamikia kuhusu mazingira ya kufanya kazi, yaliyogeuka na kuwa vurugu.

Sherehe za kanivali katika Mji Mkuu wa nchi hiyo Port -au-Prince zimefutwa kuepusha umwagaji damu.

Jeshi la Polisi walifyatuliana risasi na wanajeshi kwa saa kadhaa baada ya maandamano yao kusimama karibu na ikulu ya kitaifa, haikubainika wazi ni upande gani ulioanzisha vurugu hizo.

Katika tukio hilo mamia ya wananachi walijiunga na polisi kuwaunga mkono.Takriban maofisa watatu wa polisi walijeruhiwa katika mashambulizi hayo ambayo wizara ya ulinzi inasema yalitekelezwa na washambuliaji waliokuwa wamevalia vinyago.

Kwa miezi kadhaa sasa, polisi nchini Haiti wametaka kuimarishwa kwa mazingira yao ya kazi ikiwa ni pamoja na haki ya kuunda chama chao kitakachoweza kuwasaidia katika masuala ya uwazi pale litakapohusika suala la kushughulikia madaraka ya polisi. **DW**

## Maambukizi ya Corona Iran, Italy, Korea

**TEHRAN,** Iran

HOFU ya virusi vya corona inazidi kuwa kubwa baada ya kupanda kwa maambukizi mapya nchini Iran, Italia na Korea Kusini, ingawa kiwango cha maambukizi mapya kimeshuka ndani ya China.

Mkoa wa nne wa ukubwa nchini Korea Kusini, Daegu, umepiga marufuku watu kuingia na kutoka, huku idadi ya maambukizi mapya ikipanda juu kwa kasi.

Mashirika ya ndege ya Asian Airlines na Korean Air yamesitisha safari kwenye mji huo hadi Machi 28.

Waziri wa Afya wa Korea Kusini, Kim Kang-lip, alisema endapo watashindwa kuzuwia kusambaa kwa kirusi hicho kwenye mkoa wa Daegu, kuna uwezekano wa kusambaa nchi nzima. Alisema zaidi ya watu 700 nchini humo wameshaambukizwa.

"Kufikia leo, idadi ya wagonjwa walioambukizwa kirusi cha corona imefikia 763. Miongoni mwao, 18 wamepona kabisa na wameruhusiwa kurudi nyumbani na saba wamefariki dunia. Wengi walioambukiwa wamepatikana kwenye Kanisa la Shincheonji mkoani Daegu na kwenye Hospitali ya Daenam mjinji Cheongdo," alisema Kim Kang-Lip.

Ligi ya soka imeahirishwa kwa muda usiojulikana kote Korea Kusini kwa hofu ya kirusi cha corona.

Barani Ulaya, Waziri wa Afya wa Ufaransa, Olivier Veran alisema atakutana na wenzake wa Umoja wa Ulaya hivi karibuni kujadiliana njia za kukabiliana na uwezekano wa kusambaa kwa kirusi hicho barani humu. Hayo yanakuja wakati Italy ikithibitisha kifo cha mtu mwengine wa nne, na maambukizi ya wengine 150.

Maambukizi yameripotiwa katika mataifa ya Ghuba na Mashariki ya Kati, na kwamba Iran imethibitisha vifo vya watu 12 hadi sasa na wengine 43 wakiwa wameshaambukizwa.

Bahrain imeripoti mgonjwa wake wa kwanza na Kuwait imesema watu watatu waliowahi kutembelea Iran wamegunduliwa na kirusi hicho.

Maambukizi mengi nchini Iran yamegunduliwa kwenye mji mtukufu kwa waumini wa madhehebu ya Shia, Qom.

Saudi Arabia, Kuwait, Iraq, Uturuki na Afghanistan zimeweka masharti magumu kwa watu kuingia na kutoka Iran kupitia mipaka yao.

Hadi kufikia jana jioni, Japan ilikuwa na wagonjwa 773, wengi wao wakiwa wale walio kwenye meli iliyowekewa karantini karibu na mji mkuu, Tokyo, ambako abiria watatu, mzee wa miaka 80 raia wa Japan, alikufa kwa kirusi hicho.

China ambako ndiko chimbuko la kirusi cha corona, imeripoti wagonjwa wapya 409, kutoka kiwango cha wagonjwa 648 kwa siku.

Hii inawafanya wagonjwa walioambukizwa kufikia 77,150 na kwamba idadi ya walipoteza maisha imependa hadi 2,592 kwa China. **DW**

## Gnassingbé atangazwa rais mpya

**LOME,** Togo

TUME ya Uchaguzi Togo (CENI) jana ilimtangaza Faure Gnassingbé kwa muhula wa nne kama rais wa Togo.

Kulingana na matokeo yote yaliyohesabiwa, Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Tchambakou Ayasso alimtangaza mgombea wa chama cha UNIR, Faure kuwa rais wa nchi hiyo.

Kulingana na takwimu kutoka CENI, Faure Gnassingbé alichaguliwa tena katika duru ya kwanza ya uchaguzi wa urais kwa asilimia 72.36 ya kura, sawa na karibu alama zaidi ya 14 wakati alipochaguliwa kama rais wa Togo mwishoni mwa mwaka 2015.

Kiwango cha ushiriki kilifikia 76 sawa na asilimia 63%, pia kiwango kikubwa zaidi kuliko mwaka wa 2015 wakati ambapo kiwango cha ushiriki kilifikia asilimia 61.

Waziri Mkuu wa zamani na mpinzani mkuu wa Gnassingbé, Agbéyomé Kodjo, alipata asilimia 18.37 ya kura. Kiongozi wa ANC, Jean-Pierre Fabre alishika nafasi ya tatu kwa kupata asilimia 4.35.

Ni mara ya kwanza kwa Tume huru ya kitaifa ya uchaguzi kutangaza haraka matokeo ya uchaguzi wa urais. Matokeo haya yatapelekwa kwenye Mahakama ya Katiba, ambayo ina siku sita ya kuyachunguza na kutangaza matokeo ya mwisho.

Kwenye akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa Twitter, Faure Gnassingbé alishukuru vijana wa Togo ambao wametakiwa kusherehekea ushindi huo kwa niaba ya demokrasia. **RFI**

# Ngome ya Sugu Mbeya yatikiswa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MADIWANI 11 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wakiongozwa na Meya wa Jiji hilo, David Mwashilindi, wamekihama chama hicho na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Viongozi hao walipokewa jana jijini Dodoma na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, huku akitamba kuwa mitambo aliyoweka ya majaribio kwenye mikoa jirani, imemfikia Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' kutokana na kundi hilo kutimkia CCM.

Madiwani hao mbali na Meya Mwashilindi, ni pamoja na Naibu Meya, Fanuel Kyanula, ambaye alikuwa Diwani wa Sinde, Fabian Sanga (Kata ya Ghana), Anyandwile Mwalubha (Isanga), Anderson Ngao (Mwasanga) na Kigenda Kasebwa (Viti Maalum).

Wengine ni Dickson Mwakilasi (Ilomba), Constatine Mwakyoma (Kalobe), Furaha Mwandaliwa (Ilemi), Ibrahim Mwampwani (Isyesye)na Katibu wa Chasema wilaya ya Mbeya Mjini, Henry Mwanyambaku, ambaye pia ni Diwani wa Forest.

Akizungumza baada ya kupokea wanachama hao, Dk. Bashiru alisema kundi hilo litaongeza nguvu na kuimarisha chama hicho kidemokrasia.

"Wamenieleza kwanini wanafanya uamuzi huo mzito, nimefurahi sana kwa kuwa kazi yangu ni kuhakikisha chama kinafurahiwa na Watanzania wote, nadhani sasa ratiba yangu ya kwenda Mbeya itabidi niwahi, niwahi haya maji bado ya moto nikutane na rafiki yangu Sugu.

"Mwaka jana nakumbuka nilimtumia salamu kuwa nakuja 'kusetí' mitambo, kumbe hii mitambo ninayofunga mikoa ya jirani inafika hadi Mbeya, ila lazima niende kufunga Mbeya mitambo maana kila mkoa una mitambo yake," alitamba.

Alisema hatua hiyo ni mwendelezo mzuri unaokipa heshima chama hicho na nguvu kwa kuwapokea viongozi waandamizi kutoka vyama vya upinzani.

"Huu ni mwendelezo na hadi sasa majimbo 10 kati ya 12 yamerejea CCM, haya mawili uchaguzi bado," alisema.

Kuhusu madai ya kulindwa na vijana wa CCM waliovaa mavazi ya polisi, Dk. Bashiru alisema hana sababu ya kulindwa na kwamba vyombo vya dola vinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kuwataka Watanzania kutumia vizuri mitandao ya kijamii hasa kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

"Nimemwambia ndugu (Hamphrey) Polepole aweke kwenye mitandao ya kijamii kuwa gari linalosemwa la Katibu Mkuu linalindwa si la Katibu Mkuu na ziara ya Mtwara haikuwa kama inavyowasilishwa na mtu anayepotosha wananchi," alisema.

Meya Mwashilindi alidai amerejea kwenye chama chake kwa kuwa alikuwa mwanachama tangu mwaka 1985.

"Sababu za kurudi ni kwamba nimekuwa mstahiki meya kwa miaka minne, nimeona kazi ya Rais, na unapozungumzia Tanzania, tunaona Tanzania mpya," alidai.

Aliendelea kufafanua kuwa Rais amepeleka miradi mingi kwa jiji hilo na ameona upo umuhimu wa kuunga juhudi hizo za Rais ili kusaka maendeleo.




Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Abdulkarim Mruma (wa pili kulia), akizungumza na Meneja Mahusiano wa Taasisi za Umma wa Benki ya NBC, Azza Mnzava (wa pili kushoto), baada ya kutembelea banda la benki hiyo, wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini jijini Dar es Salaam juzi. NBC ilidhamini mkutano huo. Wengine ni maofisa wa benki hiyo, Emmanuel Gasirabo (kushoto), Anthony Lugendo na Daniel Kaila. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ofisa awaangukia viongozi wa dini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

OFISA wa Maji Bonde la Wami Ruvu, Simon Ngonyani, amewaomba viongozi wa dini na kimila pamoja na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji katika bonde hilo.

Amesema kwa kufanya hivyo, watasaidia kuleta ustawi endelevu wa upatikanaji wa maji ya kutosha kwa matumizi ya viwanda na jamii.

Alitoa rai hiyo katika kikao cha uhamasishaji na utoaji elimu juu ya utunzaji wa rasirimali maji kwa viongozi wenye ushawishi kwenye jamii kutoka mikoa ya Tanga, Pwani, Dodoma na Morogoro.

Alisema amelazimika kueleza hayo kutokana na kukithiri kwa uharibifu wa mazingira unaofanywa kwenye vyanzo vya maji ndani ya Bonde la Wami Ruvu na kutishia uhai wa mito mingi inayotegemewa na wakazi wa mikoa mitatu ya Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Ngonyani alisema umuhimu wa bonde hilo ni mkubwa kutokana na maji yake kutumika kwenye uendeshaji wa Tanzania ya Viwanda katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro na matumizi ya kawaida ya wananchi wa mikoa hiyo.

"Sasa inabidi tuchukue hatua za haraka za udhibiti wake kwa kuwatumia watu hawa maarufu kwenye jamii na tusipochukua hatua, uharibifu utaendelea kuwa ni mkubwa na kuleta athari nyingi kwani uharibifu wa vyanzo vya maji ni mkubwa ikiwamo eneo la Kilosa," alisema.

Ngonyani alisema Mto Ruvu wenye chanzo chake kwenye safu ya Milima ya Uluguru mkoani Morogoro, wakazi wake wanalo jukumu la kuhifadhi na kulinda mazingira na vyanzo vya maji ili upatikanaji wake uwe uendelevu.

Alisema Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu pia imewawezesha baadhi ya wananchi kufanya shughuli mbadala baada ya kujengewa mabwawa ya samaki, miradi ya ufugaji wa nyuki na mabirika ya maji ya kunyweshea mifugo.

Askofu wa Jimbo Katoliki Morogoro, Telesphor Mkude, aliitaka jamii kutotanguliza ubinafsi, badala yake itangulize maslahi ya walio wengi kwa nyakati za sasa na zijazo.

Chifu Kingalu Mwanabanzi wa 15 aliishauri serikali iendelee kuweka kipaumbele kutoa elimu kwa viongozi wa dini, kimila na machifu ili nao waisambaze kwa jamii hasa vijijini ambako mazingira na vyanzo vya maji vinaharibiwa kwa makusudi.

# Mil. 510/- kutengeneza madaraja ya Mtwara

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

WAKALA wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Mtwara, umesema kuwa umepanga kutumia Sh. milioni 511.3 kwa ajili ya matengenezo ya madaraja mawili makubwa ya Mkwaya na Mchauru ambayo yako katika barabara ya Mbuyuni-Makongo'onda wilayani Masasi.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Tanroads mkoa wa Mtwara, Mhandisi Doto John, wakati wa kikao cha bodi ya barabara mkoani humo.

Alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 Tanroads imepanga kufanya matengenezo makubwa ya madaraja mawili ya Mkwaya-Mchauru ambayo kwa muda mrefu yamekuwa kero kwa wananchi wa vijiji hivyo.

John alisema madaraja hayo yapo wilayani Masasi katika Kata ya Makong'onda na moja lipo Kata ya Mchauru katika barabara ya Mbuyuni-Makong'okonda kuelekea wilayani Newala.

Alisema madaraja hayo yote yatagharimu jumla ya Sh. milioni 511.3 na kwamba mkandarasi wa kujenga madaraja hayo ameshapatikana ambapo daraja la Mkwaya ujenzi wake umeshaanza.

Alisema madaraja hayo yamekuwa kitovu kikubwa cha uchumi wa wananchi wa maeneo hayo, hivyo yatakapokamilika yatafungua fursa mbalimbali za kiuchumi kwa wananchi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

YUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA GULELO:, SELF VYUMBA 3 KIMOJA IASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA MEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, INISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. IWENYE NYUMBA **0757 804 970**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


### KUPOTEA KWA CHETI



**Revina Odilo Zeno** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S.4480/0064** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Mburahati

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/URA/RB/77673/2020**

115644502

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ELIZA GERALD MHEPELA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Mark II rangi ya Trim yenye namba za usajili T.346 BFX. Engine namba 1GFE1988 Chassis namba G1X1006049884.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

2156464

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.145/2019**
**ELIYA AMBAKISYE JONGO::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**FELIX JAMES MSUKWE:::::::::::::::MDAIWA WA KWANZA**
**YAH:KUITWA SHAURINI**

KWA : FELIX JAMES MSUKWE
Fahamu kwamba Eliya Ambakisye Jongo amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 26/02/2020 saa 2:30 asubuhimbele ya Mhe.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza

Unaamriwa kuhudhuriambele ya baraza siku hiyo bila ya kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba,mbeya mjini.

Kumbuka usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahiki ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

T. Munzerere
Mwenyekiti
10/02/2020

156453

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ROSE CHARLES MBAGA Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili T 960 BQD TOYOTA HIACE

Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi

Taarifa ya Polisi
ARU/ARU/RB/169901/2020

156451

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIA (MCA/63)**
**Mahakama ya mwanzo KARATU**
**Wilaya ya KARATU**
**TALAKA MADAI NAMBARI 01 YA 2020**
**MDAI JOSEPHINA MAIKO**
**AMDAI**

**MDAIWA FILBERT LOHAY**

Kwa **MIKATA OLDEAN**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameletwa /wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) **UNAHITAJIKA HAPA MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 28/02/2020 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo kwa siku hiyo ni siku ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini kutoa hukumu kuwa ummeshindwa /mmeshindwa .

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 14/02/2020

……………………………………..
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo.

215645201

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;39/2020**

Ombi la NYEMBO HARUN LEMBA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HARUN JUMA LEMBA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 5/3/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 21/02/2020.

Sahihi ya Hakimu

156447

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**JS GROUP COMPANY LIMITED** amepotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 942 CCA.Aina yake HAUJOE.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha

Polisi Taarifa:
MOR/MOR/RB/159376/2020.

215644802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;34/2020**

Ombi la **SAID SALEHE MSANGULE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SALEHE SAID MSANGULE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 12/02/2020.

215644902

### KUPOTEA KWA CHETI



**Renatha Charles Sindabaha** anatanagza kupotea ka vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0620/0074** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika Shule ya Sekondari Tegeta, Cheti cha kidato cha Sita chenye index namba S0698/0585 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Eckenford. Cheti cha cheti cha BA Kilichotolewa na chuo cha University of Dodoma kilichotolewa mwaka 2011, cheti cha kuzaliwa na cheti cha ndoa.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: WMB/RB/160/2020**

115644102

### KUPOTEA KWA CHETI



**Ernest Mutembei** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071-0366** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari St. Matthew's..

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**DAR/JNI/RB/466285/2019**

156440

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PGT COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDCRUISER** Prado yenye namba za usajili **T522 DQX** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania aina ya. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**OB/RB/122/2020**

156442

### KUPOTELEWA NA CHETI



**JOSEPH DIETER LUAMBANO** AMEPOTELEWA NA CHETI CHAKE CHA KIDATO CHA SITA, CHA SONGEA BOYS SECONDARY SCHOOL CHENYE NAMBA **S.153/0533** CHA MWAKA 1998. CHETI HICHO KIMEPOTEA AKIWA SAFARINI NA KINAHOFIWA KUPOTELEA KATIKA WILAYA YA BUKOBA AU NGARA MKOANI KAGERA.

AMETOA TAARIFA POLISI YENYE NAMBA
KAG/BUK/RB/169608/2020
KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU AWASILIANE NAYE KWA NAMBA 0784-312836.

156444

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**
**(Rules 13(civil Procedure of Summons and Pleadings)**
**Rules. 1955 G:N.NO**
**Cap. 2 Supposed. 64**
**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**MISC CIVIL APPL No. 50 OF 2019**
**DAUDI CHIMOSA APPLICANT**

**1.LISOUS LIGHT FINANCIL LIMITED DODOMA AND AMOS EZEKEIEL DODOMA**

**TAKE NOTICE** that mention above Case suit has been set down on the 26th day of February 2020 You must produce on that day all witness upon whose evidence and all the documents upon which you into to support of your Case.

Given Under my hand and seal of the court this 13th day of February 2020

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA

156439





Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei

Poa Tupigie 0782253676


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TUCHEL AMTETEA NEYMAR KWA KADI NYEKUNDU




**PARIS,** Ufaransa

FOWADI wa Paris Saint-Germain, Neymar aliepuka kulaumiwa baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu wakati wa ushindi wa 4-3 dhidi ya Bordeaux juzi Jumapili baada ya kocha, Thomas Tuchel kukataa kumshutumu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alioneshwa kadi ya pili ya njano na kuzaa nyekundu baada ya kumchezea faulo, Yacine Adli wa Bordeaux katika muda wa nyongeza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1 pale Parc des Princes.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alibwatukiana kwa hasira na mwamuzi, Willy Delajod kabla ya kuondoka dimbani.

Hata hivyo, Tuchel anaamini kile alichokifanya Neymar ni jambo la kawaida na la kibinadamu hasa baada ya kutoka kufanyia faulo na mchezaji mwingine wa Bordeaux, Youssouf Sabaly.

Neymar sasa ataukosa mchezo unaofuata wa PSG wa Ligue 1 dhidi ya Dijon Jumamosi.

"Tumezungumza kuhusu hali yote ilivyotokea," alisema Tuchel akimzungumzia Neymar wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Alichokifanya ni cha kawaida kwa binadamu. Halafu mchezaji wa Bordeaux hakupewa hata kadi ya njano."

PSG ilipata ushindi huo kwa mabao ya Marquinhos aliyefunga mawili, Edinson Cavani aliyefikisha mabao 200 kwa klabu hiyo na Kylian Mbappe.

# Roma yataka kuwasajili jumla Smalling, Mkhitaryan

**ROME,** Italia

KOCHA wa AS Roma, Paulo Fonseca amesema kikosi chake hicho kitaka kuwasajili moja kwa moja Chris Smalling na Henrikh Mkhitaryan ambao wanacheza kwa mkopo hapo.

Smalling na Mkhitaryan walitua kwenye klabu hiyo kwa mkopo wa muda mrefu wakitoka klabu za Ligi Kuu ya England, Manchester United na Arsenal.

Mlinzi wa kati wa United, Smalling amekuwa na wakati mzuri pale Roma, ambao sasa wanataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu mchezaji huyo wa timu ya taifa ya England.

"Chris ni mtu mzuri, ni mchezaji mzuri na mwenye kipaji," alisema Fonseca akiiambia Sky Sports News.

"Kuzoea soka la Italia ilikuwa rahisi kwake. Ni kijana mabaye kila mmoja anampenda klabuni hapa kwa sababu ni mchezaji mzuri.

"Ningependa kubakia na Chris. Tunazungumza. Sijui kama itawezekana kwa sababu hali ilivyo kule Manchester United, lakini ningependa sana kumuona Chris akibakia hapa kwa sababu ni mtu muhimu.

Mkhitaryan, mchezaji mwenzake wa zamani Smalling pale United, amekumbwa na majeruhi kwa kipindi chake alichokaa hapo Roma.





# *Klopp: Mafanikio ya Liver yanavutia wachezaji*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amebainisha mafanikio yamewasaidia mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Liverpool kuvutia wachezaji, lakini "amelia" usajili ni mgumu.

Huku wakiwa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu ya England kwa pointi, Liverpool imekuwa ikihusishwa na usajili wa wachezaji wengi, akiwamo nyota wa RB Leipzig, Timo Werner.

"Ni rahisi kama wachezaji wakiona mafanikio ya klabu. Kama wakikuoa una mafanikio, ni rahisi kufanya mazungumzo na wachezaji," amesema akinukuliwa na magazeti ya Uingereza.

"Lakini kwa upande mwingine, ni ngumu kwa timu bora kupata wachezaji wapya kwa sababu watauliza maswali kama, 'nitacheza wapi na lini?'

"Tunawahitaji wachezaji ambao wanataka kuwa sehemu ya timu hii, ambao wanataka kupigania namba na mabao wapo tayari kwenda hatua nyingine na sisi na kujiimarisha wao wenyewe.

Liverpool bado haijafungwa kwenye Ligi Kuu ya England na jana usiku ilikuwa ikicheza na West Ham kwenye dimba la Anfield.

# Solskjaer amfananisha Fernandes na Scholes, Veron

**MANCHESTER,** England

KIWANGO cha Bruno Fernandes kwenye ushindi wa Manchester United wa 3-0 dhidi ya Watford kimemfanya kufananishwa na Paul Scholes na Juan Sebastian Veron, wakati Ole Gunnar Solskjaer akisifia ubora wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno.

Solskjaer amebainisha kuona uwezo wa Veron na Scholes katika uchezaji wa Fernandes ambaye alifunga bao la kwanza kwa mkwaju wa penalti kabla ya Anthony Martial kufunga la pili la Mason Greenwood la tatu.

Ushindi huo ulikuwa wa kwanza kwa Fernandes hapo Old Trafford tangu atue hapo akitokea Sporting CP, na Solskjaer amesema uchezaji wake tangu amejiunga na klabu hiyo kuimeimarisha safu ya kiungo na ushambuliaji.

"Katika soka la sasa, nafikiri tumapata mtu," amesema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari. "Amekuja na kutupa nguvu timu.

"Ina maana kubwa zaidi ya kupata mchezaji. Unaweza kuona hata mashabiki walionesha kuridhishwa na kiwango chake.

"Na ukimwangalia sana unaona staili ya Scholes na Veron. Ana kiwango cha Veron na ubora wa Scholesy. Ni kiungo mzuri na mwenye uwezo mkubwa. Anafanya kila kitu kinafanana na Veron na Scholes."






# GUARDIOLA ATAKA KUWAIGA REAL MADRID

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amewataja Real Madrid kama wafalme wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati kocha huyo wa zamani wa Barcelona akijiandaa kuiongoza timu yake ya Manchester City dhidi ya klabu hiyo anayotaka kuiiga.

City watasafiri kwenda pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu leo kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16, dhidi ya vijana hao wa Zinedine Zidane.

Madrid imetwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya mataji manne kati ya misimu sita iliyopita na ina wachezaji wengi ambao wameshinda taji hilo, huku Claudio Bravo na Scott Carson wakiwa ndio wachezaji pekee wa City kushinda taji hilo.

Guardiola amewaambia waandishi wa habari: "Ninavutiwa sana na klabu hii.

"Wachezaji waliocheza pale wamecheza mara nyingi mno kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na sijui wameba mara ngapi.

"Pengine Claudio (Bravo) ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na mchezaji mwingine. Hatuna wachezaji wengi walioshinda taji hili. Lakini tunahitaji kushinda.

"Lakini tunatakiwa kucheza kwa staili yetu kwa dakika 180 dhidi ya Real Madrid. Kwa uhakika kabisa, utakuwa mchezo wa kuvutia."

# *Cavani afunga bao la 200 PSG*

**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani, alifunga bao lake la 200 kwa klabu hiyo katika mashindano yote wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1 dhidi ya Bordeaux Jumapili.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye alisherehekea kutimiza umri wa miaka 33 mwezi huu, alisawazishia PSG kwa bao la kichwa akiunganisha pasi ya Angel Di Maria.

Lilikuwa ni bao la saba la Cavani msimu huu kwa PSG, huku akiwa amepoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha kocha, Thomas Tuchel.

Cavani alijiunga na PSG akitoka kwa miamba wa Italia, Napoli Julai 2013 na anatarajiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa mwezi huu.

Alikuwa mfungaji wa wakati wote wa PSG, Januari 2018 wakati alipoipiku rekodi ya Zlatan Ibrahimovic aliyefunga mabao 156.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: NITAMSHAWISHI AUBAMEYANG ABAKI

Asema klabu itafanya kila linalowezekana ili asiondoke Emirates kwa sababu ya...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ana matumaini ya kumshawishi Pierre-Emerick Aubameyang kubakia na klabu hiyo baada ya mshambuliaji huyo kufunga mabao mawili yaliyoiwezesha kuibuka na ushindi 3-2 dhidi ya Everton, Jumapili.

**Mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 30 amekuwa akihusishwa na klabu nyingine ikiwamo Inter Milan na Barcelona, na anakaribia mwaka wa mwisho wa mkataba wake.**

Huku kukiwa na nafasi ndogo mno ya Arsenal kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya mismu ujao, halitakuwa jambo la kushangaza kumuona Aubameyang akiamua kwenda sehemu nyingine kumaliza kipindi chake cha uchezaji.

Lakini washika bunduki hao wanamuona mchezaji huyo kama mtu muhimu zaidi kwenye kikosi chao na mabao yake mawili aliyoyafunga dhidi ya Everton yalithibitsha ubora wa thamani yake kwa timu, kwa mujibu wa Arteta.

"Yeye ni mchezaji wetu muhimu," alisema Arteta akiiambia Sky Sports. "Takwimu zake hazina maswali na umuhimu wake kwa timu ni mkubwa, hivyo nitafanya kila niwezalo kuhakikisha klabu inamshawishi abakie na sisi."

Arteta alishukuru molari ya timu baada ya kupata ushindi mara tatu ndani ya wiki, wakiwafunga Newcastle United 4-0 Jumapili iliyopita na wakapata ushindi wa 1-0 dhidi ya Olympiacos Alhamisi iliyopita kwenye mchezo wa Ligi ya Europa.

Aubameyang alifunga bao hilo la ushindi kwa Arsenal sekunde 24 baada ya kipindi cha pili kuanza.

"Kitu bora ni molari iliyoonyeshwa na timu. Tumetoka kwenye mechi ya Ulaya, mechi tatu ndani ya siku saba, baada ya kuruhusu bao dakika ya kwanza, waliamua kucheza kwa bidii," alisema Arteta.

"Kwa uhakika kabisa timu ilionesha kile nilichokitaka, walicheza kwa kujituma na tukapata ushindi tuliouhitaji, na naamini mechi zinazofuata zitakuwa kwenye ubora kama wa leo (juzi).

"Tumeingia kwenye kipindi kigumu zaidi kuelekea mwishoni mwa msimu, hivyo tulilazimika tucheza kwa kujituma zaidi kuhakikisha tunapata ushindi katika kila mchezo."

## ZISIKUPITE

### ABADILI MKATABA MILAN

MKURUGENZI wa ufundi wa Klabu ya AC Milan, Paolo Maldini, amesema Zlatan Ibrahimovic, mwenye umri wa miaka 38, amefanya marekebisho ya kipengele cha mkataba wake wa kuendelea kuichezea klabu hiyo kama itafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Daily Mail)***

### ROMA KUTOA MIKATABA

KOCHA wa AS Roma, Paulo Fonseca anataka kuwasajili kwa mikataba ya kudumu wachezaji Chris Smalling wa Manchester United mwenye umri wa miaka 30- ambaye ni mlinzi wa England, na kiungo wa kati wa Arsenal raia wa Armenia, Henrikh Mkhitaryan, mwenye umri wa miaka 31. ***(Sky Sports)***

### WAMGOMEA NYOTA LEEDS

KLABU za Wolves na Burnley zipo tayari kukabiliana na Sheffield United kwa ajili ya kumpata kiungo wa kati wa Leeds United, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 24 ambaye ni raia wa Uingereza. ***(Daily Star)***

### TUCHEL ATAKIWA MUNICH

KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel ameripotiwa kuwa kwenye mazungumzo na Bayern Munich kwa ajili ya kumrejesha katika nchi yake ya asili ya Ujerumani kuwanoa miamba hao wa Bundesliga. ***(90 Min)***

### BARCA YAMNYATIA KINDA

BARCELONA wapo kwenye mikakati ya kuhakikisha kwamba wanamasajili beki wa kushoto, Hugo Guillamon kutoka Valencia mwenye umri wa miaka 20. ***(Sport)***

### C. PALACE KUMSAJILI KOSTIC

KLABU ya Crystal Palace wanamsaka mchezaji wa klabu ya Eintracht Frankfurt, Filip Kostic kama mchezaji mbadala wanayeweza kumlipa pauni milioni 10 alizokuwa akilipwa, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 27. Winga huyo wa kimataifa wa Serbia kuna wakati pia alitakiwa na Liverpool. ***(The Sun)***

### MBIO MOJA KWA TUCKER

KLABU za Aston Villa na West Ham zipo kwenye mbio moja kumwania mchezaji aliyethamanishwa kwa viwango vya juu na klabu ya Gillingham, Jack Tucker mwenye umri wa miaka 20 anayecheza nafasi ya mlinzi wa kati. ***(Birmingham Mail).***

### HATAKI KUONDOKA MAN UTD

KIUNGO wa Manchester United na Serbia, Nemanja Matic mwenye umri wa miaka 31, anakata kubakia pale Old Trafford baada ya mkataba wake wa sasa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sunday Mirror)***

### FODEN AFURAHIA KUBAKI CITY

MCHEZAJI kinda wa Manchester City, Phil Foden mwenye umri wa miaka 19, amebainisha kwamba anafurahia kubakia katika klabu hiyo badala ya kupelekwa sehemu nyingine kucheza kwa mkopo. ***(Manchester Evening News)***

### CHELSEA YAJITOSA KWA ICARDI

KLABU ya Chelsea imeonesha nia ya kutaka kumsajili nyota wa Inter Milan, Mauro Icardi, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo pale yuko Paris St-Germain na huenda wakatupa ofa yao kipindi cha majira ya joto. ***(Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

# Simba kuivaa Stand kombe la FA leo

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Simba leo inashuka dimbani kuvaana na Stand United kwenye mchezo wa kombe la Shirikisho, mchezo ambao utachezwa mkoani Shinyanga huku wakiahidi kuendeleza ushindi.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana akiwa njiani kuelekea Shinyanga, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alisema wachezaji wote wapo vizuri kuelekea katika mchezo huo ambao ameutaja kuwa na ushindani mkubwa.

"Nashukuru hadi sasa wachezaji wote wanaendelea vizuri, hatuna majeruhi zaidi ya Athumani Miraji ambaye yupo kwenye usimamizi wa daktari kutokana na matibabu yake na kocha amesema hatafanya mabadiliko yoyote katika mchezo huo," alisema Patrick.

Hata hivyo, aliongeza kusema mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na kuwa mara nyingi wanapokutana na timu ndogo hukamiwa vikali na kuwataka mashabiki pamoja na wanachama wao waendelee kuwasapoti ili waweze kusonga mbele katika michuano hiyo.

Aidha, alisema kwa mujibu wa kocha ameahidi kuendeleza ushindi katika michuano hiyo pamoja na mechi zijazo za Ligi Kuu zilizopo mbele yao.

Aidha, alisema kikosi chao kinawaridhisha kutokana na umakini wanaoufanya uwanjani kwa kupata matokeo mazuri.

Simba inaingia kwenye mchezo huo ikitoka kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya Biashara United.

# Mashindano ya Gofu Lugalo

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali mstaafu Michael Luwongo ametangaza mashindano ya Tanapa Lugalo Open yanatarajiwa kufanyika Machi 14 na 15 mwaka huu katika Viwanja vya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti huyo ameliambia Nipashe kuwa mashindano hayo yalikuwa yafanyike Februari 29 na Machi Mosi, lakini kutokana na baadhi ya maandalizi kutokamilika imelazimu sasa kusogezwa mbele.

"Tumesogeza mbele ili kutoa fursa ya wachezaji wengi kutoka maeneo mbalimbali kuweza kufanya maandalizi na kushiriki hasa kwa wachezaji wanaotoka katika vilabu mbalimbali nje ya Dar es Salaam," alisema Brigedia Luwongo.

Aidha, alisema pia mgeni rasmi katika ufungaji wa mashindano hayo anatarajiwa kutangazwa baadaye katika mkutano na waandishi wa habari baada ya kuthibitisha kuwapo katika mshindano hayo kulingana na ratiba zake.

Kwa upande wake Nahodha wa Klabu ya Lugalo, Kapteni Japhet Masai, alisema tayari taarifa zimeshatumwa kwa manahodha wa vilabu mbalimbali na dirisha limeshafunguliwa kwa yeyote anayetaka kushiriki kuweza kujiandikisha.

# MGUNDA ALIA WASHAMBULIAJI KUIKOSA YANGA MKWAKWANI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema kutokuwa makini kwa safu yake ya ushambuliaji ndiko kulikosababisha kushindwa kupata matokeo na kuambulia suluhu dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga juzi.

Coastal ikisaka ushindi mbele ya Yanga kipindi cha pili ilimiliki zaidi mchezo na kutengeneza nafasi nyingi ambazo walishindwa kuzitumia kupata matokeo na kufanya wagawane pointi moja moja.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda alisema wachezaji wake walipambana huku safu yake ya ulinzi ikifanya vizuri, lakini washambuliaji waliwaangusha.**

Alisema uimara wa wapinzani wao Yanga, pia ni jambo lililowafanya wapambane kutafuta matokeo licha ya kuambulia sare ya bila kufungana.

"Washambuliaji wangu hawakuwa makini, tumekosa nafasi nyingi za wazi, hii ni kukosa utulivu kwa wachezaji wangu," alisema.

Naye nahodha wa Coastal, Bakari Nondo, alisema haikuwa bahati yao kuibuka na ushindi mbele ya Yanga.

"Tulipambana ili kutafuta matokeo na bahati haikuwa yetu, kushindwa kushinda si mwisho wa mapambano, tutajipanga kwa ajili ya mechi zetu zinazofuata," alisema.

Matokeo hayo yanaifanya Coastal Union kufikisha pointi 39 ikiwa nafasi ya tano nyuma ya Yanga yenye alama 41 baada ya mechi 22, michezo miwili nyuma ya 'Wagosi wa Kaya' hao.




Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, akimkabidhi kombe Kapteni wa Timu ya Mpira wa Kikapu ya Benki ya CRDB, Nibert Chaula, baada ya kuibuka na ushindi dhidi ya Baraza la Wawakilishi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Zimamoto yajipanga kubeba pointi mechi zote*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Zimamoto licha ya kupunguzwa kasi ya kuukaribia ubingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar kwa kutoa sare katika michezo yake ya hivi karibuni, imeahidi kupata alama tatu katika michezo yake itakayoanzia leo.

Zimamoto ipo nafasi ya 4 ikiwa na alama 29 katika msimamo wa Ligi Kuu ya Zanzibar yenye timu 16, huku JKU ndio kinara wa ligi hiyo ikijikusanyia alama 34.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Timu ya Zimamoto, Ali Ussi, maarufu Jongo alisema mzunguko wa lala salama unakuwa mgumu, kwa sababu timu zote zinaonesha upinzani mkali.

Alisema hivi sasa kila timu inahitaji kupata alama tatu, huku baadhi ya timu kutoa sare ni kama ushindi kwao kutokana na ugumu wa ligi katika mzunguko huu wa kumalizi msimu.

Aidha, alisema Zimamoto imejipanga kuhakikisha michezo yake yote kuanzia leo wanaondoka na alama tatu, ili timu yake hiyo iweze kujisogeza kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ambayo haina udhamini.

"Tumetoa sare nyingi karibu michezo yote tuliyocheza katika mzunguko huu, lakini haimaanishi kama tumepoteza matumaini ya kuchukua ubingwa, hapana. Matumaini yetu ya ubingwa yapo pale pale na tayari tumeshayafanyia kazi baadhi ya mapungufu katika kikosi chetu ninaamini michezo inayofata tutatoka na ushindi," alisema.

Zimamoto inatarajia kushuka dimbani Februari 29 ikiumana na maafande wa Polisi katika uwanja wa Mau A hapa visiwani Zanzibar.

# Michezo

Jumanne Februari 25, 2020

Nipashe




Arteta: Nitamshawishi Aubameyang abaki

UKURASA 30



Mchezaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin (kushoto), akipambana na mabeki wa Arsenal wakiongozwa na David Luiz wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya England baina ya timu hizo kwenye uwanja wa Emirates juzi Jumapili. Arsenal ilishinda mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga: Hesabu sasa kwa Azam si Simba

## ●●● Pumzi yatajwa tatizo, Eymael asema hawafikirii tena kuwashika vinara hao, bali…

**Na Isaac Kijoti,** TANGA

WAKATI 'kukata pumzi' katika kipindi cha pili kukielezwa ni moja ya tatizo linalochangia Yanga kushindwa kupigania ushindi, timu hiyo imekiri kwa sasa inawazia kuishika Azam FC na wala si Simba iliyopo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa sasa.

**Yanga juzi ilipata sare ya nne mfululizo baada ya kutoka suluhu na Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.**

Hiyo ni baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City, suluhu dhidi ya Tanzania Prisons mechi zote zikipigwa Uwanja wa Taifa kabla ya kwenda kutoka sare ya 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi. Na kwa matokeo hayo, yanaifanya Yanga sasa kufikisha pointi 41 baada ya mechi 22, ikiwa ni alama 21 nyuma ya vinara Simba na nne nyuma ya Azam FC iliyopo nafasi ya pili.

Hata hivyo, Simba na Azam zipo mechi mbili mbele, lakini katika nafasi ya tatu kuna Namungo FC yenye alama 43 baada ya mechi 23. Wigo huo wa pointi za Simba, umemfanya Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, kuweka wazi kwanza hesabu zake kwa sasa ni kuifikia Azam FC kwanza na si vinara hao.

Akizungumza baada ya mechi ya juzi, Eymael alisema anaiwazia Azam na hesabu zake kwa sasa si pointi za Simba.

"Kwanza nawazia kuishika Azam katika nafasi ya pili kwa sasa si Simba," alisema Eymael huku akiahidi kuendelea kuisuka safu yake ya ushambuliaji.

"Bado washambuliaji wanashindwa kutumia nafasi tunazozitengeneza, lakini pia ujanja ujanja wa wapinzani wetu uwanjani vyote hivyo vinachangia kutopata matokeo."

Pamoja na maoni hayo ya Eymael kuhusu safu ya ushambuliaji, wachambuzi wa soka, wanaeleza Yanga inaonekana kukata pumzi katika kipindi cha pili.

"Mechi ambayo Yanga ilionekana kuhimili kwa dakika 90 ilikuwa wakati ikiwa chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa dhidi ya Simba baada ya hapo inashinda kwa shida.

"Ikikukosa kipindi cha kwanza, basi timu pinzani ikikomaa na kucheza mpira wa kasi inashinda, si suala la washambuliaji tu kukosa umakini, bali hata pumzi kwa timu ni tatizo," mchambuzi Emily Collins aliliambia Nipashe.

Kwa hesabu za Eymael, kama Yanga itashinda viporo vyake viwili itafikisha pointi 47 huku Namungo nayo ikishinda kiporo chake itafikisha pointi 46, hivyo zitaipiku Azam FC yenye pointi 45.

Na kwa hesabu hizo, Yanga bado itakuwa na mlima mrefu wa pointi 15 nyuma ili kuifikia Simba kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 20.

Yanga tayari imerejea jijini Dar es Salaam na inaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Gwambina FC utakaopigwa Uwanja wa Taifa kesho.

# Sven ataka ukuta wa 'zege' Simba

**Na Saada Akida**

WAKATI leo wakishuka Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga kuivaa Stand United kwenye mechi ya Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck anataka 'kuona ukuta wa zege'.

Hiyo ni baada ya kushuhudia mabeki wake wakiruhusu bao moja wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Jumamosi.

Akizungumza na Nipashe jana, Sven alisema kujisahau kwa mabeki wake kumejitokeza tena baada ya awali kuonekana kulimaliza tatizo hilo jambo ambalo anataka kulimaliza.

"Tunahitaji ushindi, lakini mabeki wanatakiwa kuwa makini kuhakikisha wapinzani hawapati nafasi ya kufunga," alisema Sven.

Alisema anahitaji kuona wanapata ushindi, lakini na mabeki nao wakiwa makini na kuhakikisha wanawazuia wapinzani wasifunge.

Kocha huyo alisema tayari amefanyia kazi upungufu uliyojitokeza kwenye mchezo uliopita na anaamini watafanya vizuri katika mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Stand United leo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >